

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 31 Julai, 2009

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Majibu ya Serikali juu ya Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):

Majibu ya Serikali juu ya Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC).

Majibu ya Serikali juu ya Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC).

MASWALI NA MAJIBU

Na. 314

Kuviwezesha Vyuo vya Elimu Nchini

MHE. PINDI H. CHANA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inapaswa kuviwezesha Vyuo vya Elimu nchini vikiwemo Chuo cha Mzumbe na Muhimbili kwa mujibu wa Kanuni na Sheria:-

(a) Je, ni matatizo gani yanayosababisha Serikali kushindwa kuviwezesha Vyuo tajwa hapo juu kwa viwango ambavyo Wizara yenyewe imethibitisha?

(b) Je, Serikali ilipaswa ipeleke kiasi gani cha fedha kwa mwaka 2007/2008 na 2008/2009 Chuo cha Muhimbili na Mzumbe ambazo iliahidi na haikupeleka?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali huvipelezha Vyuo Vikuu vya Umma vikiwemo Vyuo Vikuu vya Mzumbe na Muhimbili kwa kulipa mishahara ya watumishi, matumizi mengineyo (OC), pesa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, pamoja na mikopo ya wanafunzi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilivipelekea fedha Vyuo Vikuu vya Mzumbe na Muhimbili kama zilivyooneshwaa katika juzu la pili na la nne ya bajeti ya mwaka 2007/2008 na 2008/2009.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, nina maswali madogo mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri. Kwa kuwa fedha zilizopokelewa na Chuo cha Muhimbili na Mzumbe kwa mwaka 2007/2008 na 2008/2009 si kama ilivyoelezwa katika juzu la pili na la nne la bajeti; Waziri atakubaliana nami kwamba nimwone baadae ili tuweze ku-reconcile nikiwa kama *Council Member* wa Muhimbili?

Pili, kutokana na upungufu wa fedha ambazo zinapatikana katika Vyuo hivi kupelekea Vyuo kuongeza ada na wakati mwininge huongeza ada pasipokuwasiliana na Bodi ya Mikopo. Wizara itakubaliana na ushauri wangu kwamba vyuo vyetu vya umma vinapotaka kuongeza ada ni vyema vikawasiliana na Bodi ya Mikopo kwa sababu mikopo ni lazima itarudishwa?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa nafasi hii na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu zuri.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, fedha kwa ajili ya kuendesha Vyuo Vikuu vyetu vya Umma kwa kweli ni finyu. Ndio maana Serikali imefanya juhudu kubwa ya kutengeneza Mradi wa Kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ualimu katika Vyuo Vikuu vyetu vya Umma, ambavyo vimeanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha uliopita na utaendelea katika mwaka huu na kwamba, Serikali pia imetengeneza Mradi wa Maendeleo wa Vyuo Vikuu (MMETU), ambao uko sawasawa na MMES na MMEM ili kuondoa upungufu ambao upo katika Vyuo vyetu Vikuu vya Umma.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili litaondoka na matatizo yaliyoko Muhimbili pamoja na Mzumbe yataondoka.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja tu la nyongeza na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Niseme tu kwamba, mimi ni Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dodoma, kwa niaba ya Bunge hili.

Swali langu linahusiana na suala la matumizi mengineyo (OC). Utakuta chuo kama Chuo cha Ardhi chenye wanafunzi 1,200 kinapata OC mara mbili kuliko Chuo Kikuu cha Dodoma, ambacho ifikapo Novemba kitakuwa na wanafunzi 17,000. IFM inapata fedha nyingi zaidi na matumizi mengineyo kuliko Chuo Kikuu cha Dodoma. Kwa nini jambo hili la mgawanyo wa matumizi mengineyo halizingatii majukumu halisi ya chuo husika?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna tofauti hizo ndogo katika mahitaji na katika mgawanyo wa fedha. Mheshimiwa Mbunge, angekwenda katika Chuo Kikuu cha Ardhi, akaangalia hali halisi ilivyo pale kwenye Chuo Kikuu cha Ardhi, angekubaliana kwamba fedha walizopewa wala hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuvihudumia Vyuo vyetu Vikuu ili kuhakikisha kwamba, elimu bora inayotolewa inakuwa bora zaidi.

Na. 315

Kuwasaidia Wavuvi wa Ziwa Kitangili

MHE. JUMA H. KILLIMBAH aliuliza:-

Kwa kuwa Ziwa Kitangili hivi sasa linakabiliwa na matatizo kama vile upungufu wa kina cha maji na ukosefu wa Wataalam wa Uvuvi; na kwamba Serikali Wilayani Iramba imeshindwa kumudu shughuli za Maendeleo ya Uvuvi katika ziwa hilo:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kutoa Wataalam wa Uvuvi ili washirikiane na Wavuvi wa Kitangili katika mafunzo ya uvuvi bora?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuwajengea Vituo Maalum Wavuvi ili mara wanapomaliza kuvua watumie vituo hivyo kupumzika?

(c) Je, Serikali itasaidia kujenga Ofisi ya Afisa Uvuvi katika eneo la Doromoni badala ya kumtumia Afisa kutoka Kiomboi ambaye huja Kitangili mara moja kwa mwezi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvubi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa mafunzo kwa wavuvi wadogo kwenye maeneo ya uvubi nchini. Mafunzo haya, hutolewa kwa awamu kwa kuzingatia uwezo wa kifedha. Wavuvi wa Ziwa Kitangili ni baadhi ya wavuvi walionufaika na utaratibu huo wa mafunzo, ambapo mwezi Februari, 2004 jumla ya wavuvi 257 kutoka vijiji vinne vya Doromoni, Shauritanga, Tulya na Geta, walipewa mafunzo ya uvubi. Mafunzo hayo yalihusu matumizi ya zana bora za kisasa za uvubi, sheria za uvubi na athari zitokanazo na uvubi haramu. Mafunzo yalifanyika kwa ushirikiano kati ya Wizara yangu na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba na ni nia ya Serikali kuendeleza utaratibu wa kuwapatia mafunzo wavuvi katika maeneo yote ya uvubi kama nilivyoeleza.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga vituo viwili maalum, kwa ajili ya wavuvi wa Ziwa Kitangili kupumzika baada ya kutoka kuvua. Katika mwaka 2009/2010, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, imetenga shilingi 5,600,000 kwa ajili ya kujenga Vituo Maalum vya kupumzika wavuvi vya Doromoni na Shauritnga. Pamoja na kazi nyingine, vituo hivyo pia vitatumika kuboresha uvunaji, uchakataji na uhifadhi wa mazao ya uvubi.

(c) Mheshimiwa Spika, katika eneo la Doromoni, kuna ofisi na nyumba za kuishi Maafisa wa Serikali. Aidha, imeajiri wataalam wawili wa uvubi, mmoja tarehe 1 Mei, 2007 na mwingine tarehe 1 Juni, 2009. Wataalam hao; mmoja ana Stashahada (*Diploma*) ya Uvubi toka Chuo cha Uvubi Kunduchi na mwingine ana Astashahada (*Certificate*) toka Chuo cha Uvubi Nyegezi. Watumishi hawa wameajiriwa kama Maafisa Uvubi wa Kitangili na wanaishi hapo hapo Doromoni katika nyumba za Serikali na ninaamini watasaidia kuendeleza shughuli za uvubi katika eneo hilo.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kabla sijaauliza maswali, ningombaa yafanyike masahihisho kidogo ili kuweka kumbukumbu vizuri. Wakati wa majibu, kipengele (a) Mheshimiwa Naibu Waziri anasema, vijiji vinne na amevitaja Doromoni, Shauritanga, Tulya na Geta. Ninacheweza kusema ni kwamba, Shauritanga na Geta ni Vitongoji, kwa hiyo, vijiji ni viwili tu. Sasa nakuja kwenye swali.

La kwanza; je, Mheshimiwa Waziri au Naibu wake watakuwa tayari kuja kutembelea hasa kule sehemu ya Tulya ambako ndiyo Kata yenyewe ya Tulya ili waje katika Ziwa Kitangili na wajionee ile hali halisi badala ya kuzungumzia kinadharia kama hivi anavyonijibui?

La pili, katika hii hesabu anayosema shilingi 5,600,000, mimi naona ni fedha ndogo sana kwa vituo viwili. Pamoja na hali halisi inayoendana na nyumba hizi ambazo zimetajwa, wanazoishi hawa maafisa; je, Wizara iko tayari kuweka nyongeza ya fedha

zikawa nyingi kidogo ili kuweza kurekebisha pamoja na nyumba ambazo zimechoka wanazoishi hawa maafisa kule kwenye Ziwa Kitangili?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, hatuna tatizo, mimi na Mheshimiwa Waziri, tutapanga kufuatana na nafasi iliyopo ili tuweze kutembelea na kuona hali hiyo. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hilo litawezekana ili tuweze kutembelea na kuona hali ilivyo katika Kijiji cha Tulya.

Kuhusu shilingi 5,600,000 kwa ajili ya kujenga vituo viwili; kweli ni ndogo. Tuliwasiliana na Halmashauri, wakasema kazi hii itafanyika kwa awamu. Kwa hiyo, mwaka huu wametenga fedha, zitafanya kazi na mwaka kesho naamini watatenga fedha zaidi za kumalizia kazi.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa vile swali la msingi limezungumzia kina cha maji kupungua, ambayo nahisi sehemu kubwa inatokana na tope kujaa kwenye ziwa hilo na nalifahamu. Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba kuna umuhimu wa Wizara hii kuchukua hatua au nibadilishe swali; kwa nini Serikali haichukui hatua ya kusimamia matumizi ya ardhi kwenye kidakamaji (*catchment*) ili kuzuia tope lisiendelee kujaa kwenye maziwa kama haya?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, watu wameachiwa wanalima mpaka karibu na vyanzo vya maji na kukata miti na kuharibu mazingira. Nafikiri ni Sera ya Serikali kwamba, wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri zao na Serikali Kuu, wahakikishe kwamba, hawaharibu hivyo vyanzo vya maji; na hivyo basi, wasilime karibu sana kufikia ziwa; na vile vile wasikate miti na hatua nyingine zichukuliwe kama inalazimu kupanda miti ili kuzuia mmonyoko wa udongo ambaa unasababisha maji kukimbia na kuchukua mchanga kupeleka kwenye maziwa.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Ziwa Kitangili linaungana na Mto Sibiti unaotoa samaki, unalisha Iramba Mashariki sehemu ya Karatu, Mbulu na Singida Kaskazini. Je, Waziri atakuwa tayari wakati akitembelea Kitangili aende na Mto Sibiti kutoa elimu na vile vile kuwatafutia zana za kisasa za uvuvi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, wakati tutakapotembelea hili Ziwa, hatutafika pale tu na kurudi. Kwanza, tutapenda kukagua shughuli za mifugo na vile vile kutembelea sehemu za vyanzo vya maji kama huu Mto Sibiti. Kwa hiyo, namhakikishie Mheshimiwa Msindai kwamba, tutakapokwenda pale, tutamwarifu na tutaungana naye kwenda kutembelea huo Mto na kuangalia namna tunavyoweza kuwasaidia wavuvi.

Kupeleka Umeme wa Grid Katika Mji wa Songea

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Songea umekuwa ukikabiliwa na ukosefu wa umeme mara kwa mara kutokana na hitilafu ya mashine ya kufua umeme; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikiahidi Bungeni kuwa kuna juhud za kupeleka umeme wa gridi wa kilovoti 132 kwa msaada wa SIDA (Sweden):-

- (a) Je, mpango huo unatarajiwa kuanza lini?
- (b) Je, ni hatua zipi zimefikiwa hadi sasa?
- (c) Kwa kuwa *Line* hiyo haikuoneshwa wakati wa kujadili *Master Power Plan*; je, marekebisho hayo yamehusishwa kwenye mpango huo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Mji wa Songea umekuwa ukikabiliwa na ukosefu wa umeme mara kwa mara, kutokana na uchakavu wa mitambo na uhaba wa vipuri kwa ajili ya kuifanyia matengenezo mitambo hiyo. Hali hiyo inatia huzuni kwa kuwa wananchi wanapata tabu, lakini kazi za matengenezo zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2009.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, ahadi ya Serikali ya kupeleka umeme wa Gridi wa msongo wa kilovoti 132, bado ipo pale pale. Mpango huu unahusisha ujenzi wa njia kuu ya usafirishaji umeme kutoka Makambako hadi Songea, yenye urefu wa kilomita 250, ujenzi wa vituo vya kusambaza umeme (132/33kV) Songea na Madaba na ujenzi wa kilomita 900 za msongo wa kilovoti 33. Mradi huu utahusisha pia kufikisha umeme wa Gridi Mbinga, Namtumbo, Ludewa, pamoja na vijiji vya njiani. Upembuzi yakinifu wa mradi ulikamilika Juni, 2006 na maombi ya ufadhili wa Mradi wa Dola za Kimarekani 70.4 milioni yalipelekwa SIDA na makubaliano kati ya SIDA na Serikali ya Tanzania kusainiwa mwezi Desemba mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa kupeleka umeme wa Gridi Songea, kwa msongo wa kilovoti 132, umeanza mwezi Desemba, 2008 kwa kusainiwa makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Maendeleo ya Sweden (SIDA). Tangazo la *Expression of Interest* (EoI), lilitangazwa gazetini tarehe 28 Mei, 2009. Kazi zitakazofanyika mwaka 2009/2010 ni kuandaa zabuni za kujenga njia za umeme ya msongo wa kilovoti 132 ya urefu wa kilomita 250 na usambazaji za msongo wa kilovoti 33 zenye urefu wa kilomita 900 kwenye miji na vijiji vya Wilaya za Mikoa ya Iringa na Ruvuma, kuwateua wazabuni watakaojenga njia hizo na kuunganisha wateja zaidi ya 6,800, kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamii na kuanza ujenzi wa Mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2013 na maelezo yake kwenye Kitabu cha Makadirio ya Wizara yetu, ukurasa wa 69.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili *Power System Master Plan* (PSMP), njia hiyo haikuoneshwa kwa sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kwamba, wakati majadiliano baina ya Serikali hizi mbili yako katika hatua za kukamilishwa, Mpango huu wa PSMP ulikuwa ukamilishwe mwishoni mwa mwaka 2007. Mabadiliko yanayotokana na utekelezaji wa Mradi huu, ikiwa ni pamoja na manufaa yanayopatikana kwa mfumo wa umeme na kwa wananchi husika, yameainishwa kwenye maelezo mapana ya Mradi huu wa Makambako – Songea.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri, ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kutoa masikitiko juu ya ucheleweshaji wa jibu la swali hili; kwa kweli lilipangwa toka tarehe 24 halafu likawekwa tarehe 27, Siku ya Bajeti na likaahirishwa bila ya kupewa taarifa yoyote. Pamoja na masikitiko hayo, nashukuru kwa majibu na niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa katika *Power Master Plan* ya umeme huu wa 133 kilovoti, ambao pia katika Mkoa wa Ruvuma tumebahatika kuwa na eneo linaloweza kuchimba mkaa wa mawe na kuweza kuzalisha umeme zaidi ya megawati 400, kama ambavyo mara ya mwisho Mheshimiwa Kayombo alizungumzia katika Jimbo lake; na kwa kuwa umeme huo endapo ungewezeshwa kuzalishwa mapema ungeweza pia kuondoa tatizo ambalo linahitajika katika kuzalisha Chuma cha Liganga; je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami umuhimu wa kuupatia nguvu ya kutosha Mradi huu ili kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa si soko la umeme badala yake inakuwa ni nchi ambayo inaweza ikaiza umeme katika nchi hata za jirani?

(ii) pamoja na gridi hii ambayo tunaitegemea Mkoa wa Ruvuma; kwa kuwa pia kuna mpango wa kuongeza nguvu za umeme yaani kwa kuongeza uzito wa laini katika eneo la kati; na kwa kuwa Singida imejulikana sasa kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa upopo ambao kwa kuusaidia mapema ungesaidia hata kutatua tatizo la Kanda ya Kaskazini kwa kuhakikisha umeme unazalishwa katika sehemu za Kati; je, miradi hiyo ya upopo ya Singida imepewa kipaumbele kwa kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme huu Mradi wa Makaa ya Mawe ambaa ameuzungumzia, upo Jimboni kwa Mheshimiwa Gaudence Kayombo. Kweli makaa ya mawe yamegundulika pale, GSD wanayaafanya kazi, labda niseme tu kwamba, Sheria yetu ya Umeme inaruhusu wawekezaji kuingia na kuwekeza kwenye maeneo hayo ya makaa ya mawe kama ilivyo kwenye vyanzo vingine vyotevyote vya nishati.

Kwa hiyo, nimepokea ushauri wake kwamba, Serikali ifanye kazi ya kutangaza chanzo hicho cha umeme na kusema siyo chanzo hicho tu kuna Mchuchuma, Makaa ya Mawe ya Mbinga, Ruhuji, yote yako maeneo hayo hayo. Kwa hiyo, kusema kweli siyo megawatt 200 tu au 400 za makaa ya mawe ya hapo tu, isipokuwa Kanda nzima ile ikifanyiwa uwekezaji wa kutosha, inaweza ikapatikana hata megawatt 1000 kwa Kanda ile ile tu. Hiyo ni gharama kubwa na inategemea na uwekezaji na nakubaliana naye kwamba, uwekezaji ukifanywa vya kutosha, kwa muda huu wa sasa tutakuwa pia tuna umeme wa kutosha wa kuuza nje. Kwa hiyo, tumeupokea ushauri wenu na tutaufanya kazi, lakini ni maamuzi ya uwekezaji kulingana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la mpango wa kuongeza nguvu tumelisema. Waziri alilisema juzi wakati wa Makadirio ya Fedha. Mimi nililisema, kadiri tutakavyoongeza uzalishaji kwenye maeneo tofauti ya Tanzania, ndio tunapunguza mzigo wa umeme unaokwenda maeneo mengine. Kwa hiyo, kwa kuwa umeme mwangi unazalishwa kwenye Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Singida wakiingiza hata hizo megawatt 15 tu ambazo tunatarajia zitaingia mwaka ujao na maeneo ya Kigoma wakaingiza umeme huo, lakini bahati nzuri umeme wa Kigoma hautegemei gridi, lakini Mkoa wa Mwanza ukiingia megawatt 90 ni kweli kabisa kwamba, *load* itapungua Kusini na kwa hiyo, usambazaji wa umeme kwa Kanda hizo utakuwa na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tumepokea maelezo yake na ndio utaratibu na tunaufanya kazi hivi sasa.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake ya maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Stella Manyanya kama ifuatavyo:-

Kuhusu Mradi wa Ngaka kama tulivyoeleza juzi wakati tunafanya majumuisho ya bajeti yetu; ni mradi ambaa tunautambua vizuri. Kimsingi, kutokana na taarifa zao na tathmini walizofanya sasa hivi; ni mradi unaotarajia kuanza kuzalisha umeme wa megawatt 400 mwaka 2013. Tungependa ifanyike kabla ya hapo na juzi tulikuwa na kikao na hao wawekezaji, taarifa zinatia moyo sana.

Kuhusu Mradi wa Umeme wa Upopo hapo Mkoani Singida, kama tunavyokumbuka, ukisoma *Power System Master Plan* inaonesha kwamba, Mradi ule umeanza kutoa umeme kuanzia mwaka 2015. Tunasema baada ya kuongea na wawekezaji, tunauharakisha ili uanze kutoa umeme mwaka kesho na taarifa za kiutafiti zinaonesha kwamba, unaweza kupatikana zaidi hasa wa megawatt 100 kwa kadiri uwekezaji utakavyokuwa umeongezeka.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza, naomba niipongeze Serikali kwa kutia saini mkataba huu wa Mradi wa Msongo Kilovoti 132 kutoka Makambako, Songea, Mbinga, Ludewa na Namtumbo. Kwa kuwa Wilaya zitakazopelekewa Mradi huu ni Wilaya ya Namtumbo pekee haina umeme kabisa; na kwa kuwa kwa taarifa tulizonazo Namtumbo tunategemea kuwa na mahitaji ya megawatt 11, megawatt 9 katika Mradi wa *Uranium* na megawatt mbili katika mahitaji ya Wananchi wa Wilaya Namtumbo; je, Serikali inaweza kuwaambia nini Wananchi wa Namtumbo kwamba inaweza kuupeleka umeme huu utakapofika Songea kwanza katika Wilaya ya Namtumbo halafu Wilaya nyingine zifuate?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, Mradi wa awali wa Makambako Songea, ulikusudia kupeleka umeme Namtumbo, kwa mahitaji ambayo yamekadiriwa ya Namtumbo kama tulivyosema na kama mwenyewe alivytambua ya megawatt mbili. Pia katika kila upelekaji wa umeme nchi nzima, tunatambua mahitaji ya ziada ya migodi na kadhalika, ambayo inaongeza uzalishaji na inaongeza pia tija na uchumi kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hili la mgao wa umeme, nadhani kwa sasa hivi umeme umepangwa kwamba, ukifika pale utakwenda Mbinga. Labda nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mahitaji yote haya ya umeme ya Namtumbo yamezingatiwa, pamoja na mahitaji ya mkoaa mzima. Kwa hiyo, sipendi kumwambia kama nitapeleka umeme kabla ya Jenista Mhagama, tunaweza tukapata balaa.

SPIKA: Na hiyo ni kujitakia magumu tu maana yake! (*Makofî/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, sasa ni zamu ya Wizara ya Fedha na Uchumi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Kigamboni.

Na. 317

Mpango wa Kupunguza Riba na Kuongeza Mikopo kwa Wananchi

MHE. IDD M. AZZAN (K.n.y. MHE. MWINCHOUM A. MSOMI) aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imedhamiria kupunguza riba za Benki kwa nia ya kuondoa tofauti kubwa iliyopo baina ya riba za kukopesha na riba za kukopa na hivyo kujenga mazingira mazuri kwa wananchi kujiwekea akiba na kupata mikopo:-

- (a) Je, mpango huo umetekelizwa kwa kiasi gani hadi sasa?
- (b) Je, ni mikopo ya kiasi gani imetolewa na benki mbalimbali kutokana na juhudhi hizo?

(c) Je, mwenendo wa uwekaji akiba ukoje na kuna ongezeko la asilimia ngapi kwa wastani katika uwekaji wa akiba Benki?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, biashara ya mabenki iliwekwa huru mwaka 1991, ilipopitishwa Sheria ya Usimamizi wa Mabenki na Vyombo vya Fedha ya Mwaka 1991. Sambamba na Sheria hii, mabenki binafsi yamepewa nafasi ya kupanga riba za huduma inayotolewa kulingana na mazingira ya kiuchumi, ambayo ni ya ushindani. Lengo la kuweka ushindani katika Sekta ya Fedha ni kuhakikisha kwamba, bidhaa na huduma za kibenki na kifedha zinazotolewa kwa wananchi na wateja zinaongezeka, zinatolewa kwa ufanisi na kwa gharama inayobebeka, ikiwa ni pamoja na riba nafuu ya mikopo.

Hivyo, Serikali inaendelea kujenga mazingira ya ushindani na kuimarisha soko la dhamana, kwa lengo la kufikia viwango halisi vya riba visivyobadilika badilika kama njia mojawapo muhimu ya kuongeza ufanisi katika vyombo vya fedha. Kutokana na juhudhi hizo za Serikali, tofauti kati ya riba za amana na riba za mikopo, ilipungua kutoka wastani wa asilimia 10 mwaka 2005 hadi kufikia wastani wa asilimia 5 katika miezi kumi na moja ya mwanzo ya mwaka 2008/2009. Wakati ambapo viwango vya riba kwa wakopaji wa mikopo isiyozidi mwaka mmoja ilishuka kutoka wastani wa asilimia 15.65 mwaka 2005 hadi wastani wa asilimia 13.59, riba ya amana za mwaka mmoja iliongezeka kutoka asilimia 7.26 hadi asilimia 8.39 katika kipindi hicho hicho.

Mheshimiwa Spika, wastani wa riba kwa dhamana za Serikali (*Weighted T-Bill rate*), ulishuka kutoka wastani wa asilimia 14.84 mwaka 2007 hadi wastani wa asilimia 9.1 mwaka 2008 na hadi mwezi Juni, 2009, wastani wa riba katika soko la amana za Serikali ulikuwa asilimia 6.97.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka miwili iliyopita (2007 na 2008), mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 40 kwa mwaka, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 30 miaka miwili iliyotangulia (2005 na 2006). Katika mwaka ulioishia Septemba 2008, mikopo iliongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,288 na kufikia shilingi bilioni 3,945. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 48.5 kwa mwaka, ikilinganishwa na asilimia 35.4 kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2007. Hali kadhalika, katika mwaka ulioishia Mei, 2009, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa shilingi bilioni 4,684.9, sawa na ongezeko la asilimia 32.2 kutoka mwaka ulioishia Mei, 2008.

Mheshimiwa Spika, hali ya uwekaji akiba katika mabenki imekuwa ya kuridhisha, ingawa bado jitihada zaidi zinahitajika katika kuhakikisha kwamba, sekta isiyo rasmi na wananchi vijijini wanachangia katika kasi ya ongezeko la akiba kwenye mabenki na

taasisi za fedha. Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Mei, 2008 hadi Mei, 2009, akiba ya sekta binafsi kwenye benki zetu iliongezeka kwa shilingi bilioni 752.3 hadi kufikia shilingi bilioni 6,162.4. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 13.9 kwa mwaka.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa baadhi ya mabenki binafsi yamekuwa yakitoza riba kwa utofauti mkubwa na mengine yamekuwa yakitoza riba kubwa sana; je, Serikali haioni kwamba sasa wakati umefika angalau kuweka riba elekezi?

(ii) Kwa kuwa Jimbo la Kigamboni limekuwa na wakazi wengi hivi sasa; Wizara haiwezi kusaidia kuzishawishi baadhi ya Benki kwenda kufungua matawi katika Jimbo hilo la Kigamboni?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kama nilivyo sema, kwa sasa ni soko ndilo linaloamua kiwango cha riba ambayo itatozwa na Mabenki ambayo nayo inatokana na kiwango cha riba cha hati fungani za Serikali za mwaka mmoja, ambayo nayo inatokana na utekelezaji wa Sera ya Fedha na Uchumi.

Kwa hiyo, cha msingi ni kwa kiwango gani ile riba kinachotokana na amana za Serikali za hati fungani, zinakua elekezi kwa Mabenki ya Biashara na vyombo vingine vya fedha. Tabu mmoja hapa ni kwamba, sera zile za fedha, pamoja na kiwango cha riba za hati fungani za Serikali siyo tu kazi yake kutoa kielelezo ama uelekezi kwa kiwango cha riba ambacho Mabenki na vyombo vingine vya fedha zitatoza.

Kwa swali la pili; mimi naamini hilo litafanyika pale Kigamboni, kama tunavyojua itakapokuwa imejengeka upya kama mipango ya Serikali inavyotuelekeza hivi sasa.

Na. 318

Fedha na Miradi Inayotekelawa na TCRA

MHE KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (K.n.y. MHE. BAKARI SHAMIS FAKI) aliuliza:-

Kwa kuwa TCRA ni moja kati ya Mamlaka zinazokusanya fedha nyingi:-

(a) Je, katika kipindi cha Juni, 2005 - 2008 TCRA ilikusanya fedha kiasi gani?

(b) Je, ni miradi mingapi na yenye thamani kiasi gani imetekelawa TCRA kwa kipindi hicho?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swal la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Serikali inayojitegemea, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Namba 12 ya 2003. TCRA ina mamlaka ya kudhibiti na kusimamia maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano nchini. Majukumu ya Mamlaka ni pamoja na kutoa leseni kwa watoa huduma za mawasiliano na kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kufuatilia utendaji wa makampuni yaliyopewa leseni za kutoa huduma zinazosimamiwa na Mamlaka, kusimamia Masafa ya Taifa ya Mawasiliano, pamoja na kufuatilia na kusimamia matumizi ya huduma za mawasiliano hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa napenda kujibu swal la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kipindi cha Juni 2005 – Juni 2008, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilikusanya jumla ya shilingi 64,384,462,217,00 kutoka vyanzo mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya Mwaka 2003.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Juni 2005 – Juni 2008, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imetekeliza jumla ya miradi 21, yenye thamani ya shilingi 53,116,817,548.00.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri. Nina maswali mawili madogo ya kumuuliza:-

(i) Chombo hiki utendaji wake wa kazi ni wa Kimuungano pamoja na kuwa hakioneshwi waziwazi katika orodha ya mambo ya muungano. Je, anaweza kulieleza Bunge hili linasaidiaje upande wa pili wa Muungano katika kufanya shughuli zake hizi?

(ii) Sijui Mheshimiwa Waziri kama ana habari ya kuwa hiki chombo mara nyingine kinachelewesa baadhi ya vyombo kufungua Radio na vitu vingine kama ilivyotokea kwa Chama cha Wananchi (CUF), ambapo ni miaka miwili na nusu tokea wamepeleka ombi la kufungua radio na kila siku ni danadana. Anasemaje juu ya jambo hili?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, TCRA ni chombo cha Muungano na kwamba, kimekuwa kikisaidia hata upande wa pili wa Muungano na vilevile katika hiyo Bodi tuliyonayo, kuna Wajumbe wanaotoka upande wa pili wa Muungano.

Kuhusu kuchelewesha utoaji wa leseni, hii imekuwa ikitokea pale ambapo Mamlaka lazima ijiridhishe kwamba, masafa ambayo yanatafutwa kweli yapo na kumekuwa kukifanyiwa hii *audit* kwa ajili ya kuwa na uhakika kamili kwamba, masafa hayo yanapatikana. Jambo ambalo linatekelezwa, mara baada ya kuwa na uhakika, basi kunakuwa na urasimu wa kutoa leseni hizo

Na. 319

Jengo la Makao Makuu ya Uhamiaji - Zanzibar

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN aliuliza:-

Kwa kuwa Jengo Jipya la Makao Makuu ya Uhamiaji Zanzibar ambalo linajengwa hivi sasa limeshachukua muda mrefu na jambo hili linaathiri utendaji wa kazi za uhamiaji:-

- (a) Je, ni kwa nini Jengo hilo linasuasua wakati limeshapangiwa bajeti yake hadi kumalizika?
- (b) Kuchelewa huko kwa Jengo hilo kama ilivyopangwa; je, Serikali haioni kuwa itapata hasara kutokana na upandaji gharama za ujenzi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Uhamiaji Zanzibar, ulianza tarehe 28 Juni, 2007 na ultarajiwa kukamilika Desemba, 2008, iwapo fedha za ujenzi huo zingepatikana kama ilivyotarajiwa na kwa wakati. Fedha za ujenzi wa jengo, zinatokana na gawio la asilimia 50 ya makusanyo ya Idara ya Uhamiaji Zanzibar, ambalo kwa sasa hutolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuchelewa kukamilika kwa ujenzi huo, kunaongeza gharama za ujenzi wa Jengo hilo. Kutokamilika kwa jengo hilo, mwishoni mwa mwezi Desemba 2008, kumetokana na sababu za kupanda na kushuka kwa makusanyo ya kila mwezi ya huduma za uhamiaji. Hivyo, kusababisha fedha za ujenzi kulipwa kadiri ya makusanyo na kiwango cha gawio kinavyopokelewa kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na si vinginevyo. Jengo hilo sasa liko katika hatua za mwisho na kama makusanyo yatapatikana kama tunavyotarajia, uwezekano wa kukamilisha na kukabidhi katika mwaka huu wa fedha wa 2009/2010 ni mkubwa sana.

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba makusanyo haya yanasuasua na inaelekea kwamba

jengo hili litachelewa kukamilika; je, Serikali ya Muungano itasaidia vipi ili jengo hili likamilike angalau sherehe za Mapinduzi mwakani tuweze kulikabidhi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba, ujenzi wa jengo hili unategemea sana mapato ambayo yanatokana na makusanyo, lakini makusanyo haya yanakwenda katika Mfuko wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na asilimia 50 ndio inakwenda katika ujenzi wa jengo hilo. Kwa mujibu wa takwimu wa tulizonazo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kiasi cha fedha kilichasalia ili kumaliza jengo, hatuna shaka kwamba katika mwaka wa fedha huu ambaa tuliuanza, jengo hili litakamilika na ningemwomba asiwe na wasiwasi kuhusu hilo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa hata Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Manyoni kina tatizo la kuvuja sana batizake; na kwa kuwa sasa hivi masika yamekaribia; na kwa kuwa ahadi hiyo tulishapewa siku nyingi na Mheshimiwa Bakari Mwapachu alipokuwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii; je, Serikali ina hatua gani za haraka kunusuru Kituo hiki kabla masika haijafika?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, swalii la msingi lilikuwa linahusu majengo ya Uhamiaji Zanzibar, hili swalii la nyongeza ni la Kituo cha Polisi, naona ni vitu viwili tofauti. Namjibu kwamba, katika Bajeti yetu ambayo Bunge limepitisha, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hilo tutalitazama jinsi gani tunaweza kulitatu. Siwezi kumpa jibu la uhakika kwa sasa hivi, kwa sababu nilikuwa sijajiandaa vizuri na swalii lake.

SPIKA: Kwa hiyo, Mheshimiwa Maneno lisiwe tena la Polisi, endelea.

MHE. RAMADHANI A. MANENO: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swalii moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa matatizo ya majengo kwenye Idara ya Uhamiaji ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri vya doria kwenye maeneo ya bahari kama Bahari ya Hindi upande wa Bagomoyo; na kwa kuwa kuna wahamiaji haramu wa kutoka Somalia wanaopitia Bagamoyo kwa maana ya Bahari ya Hindi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea au kuwapa vitendea kazi Watumishi wa Bagamoyo ikiwemo vyombo vya doria nchi kavu na majini ili waweze kukabiliana na wahamiaji haramu kutoka Somalia?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, suala la vitendea kazi na kudhibiti mipaka yetu hususan mipaka ya maji, hasa mipaka ya Bahari ya Hindi, lakini pia tuna mipaka ya kwenye Maziwa. Katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii, ambayo Bunge lako lilipitisha ni kwamba, hii ni sehemu ambayo tumesema tutaifanya kazi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Maneno kwamba, hili ni eneo moja ambalo tutalifanya kazi. Kwa sababu tatizo sio tu wahamiaji haramu, lakini pia kuna tatizo kubwa la biashara ya binadamu, ambayo inafanya kwa kupitia maeneo hayo hayo aliyyotaja na maeneo mengine katika Tanzania kwenda katika nchi za Kusini mwa Afrika.

Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Maneno kuwa, tunajipanga kuona ni vitendea kazi gani tutaweka ikiwa ni pamoja na vyombo vya doria katika Bahari ya Hindi, lakini pia katika sehemu nyingine kama Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na kadhalika.

Na. 320

Wananchi Waliotupia Mawe Msafara wa Rais wa Nchi

MHE. KABWE Z. ZITTO aliuliza:-

Kwa kuwa mnao Mwezi Oktoba, 2008 nchi yetu ilipatwa na tukio la aibu kwa baadhi ya Watanzania kutupia mawe Msafara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Kijiji cha Kanga Wilayani Chunya, tukio ambalo sio zuri kwa utamaduni wetu; na kwa kuwa baada ya tukio hilo kutokea Jeshi la Polisi Mbeya liliwakamata Wananchi wa Kanga na kuwapeleka Kituo cha Polisi Mbeya ambako inasemekana kuwa waliteswa kwa kuwekwa ndani siku sita bila kufikishwa Mahakamani, pia walilazwa kwenye maji baridi kwa muda wa siku tatu:-

(a) Je, ni Sheria ipi katika nchi hii inaruhusu mateso ya aina hiyo kwa watuhumiwa?

(b) Je, Serikali iko tayari kufanya uchunguzi maalum ili kutambua kuwepo kwa mateso na aina ya mateso na kuchukua hatua ipasazo?

(c) Je, kwa nini Mkuu wa Wilaya ya Chunya na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya hawajawajibika mpaka sasa kufuatia tukio hilo wakati ndio chanzo kwa kushindwa kushughulikia malalamiko ya wananchi kufuatia michango yao ya sekondari kuliwa na Viongozi wa Kata?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna Sheria yoyote ya nchi inayoruhusu mtuhumiwa wa uhalifu kuteswa?

(b) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alipokea malalamiko kuhusu kuwepo kwa mateso dhidi ya watuhumiwa wa tukio la kushambulia Msafara wa Rais na kuharibiwa kwa mali ya Serikali. Waziri analifanya kazi suala hilo, kuititia Kitengo cha Malalamiko ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

(c) Mheshimiwa Spika, shauri hili kwa sasa liko Mahakamani, ambapo watuhumiwa tisa wameshtakiwa na tayari mashahidi sita wametoa ushahidi wao. Kesi imesikilizwa mara ya mwisho tarehe 28 Julai, 2009 na imepangwa kuendelea tarehe 24 Agosti, 2009. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, tutoe nafasi kwa Sheria kuchukua mkondo wake. Ni matarajio yetu kwamba, baadaya kesi kusikilizwa, Mahakama itaweza kubaini chanzo cha vurugu hizo.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametamka kwamba, hapa hakuna Sheria yoyote ambayo inawaruhusu Polisi au Maafisa wowote wenyewe uwezo wa kutesa watuhumiwa; na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana sehemu mbalimbali, watu wanaokamatwa wanateswa, wanapigwa kwa ajili ya kutaka watoe ushahidi; Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na sauala hilo la mateso ya wananchi wanapokuwa ni watuhumiwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli hata na sisi tunapata malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba, wakati mwingine wanapata mateso na tumekuwa tunatamka na ninazidi kutamka hapa kwamba, Jeshi letu la Polisi kwa ujumla wake, linafanya kazi nzuri na hii inaweza ikadhibitika kwa hali ya usalama tuliyonayo katika taifa letu. Hiyo haina maana kusema kwamba, wapo wale ambao wanakwenda kinyume na taratibu. Siku zote tumekuwa tunasema kwamba, Polisi wafanye kazi zao kwa kuzingatia weledi na viro vigezo ambavyo ni muhimu na taratibu ambazo ni muhimu.

Niseme kwamba, Serikali haiwezi kuzembea ama kufumbia macho suala la kusema kwamba, raia wao wanateswa na chombo ambacho kipo pale kutazama usalama wao na kulinda mali zao. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Zitto kwamba, *position* ya Serikali ipo wazi na maelekezo ya Serikali yapo wazi. Jeshi la Polisi linajua hivyo, lakini pia si barabara sana kila mara tunalaumu Polisi, kwa sababu zipo kesi na pahala ambapo tunakuta kwamba, wamekiuka taratibu, kweli Sheria inachukua mkondo wake na kuna baadhi ya Polisi ambao wameachishwa kazi na wengine wamepatiwa adhabu kufuatana na utaratibu wao.

Mimi niseme, tuisiwavunje moyo, hiki ni chombo tunachokihitaji kwa usalama wa taifa letu. Kwa hiyo, ipo haja ya kuwa na *balance*, lakini nazingatia kauli ya Mheshimiwa Zitto kwamba, malalamiko hayo yapo; si kwamba ni ya kwake, hata sisi tunayapokea na tunayafanyia kazi.

Na. 321

Kutengeneza Barabara kwa kiwango cha lami

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imedhamiria kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Mwigumbi – Bariadi – Mkula – Lamadi kama ambavyo imeainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005:-

- (a) Je, ujenzi huo umefikia kiwango gani na lini Mradi huo unatarajiwa kukamilika?
- (b) Je, ni kampuni gani ya ujenzi iliyoteuliwa kujenga barabara hiyo?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, iliainisha kuwa Barabara ya Mwigumbi - Bariadi - Mkula hadi Lamadi, yenye urefu wa kilomita 171, ifanyiwe upembusi yakinifu na usanifu. Upembusi yakinifu wa barabara yote, ulikamilika mwezi Oktoba 2007, kwa gharama ya shilingi milioni 215.09. Aidha, kazi ya usanifu imekamilika kwa sehemu ya Barabara ya Bariadi - Mkula - Lamadi (kilomita 71.8), ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2009. Usanifu wa sehemu zote mbili unatarajiwa kugharimu shilingi milioni 710.5.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii, Serikali imeamua kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, ambapo mchakato wa kumpata Mkandarasi wa kazi za ujenzi wa sehemu ya Bariadi hadi Lamadi umeanza mwezi Mei 2009 na inatarajiwa Mkandarasi atapatikana katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha wa 2009/2010.

Mkandarasi wa kujenga sehemu iliyobaki ya Mwigumbi hadi Bariadi, anatarajiwa kupatikana baada ya kukamilisha usanifu wa sehemu hiyo.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Naipongeza sana Serikali ya CCM, kwa kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi. Hii ni historia kwa Wananchi wa Jimbo la Busega na Wilaya ya Bariadi na Maswa. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa ujenzi huu utahusisha fidia kwa baadhi ya mali ya wananchi katika maeneo husika katika Vijiji vya Rutubiga, Mkula, Sapiwi, Tutwa na kadhalika. Je, Serikali imejipanga fidia hii italipwa mapema ili kuhakikisha ujenzi wa barabara hii?

(ii) Kwa kuwa barabara hii inaungana na barabara inayotoka Dutwa, Ngasamo kwenda mpaka Nyashimo. Je, wakati wa matengenezo barabara hii ambayo ni ya Mkoa itatengewa fedha maalum ili kuruhusu baadhi ya magari mazito yaweze kutumia barabara hii wakati barabara hii inafanyiwa matengenezo?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi, napokea shukrani zake kwamba, siyo tu tumetimiza ahadi, bali tumetimiza

zaidi ya kile kilichoahidiwa na Ilani. Ilani iliahidi kufanya upembuzi na usanifu, lakini tunawenda kwenye hatua ya ujenzi kabla ya muda uliotajwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, taratibu za fidia zitatekelezwa kwa umakini ili kuhakikisha kwamba, hakuna utata kwa wananchi ambao wataathirika na ujenzi wa barabara hii. Mwisho, sehemu ya Dutwa mpaka Njashimo, kwa sasa haimo kwenye utaratibu wa ujenzi wa barabara hii. Tutaangalia kile ambacho tutaweza kukifanya ndani ya Bajeti ya mwaka huu wa 2009/2010.

SPIKA: Aah! nimewaona akina Luka wawili; aanze Mheshimiwa Dkt. Luka Siyame, halafu amalizie Ustadhi Lucas Selelii.

MHE. DKT. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika utekelezaji wa Ilani ya CMM juu ya kuboresha miundombinu hapo awali Daraja la Mto Momba kwenye Barabara Mloo - Kamsamba Wilayani Mbozi, lilikuwa lijengwe katika Kijiji cha Kamsamba lakini baada ya utafiti na tathmini ya kina, Daraja hilo sasa hivi limehamishiwa katika Kijiji cha Mkulwe ambapo kwa hivi sasa Wananchi wa Mkulwe wanafurahia lakini Wananchi wa Kamsamba wanaona kuna harufu ya upendeleo na katika hali ya kawaida gharama za ujenzi zinaongezeka; je, Wizara ya Miundombinu inatoa ufanuzi gani kuhusu suala hili?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Siyame kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati wa usanifu na ujenzi wa madaraja, utaalamu unatumika ili kubaini eneo ambalo litaweza kujengwa daraja kwa umakini na kwa mafanikio na kwa gharama nafuu iwezekanavyo. Sina uhakika sasa hivi katika daraja lile ambalo lilikuwa limepangwa kujengwa pale Kamsamba katika barabara hii ya Mloo – Kamsamba, kitu gani kilikuja kugundulika ambacho kimesababisha daraja lisijengwe Kamsamba na badala yake lijengwe katika Kijiji cha Mkulwe. Nitafuatilia hilo ili kufahamu wataalam wametumia vigezo gani kufanya mabadiliko hayo. Imani yangu ni kwamba, wametumia vigezo vytaalamu kuweza kufikia hapo na nitamjibu Mheshimiwa Dkt. Siyame kama ambavyo nitaelimishwa na wataalam.

SPIKA: Hatimaye Ustadhi Selelii; kweli leo umependeza sana Mheshimiwa! (*Makofî*)

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, asalaam Alaykum?

Kwa kuwa barabara hii ya kutoka Mwigumbi – Bariadi – Lamadi ni moja lakini katika maeleo ya Mheshimiwa Waziri amesema itaanza kujengwa kuanzia Lamadi – Nkula – Bariadi; kwa kuwa barabara ikiwa ni moja, sehemu nyingine inaweza kujengwa na sehemu nyingine ikachelewa kujengwa, itachelewesha zaidi maendeleo katika

barabara hiyo hiyo moja; je, ni lini sasa hiki kipande cha Mwigumbi – Bariadi nacho kitaanza kujengwa kama kilivyo kile kingine?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Ustadhi Selelii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la awali kwamba, katika barabara hii ambayo ina urefu wa kilomita 171, Serikali imetimiza zaidi ya ahadi yake ilioitoa katika Ilani ya Uchangazi na kwa sasa imeanza na kipande cha Bariadi –Lamadi, lakini inamalizia usanifu katika kipande cha Mwigumbi – Bariadi; na kama nilivyosema, mara tukimaliza usanifu tutaiweka katika utaratibu wa ujenzi barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtaona tayari muda wa maswali umepita, lakini tunaendelea kidogo ili tuyamalize haya mawili. Wizara hiyo hiyo, swal linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Charlse Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini.

Na. 322

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Ibadakuli

MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA: Aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Ibadakuli Shinyanga unajumuisha upanuzi, kuweka lami katika njia za kurukia ndege na maboresho mengine; ni utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2005; na kwa kuwa Kiwanja hiki ni muhimu kiuchumi kwa Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla:-

Je, kazi hiyo itatekelezwa lini kwa ukamilifu?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Dkt. Charles Ogessa Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga ni moja kati ya viwanja saba vilivyofanyiwa usanifu wa kina, kwa msaada wa fedha kutoka Benki ya Dunia ili hatimaye kiweze kuimarishwa kwa kujenga miundombinu imara na majengo ya kisasa, yatakayokidhi viwango vya Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga Duniani (*International Civil Aviation Organisation - ICAO*). Kwa sasa kazi ya usanifu wa kina ya Kiwanja hicho imekamilika na Mhandisi Mshauri amewasilisha Serikalini, ripoti ya mwisho ya upembuzi yakinifu na usanifu. Serikali kwa sasa imeanza mazungumzo na Benki ya Dunia ili kupata fedha za kujenga Kiwanja hicho, pamoja na viwanja vingine sita kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa Kiwanja cha Ndege cha Ibadakuli - Shinyanga na kwa kutambua hivyo, imekiweka katika Programu ya Kitaifa ya Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uchukuzi (*Transport Section Investment Programme*). Chini ya Mpango huu, Kiwanja cha Ibadakuli ni moja ya miradi inayotafutiwa fedha za kukiendeleza chini ya Mpango huo. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, imetenga jumla ya shilingi milioni 150 kwa ajili ya matengenezo ya njia ya kurukia na kutua ndege (*runway*). Matengenezo haya, yatawezesha Kiwanja kuendelea kutumika kwa usalama wakati Serikali ikiendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kama nilivyoeleza.

MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kupitia Waziri huyu msikivu. Pamoja na majibu hayo mazuri, kwa jinsi hiyo nina maswali mepesi ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba iko haja ya kuwafidia Wananchi wa Ibadakuli walioguswa na upanuzi na uboreshaji wa Kiwanja hiki wakati tunasubiri ujenzi?

(ii) Kwa kuwa Kiwanja hiki kitakapokamilika katika kiwango alichokieleza Mheshimiwa Waziri kitafungua mlango wa pili wa utalii katika Mbuga za Serengeti na Ngorongoro; Serikali itakubaliana na mimi kuwa pesa zitakapopatikana Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga kitakuwa ni kipaumbele cha kwanza kati ya viwanja hivyo alivyovitaja Mheshimiwa Waziri?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii, kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Mlingwa kama ifuatavyo:-

Kwanza; ni Sera ya Serikali kuhakikisha kwamba, wananchi wote ambao wanaathirika katika ujenzi wa miundombinu, wanalipwa fidia zao na kwa kadiri inavyowezekana, kulipwa fidia hizo kwa wakati. Tutafanya hivyo pia kwa Kiwanja cha Ibadakuli; kama ambavyo tumetekeleza sehemu nyingine, nitajitahidi kuhakikisha hilo linatekelezwa kwa wakati.

Kuhusu kipaumbele; tuna viwanja hivi ambavyo vinaizunguka nchi yetu katika maeneo mbalimbali Kaskazini na Kusini, tumechagua saba ambavyo ni *Strategic*, vyote ni kipaumbele kwa maendeleo ya nchi hii, lakini tunafahamu umuhimu wa Ibadakuli Shinyanga. Kwa hiyo ili kutoa fursa za kiuchumi na za kiutalii, kwa maana hiyo ni kwamba, kila linalowezekana litafanywa kuhakikisha kwamba, Kiwanja hiki kitang'ara ili kiweze kutoa huduma ile ambayo itakidhi mahitaji ya kiuchumi ya nchi hii.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nina udhuru kidogo, namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Job Ndugai, aweze kuja kunishikia Kiti kwa sasa.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Yapo matangazo.

WABUNGE FULANI: Kuna swali!

MWENYEKITI: Kuna swali? Haya swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Meshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mbali ya Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga viko viwanja vya ndege kama vile Iringa na Dodoma, ambavyo havina ndege za abiria; na kwa kuwa Iringa kuna viwanda vingi na ajali nyingi za barabarani zinatoka kutokana na msongamano wa watu; je, Mheshimiwa Waziri, una mipango gani wa kufanya viwanja vya ndege vya huko viwe na ndege za abiria ili kupunguza msongamano wa magari?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Viwanja hivi saba ambavyo nimevitaja ni vya kipaumbele, lakini Mpango wa TICAP umeainisha viwanja vingine 16, ambavyo Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba, vinajengewa miundombinu yake kwa kiwango cha juu ili viweze kutoa huduma nzuri ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Mashirikia ya Ndege kuweza kutoa huduma zao katika viwanja hivyo, nini ambacho Serikali tunaweza kufanya; ni kuhamasisha mashirika hayo ya ndege yaweze kutoa huduma katika viwanja hivi ambavyo tunaviboresha, kikiwemo Kiwanja cha Iringa, ambacho hivi sasa kipo katika hali nzuri na kinatumiwa na ndege mbalimbali. Aidha, usafiri wa ndege ni sekta binafsi, tutajitahidi kuwashawishi wenze mashirika ya ndege kutoa huduma hizo, lakini pia Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba, viwanja hivi viko katika hali nzuri ili mashirika ya ndege hayo yaweze kuvitumia viwanja hivi kwa ufanisi.

Na. 323

Sheria ya Uhujumu Uchumi

MHE. STEPHEN J. GALINOMA aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo mwaka 1983 Bunge lilipitisha Sheria Na. 9 (*Economic Sabotage*) inayoweka utaratibu wa kushughulikia wahujumu uchumi; na kwa kuwa Sheria hiyo ilifutwa lakini haitumiki licha ya ukweli kwamba hali ya uhujumu uchumi kwa sasa ni kubwa zaidi kiasi cha kuchukua sura ya ufisadi na kwamba hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi ya wote wanaobainika na kutuhumiwa kulihujumu taifa:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni kwa nini Sheria hiyo haitumiki kikamilifu?

(b) Je, Serikali inaweza kutoa takwimu za kesi za uhujumu uchumi kwa kipindi cha miaka miatatu iliyopita zilizopelekwa Mahakamani na zilizosikilizwa?

(c) Je, kwa nini wahujumu/mafisadi wanaotuhumiwa au kubainika wasichukuliwe hatua kwa mujibu wa Sheria hiyo au Sheria ya Rushwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mbunge wa Kalenga, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, siyo sahihi kusema kwamba, wanaojihusisha na vitendo vya uhujumu uchumi, hawachukuliwi hatua zozote. Wale wanaobainika kujihusisha na vitendo hivyo, hufikishwa mahakamani chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi Na. 13 ya Mwaka 1984, ambayo ilifuta Sheria ya Uhujumu Uchumi Na. 9 ya Mwaka 1983. Sheria hii Na. 13 ya Mwaka 1984, ndiyo imeweka utaratibu wa kushughulikia makosa ya Uhujumu uchumi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kuanzia mwaka 2006 mpaka 2008, jumla ya kesi zilizopelekwa Mahakamani zilikuwa 8,725 na kesi zilizosikilizwa na kumalizika ni 3,239. Jumla ya kesi 4,486 zilizobakia kwa kipindi hicho, bado zinafanyiwa kazi zikiwa katika hatua mbalimbali.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la sehemu (a), wahujumu uchumi wamekuwa wanachukuliwa hatua kwa kufuata Sheria Na. 13 ya Mwaka 1984. Aidha, wale wanaojihusisha na vitendo vya rushwa, huchukuliwa hatua kwa kufuata Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Waziri, kwa majibu yake. Pamoja na hayo, nina swali moja la nyongeza:-

Hakuna mashaka kwa watu wengi kwamba, kasi ndogo ya kesi hizi za uhujumu, rushwa na ufisadi, inaweza kutuletea shida iwapo itaendelea hivyo mpaka wakati wa uchaguzi mwaka kesho. Je, Serikali haioni kwamba itakuwa busara zaidi kupanga na kuzungumza na Mhimili wa Mahakama kwa lengo la kuunda Mahakama Maalum ili kukamilisha kesi hizi tusiendelee na kiwingu hiki wakati wa uchaguzi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stephen Galinoma, kama ifuatavyo:-

Ninachukulia kwamba, aliyoyasema ni maoni na tahadhari kwamba, ucheleweshaji au mwenendo unavyokwenda, unaweza ukaathiri mambo fulani. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, pendekezo lake la kuona kwamba, Serikali inaweza ikazungumza na Mahakama wakaweka Mahakama Maalum ya

kutazama suala hili, nalipokea na nitaliwasilisha Serikalini na kutazama jinsi linavyoweza kufanyiwa kazi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na kama mnavyoona muda wetu umeenda sana; ningeliomba sana muiangalie *Order Paper* vizuri, kule mwisho shughuli za leo ni nyingi kidogo ili tuweze kwenda sambamba. Kabla ya hayo, nina matangazo kama ifuatavyo:-

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni pamoja na mgeni wa Mheshimiwa Spika, Ndugu Paschal Mayala, ambaye ni Mshauri wa Siasa wa Balozi wa Uingereza hapa nchini. Karibu sana Paschal. Alikuwa Mtangazaji siku zilizopita.

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ambao ni binti zake; Lucy na Lilian. Lucy ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini mwaka wa pili, *Bachelor of Community Development*. Lucy yuko wapi? Eeh, ahsante sana. Lilian ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Mzumbe, yeze anafanya *Bachelor of Business Administration, Procurement and Logistics*. Hongereni sana.

Kuna wageni wa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, ambao ni Wenyeviti wa UWT wa Kata tisa za Jimbo la Ukonga. Naomba Wenyeviti wasimame. Karibuni sana.

Kati ya Wenyeviti hawa, mtanyoosha mkono mmoja mmoja ni Eva Nyamoyo – Kata ya Kitunda, Alice Mwangomo – Kata ya Pugu, Imelda Samjela – Kata ya Pugu, Beartha Maatane – Kata ya Ukonga, Mwanaisha Mwita – Kata ya Buguruni, Sophia Kiwanga – Kata ya Vingunguti, Rehema Manzi – Kata ya Kiwalani na Zainab Mbwana – Kata ya Msongole. Karibuni sana.

Pia, tunao wageni wa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, ambao ni walimu wanne na wanafunzi sita kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini, Campus ya Lushoto.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila, ambao ni wanachuo 19 wanasoma Vyuo Vikuu mbalimbali vya hapa Dodoma. Karibuni sana.

Kuna wageni pia kutoka Chama cha Waganga na Wakunga wa Tiba Asilia (CHAWATIATA), ambao ni wanne. Karibuni sana; Vita Magombeka – Katibu Mkuu, yupo Tabibu Fatuma Mwachangwa – Katibu Mwenezi, yupo Ndugu Edward Masanja Ng'wani – Mlezi, huyu inaelekea anatokea kule kule na Tabibu Abdallah. Karibuni sana.

Wapo wageni wa Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama, ambao ni Viongozi sita toka Chama cha Wanawake Kahama (CHAWAKA). Karibuni sana. Yuko Ndugu Joyce Luleka – Katibu Kiongozi, Amina Ikombe, Florah John, Anna Kipilimba, Vumilia Shaban na Elizabeth Tungila. Karibuni sana kutoka Kahama. Hapa ni Dodoma, mnakaribishwa wote.

Wapo wageni 25 wa Mheshimiwa Geoge Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kutoka Shule ya Sekondari Matomondo Mpwapwa. Inaelekea wanaweza wakawa *basement* na Mheshimiwa Lubeleje simwoni, nadhani yuko nao.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero, naomba wote wasimame. Yuko Shema Ndama – Diwani wa Kata ya Kiberege, Lyoka – Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiberege, Mbingi – Afisa Mtendaji Kata ya Kiberege, Libahala – Mtendaji wa Kijiji cha Kiberege, Ching’ota – Mwenyekiti wa Mgeta SACCOS na Mwasyola – Mjumbe wa Mgeta SACCOS. Ahsanteni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Abdulkarim Shah wa Mafia ni watoto wake Naima, yuko wapi ahsante! Halafu Ismail; ahsante sana. Nirshad, ahsante kabisa; na mjukuu Salum yuko wapi! Haya hongereni sana na karibuni sana Dodoma.

Yupo Mama Mari Mbogoni, Mwalimu na Mkazi wa Dodoma, amekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge; karibu mama Mbogoni na kwa jina lako inaelekea unatoka Kongwa; karibu sana.

Henry Mgonja, mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, anatembelea Bunge; karibu sana Mgonja. Wapo wageni wengine watatu kutoka Dodoma nao wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge, ambao ni Similwa Mdumbwa, Ndugu Theresia Peter na Rose Jeremiah; karibuni sana.

Wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Ualimu cha Don Bosco Pharecian Seminary Dodoma, karibuni sana wanafunzi Bungeni Dodoma. Pia wapo wanafuzi 40 na walimu wao kutoka Shule ya Sekondari ya Ufundı ya Hijra Dodoma, hawaonekani inaelekea na wako *basement*.

Mheshimiwa Pindi Chana ana wageni; Ommy and Company ambao ni Wajasiriamali wa hapa Dodoma, karibuni sana. Pia, Mheshimiwa Dustan Mkapa na Mheshimiwa Mariam Kasembe, wana wageni ambao ni ndugu zao kutoka Mtwara, Ndugu Donald Mkapa na Vick Kasembe; karibuni sana.

Mheshimiwa Nyami, anawaomba Waheshimiwa Wabunge, ambao wanajifahamu wenyewe wanaoshughulikia suala la mfumo wa pensheni, wakutane Saa Saba, Chumba Na. 227.

Mheshimiwa Omar Kwaangw’, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, anaomba Wajumbe wa Kamati yake ya Kudumu ya Mambo ya Huduma za Jamii, kutakuwa na kikao saa saba mchana, terehe 31 Julai, Ukumbi wa Pius Msekwa B.

Mheshimiwa Shellukindo, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini kwamba, mkutane saa nane mchana Ukumbi Na. 219. Mheshimiwa Wilson Masilingi, pia anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na

Usalama, wakutane saa saba Ukumbi wa Pius Msekwa. Kamati ya Maliasili na Mazingira, tunaombwa kukutana saa saba mchana chumba Na. 133.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya na kama nilivyowaeleza, shughuli zetu ni nyingi kwa siku ya leo, naomba sasa nimwite Katibu kwa hatua inayofuata.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Mazao ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko wa Mwaka 2009 (*The Cereal and Other Produce Bill, 2009*).

Muswada wa Sheria ya kufanya Marekebisho katika Sheria mbalimbali za Mazao wa Mwaka 2009 (*The Crops Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2009*).

Muswada wa Sheria Mpya ya Korosho wa Mwaka 2009 (*The Cashewnut Industry Bill, 2009*).

Muswada wa Sheria ya Mtoto wa Mwaka 2009 (*The Law of the Child Bill, 2009*).

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni
Mara ya Kwanza)*

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009 (*The Appropriation Bill, 2009*).

(Muswada Uliotajwa hapo juu Ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)

**Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali
wa Mwaka 2009 (*The Appropriation Bill, 2009*)**

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria wa kutumia kiasi cha shilingi 9,513,685,000,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo, itakayotekelizwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/10 na kutumia fedha zitakazotolewa na Serikali kwa ajili hiyo, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba, katika Hotuba ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2009/10, nilieleza shabaha na malengo ya Serikali ya kutumia shilingi 9,513,685,000,000 kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/10, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, matumizi ya kawaida shilingi 6,688,253,600,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, matumizi ya Miradi ya Maendeleo shilingi trilioni mbili, bilioni mia nane ishirini na tano milioni, mia nne themanini na moja elfu, (2,825,431,000,000). Jumla ni shilingi trilioni tisa, bilioni mia tano na kumi na tatu, milioni mia sita thelathini na tano (9,513,685,000,000).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu, limekwishajadili na kupitisha hoja mbalimbali za Waheshimiwa Mawaziri wakati walipowasilisha makadirio ya Wizara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu ni kuliomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/10 ya jumla ya shilingi trilioni tisa, bilioni mia tano kumi na tatu, milioni mia sita themanini na tano (9,513,685,000,000) kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo, iliyokubaliwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tumesikia mawasilisho ya Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunashughulikia *Appropriation Bill*, ambayo ndiyo inafunga shughuli nzima ambayo tumekuwa tukiifanya katika kipindi chote cha Bunge hili. Kwa hatua hii, sasa nitawahoji muiamue hoja hiyo.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

**Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali
wa Mwaka 2009 (The Appropriation Bill, 2009)**

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa*)

HOJA ZA SERIKALI

M A A Z I M I O

MWENYEKITI: Naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa ajili ya Azimio.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha na Uchumi, kufuta au kusamehe maduhuli yaliyoshindikana kukusanya, madeni au hasara ambazo hazilipiki, zitokanazo na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali, kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2008 kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura Namba 348, kifungu Na. 43 (1). Aidha, Azimio hili lilijadiliwa na kupitishwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), katika kikao chake cha tarehe 28 Julai, 2009, kilichofanyika hapa MJINI Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki (UDP), pamoja na Wajumbe wote wa Kamati, kwa maoni yao mazuri, yenye lengo la kuboresha udhibiti na uimarishaji wa usimamizi wa mali na vifaa vya Serikali kwa lengo la kupunguza au kuepuka upotevu wa mali na vifaa vya Serikali. Aidha, ushauri wao kwa kiasi kikubwa umezingatiwa na Serikali katika kuboresha Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio linalowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, linakusudia kufuta na kusamehe maduhuli yaliyoshindikana kukusanya, madeni, hasara na potevu ambazo hazilipiki, kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2008. Aidha, hasara na upotevu huu unajumuisha hasara na potevu chache zilizotokea miaka ya tisini na nyingine zikiwa ni za kati ya kipindi cha kuanzia Julai, 1987 hadi Juni, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa hasara na upotevu huu, umefanyika kwa ushirikiano baina ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Aidha, hasara au upotevu huu, umekuwa ukishuka mwaka hadi mwaka, kuanzia shilingi 72.9 bilioni katika mwaka ulioishia 30 Juni, 2002 mpaka shilingi 15.1 bilioni kwa mwaka ulioishia 30 Juni, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasara husika zimegawanyika katika sehemu kuu tatu. Mgawanyo huu una lengo la kuainisha kwa uwazi zaidi, hasara husika ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuzielewa vizuri na hatimaye kufikia uamuzi ulio sahihi. Hasara hizi ni kama ifuatavyo:-

(i) Zile zinazohusu upotevu wa fedha, vifaa vya shilingi 462,837,346.81; na malipo ambayo Serikali haikupata manufaa ya kiasi cha shilingi 1,782,344,678.00.

(ii) Zile zinazohusu mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanya ya kiasi cha shilingi 11,415,115,538.80.

(iii) Marekebisho ya vitabu shilingi 1, 387, 777,455.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya upotevu wote ni shilingi 15,048,075,018.61, ambayo maelezo yake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hasara zinazohusu upotevu wa fedha, vifaa na malipo yasiyoiletea Serikali manufaa (*Value for Money*), shilingi 2,245,182,024.81. Hasara hizi zinahusisha upotevu wa fedha taslimu, upotevu au uharibifu wa vifaa na malipo, ambayo Serikali haikupata manufaa yoyote. Upotevu huu ulitokea katika miaka ya 1987 mpaka kipindi kinachoishia 30 Juni, 2008. Upotevu huu umetokana na sababu mbalimbali, zikiwemo wizi wa makusanyo ya mapato uliosababishwa na watumishi wasio waaminifu, kudokoa na kupeleka fedha Benki zikiwa pungufu, majambazi kuvunja na kupora fedha na vifaa, ajali za moto kuunguza vifaa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sababu nyingine za upotevu ni pamoja na wizi wa mali, vifaa na uzembe, ambapo vifaa huachwa bila kuangaliwa na mwishowe huharibika hasa kwa vifaa viliwyopo katika Bohari za Serikali, vifaa viliwyoko katika Bohari kuitwa na wakati hivyo kutofaa kwa matumizi na malipo yaliyofanyika bila Serikali kunufaika na huduma yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, maduhuli yaliyoshindikana kukusanya, yanayoombewa kufutwa ni shilingi 11,415,115,538.80. Maduhuli yaliyoshindikana kukusanya, yametokana na sababu mbalimbali zikiwemo, kafilisika kwa walipa kodi, gharama za ukusanyaji maduhuli kuwa kubwa kuliko kiasi kinachotarajiwa kukusanya, maamuzi mbalimbali ya Mahakama yanayoizua Serikali kukusanya maduhuli dhidi ya wadaiwa na baadhi ya walipa kodi kutojulikana walipo, baada ya kuhamisha au kufunga shughuli zao na wengine kufariki dunia. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imekuwa inadai Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Benki Kuu ya Tanzania, kiasi cha shilingi 7,862,362,894.80. Kodi hii ilitokana na VAT iliyotozwa BOT na Kampuni ya Group Five, iliyokuwa na mkataba wa ujenzi wa Majengo Pacha ya Benki Kuu ya Tanzania. Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya Mwaka 2006 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, Benki Kuu ya Tanzania haipaswi kulipa kodi hiyo. Hata hivyo, kuitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2005, Benki Kuu ya Tanzania ilitakiwa kulipa kodi, hali iliyosababisha kuwepo kwa deni hili. Matakwa haya ya kisheria, yalidumu kwa kipindi cha mwaka mmoja tu hadi mwaka 2006, ambapo Sheria ya Fedha ya mwaka 2006, ilirejesha msamaha huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maduhuli ya shilingi 3,487,752,644.00 yalikuwa yakusanywe kutoka kwa walipa kodi mbalimbali kutoka kwa makampuni na watu binafsi kutoka Mikoa yote ya Kodi Tanzania Bara. Pamoja na juhudni za kukusanya, maduhuli haya yameshindikana kukusanya kutokana na makampuni na watu binafsi katika mikoa inayohusika, kafilisika, kufariki au kutojulikana waliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kiasi cha shilingi 1,387,777,455.00, kinahusu marekebisho ya vitabu (*Book Adjustments*), yanayotokana na kodi ya ushuru wa forodha, iliyokuwa ikidaiwa kutoka kwa Kampuni ya Joseph Majige. Madai haya ya kodi yalitokana na Hoja ya Ukaguzi Na. 33 ya 2002/2003, ambayo Kampuni hiyo ilidaiwa kuingiza mafuta ya petroli nchini kutoka Kenya. Kiasi kilichodaiwa kuingizwa, kilikuwa kikubwa kuliko mafuta halisi yaliyopokelewa na kulipiwa kodi Bandarini Mwanza; hivyo, kampuni hiyo kupinga kodi hiyo na kuishtaki TRA (Kesi ya Mahakama Kuu Na. 49 ya Mwaka 2000 inahusika).

Kesi hii iliendelea hadi mwaka 2005, wakati mmiliki mkuu wa Kampuni ya Joseph Majige alipofariki dunia. Baada ya mhusika kufariki, Wakili wake alifuta kesi hiyo mahakamani. Katika juhudzi za kuhakikisha kodi hiyo inakusanywa, TRA waliazimia kukamata mali za Kampuni, lakini baada ya uchunguzi, waligundua kwamba, kampuni hiyo haikuwa na mali zozote wala akaunti ya benki ambayo ingeweza kukamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapendekeza kufuta na kusamehe maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa, madeni, hasara na upotevu ambao haulipiki, kiasi cha shilingi 15,048,075,018.61, kama ilivyoainishwa katika jedwali ambalo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa ili kutoa picha halisi ya vitabu vya mahesabu. Aidha, kibali cha Bunge cha kuidhinisha Azimio hili, kitaisaidia Serikali kufanya marekebisho katika vitabu vyake vya hesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kufuta na Kusamehe Maduhuli Yaliyoshindikana Kukusanywa, Madeni, Hasara na Upotevu wa Fedha na Vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia 30 Juni, 2008, kama ifuatavyo:-

KWA KUWA; kifungu cha 5 cha Sheria ya wa Fedha za Umma, Sura Namba 348, kinampa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, mamlaka ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kugawa na kuidhinisha matumizi ya fedha hizo baada ya kupata idhini ya Bunge;

NA KWA KUWA; kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura Namba 348, kinalipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka kupitisha Azimio la Bunge kumruhusu Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kufuta hasara na upotevu wa vifaa vya Serikali, madai ya kodi, pamoja na riba itokanayo na malimbikizo ya kodi;

NA KWA KUWA; Vitabu vya Hesabu za Serikali vimeonesha kuwepo kwa upotevu wa fedha na mali za Serikali pamoja na maduhuli kutokana na kushindikana kukusanywa;

NA KWA KUWA; kutokana na upotevu na upungufu huo wa fedha, vifaa na maduhuli ya Serikali, upo umuhimu wa kusawazisha kumbukumbu katika vitabu hivyo vya Serikali;

KWA HIYO BASI; kwa mujibu wa kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura Namba 348, sasa Bunge hili, katika Mkutano wake wa kumi na sita, linaazimia kumuidhinisha Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha, kusamehe na kufuta upotevu wa fedha, vifaa, malipo batili na maduhuli yaliyoshindikana kukusanya wa kwa kipindi kinachoanzia mwaka wa Fedha 1987/1988 hadi 30 Juni, 2008 na kwa ajili hiyo, kusawazisha kumbukumbu kwenye Vitabu vya Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Upotevu wa fedha taslimu, vifaa na matumizi yasiyoleta manufaa kwa Serikali shilingi 2,245,182,024.81.

(b) Mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanya shilingi 11,415,115,538.80.

(c) Marekebisho ya vitabu shilingi 1,387,777,455.00.

Jumla kuu ni shilingi 15,048,075,018.61.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Katika kuendelea na Azimio hili, ipo Kamati ambayo imechambua jambo hili. Naomba sasa moja kwa moja nimwite Mwenyekiti wa Kamati husika, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, kwa niaba ya Kamati. Naomba vilevile Msemaji wa Upinzani ajiandae.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu azma ya Serikali kufuta madeni na upotevu wa vifaa vya Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, kwa kunipa heshima ya kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa John M. Cheyo - Mwenyekiti, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Muhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Dkt. Chrisant M. Mzindakaya,

Mheshimiwa Manju S. Msambya, Mheshimiwa Ali Haji Ali, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na Mheshimiwa Hasnain G. Dewji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilielezwa mbele ya Kamati kuwa, Serikali inaomba kibali cha kufuta upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kiasi cha Sh.15,048,075,018.61 katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2008. Aidha, mwaka uliopita, hoja hii ilikuwa ni ya shilingi bilioni 73. Kwa hiyo, kuna mafanikio sasa kwa Serikali katika kupunguza potevu na hasara zitokanazo na uzembe na utunzaji wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilielezwa kuwa, hasara/potevu za fedha na vifaa vya Serikali mpaka mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2008 ni zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasara/potevu zinazohusu Fedha, Vifaa na Malipo ambayo Serikali haikupata manufaa/tija Sh.2,245,182,024.81, ambazo zinatokana na sababu mbalimbali zikiwemo:-

- Wizi kwa njia ya watumishi kudokoa maduhuli kabla ya kuyapeleka benki, wizi wa majambazi kuvunja na kupora fedha na vifaa katika stoo, ajali za moto kuunguza vifaa, ikiwa ni pamoja na uzembe kama vile kuacha vifaa bila uangalizi na mwisho wake kupotea au kuharibika.

- Hasara nyingine ambayo imo ndani ya Sh. 2,245,182,024.81 ni ile ya malipo yasiyo na tija/manufaa kwa Serikali ya Sh.1,765,654,721.000, yaliyofanya na Wizara ya Maji na Umwagiliaji wakati waliponunua mitambo mitatu ya shindilia hewa katika nyakati tofauti katika 2000/2001 na 2003/2004 kutoka Nchini Canada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasara/potevu zilizotokana na Serikali kushindwa kukusanya mapato/maduhuli iliyokusudia kuyapata Sh.11,415,115,538.80. Hasara hizi zimetokana na sababu mbalimbali, kama vile:-

- Madai ya madeni jumla ya sh. 65,000,000.00, ambayo Hazina ilikuwa inadai Bodi ya Utalii Tanzania tangu mwaka 1996/1997, lakini Bodi ya Utalii imeshindwa kulipa deni hilo kutoptaka na chanzo cha mapato ilichokuwa ikitegea (nyumba waliyokuwa wamekodisha kwa Ubalozi wa Marekani), kuungua moto tarehe 07 Agosti, 1998, kufuatia nyumba hiyo kupigwa mabomu na kuteketea. Hivyo, Bodi hiyo imeshindwa kulipa deni hilo kwa vile haikuwa na chanzo kingine cha mapato isipokuwa ruzuku ya Serikali.

- Madeni sugu ya Sh.3,487,752,664.00 yanayotokana na kodi mbalimbali, ambazo Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), imeshindwa kukusanya kutoka kwa makampuni mbalimbali na watu binafsi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara katika kipindi cha 1998/1999 hadi 2007/2008. Aidha, juhudhi kubwa zimefanywa katika kukusanya malimbikizo hayo, lakini hazikufanikiwa kwa vile wengi wa Wafanyabiashara na Makampuni hayo yamefilisika na Wakurugenzi wao wamefariki dunia, bila kuacha mali zozote ambazo zingelipia madeni hayo.

- Mapato/Maduhuli yaliyokuwa yakusanywe na Mamlaka ya mapato mwaka 2005/2006 kama Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya jumla ya Sh. 7,862,362,894.80 kutoka Kampuni ya *Group Five*, iliyokuwa na mkataba wa kujenga majengo pacha ya Benki kuu, lakini mapato hayo hayakukusanywa kwa vile *VAT Act No. 13* ya 1997 inasema wazi kuwa, Benki Kuu hawakutakiwa kulipa VAT, lakini *GN No. 13* ya 2005, iliyotumika kimakosa, ilitaka Benki Kuu kulipa VAT. Hivyo, kwa kuzingatia *VAT Act* ya 1997 na *Finance Act* ya 2006, kodi hiyo haiwezi kulipwa na Benki Kuu. Kwa hiyo ni vyema ikafutwa kwenye Vitabu vya *TRA* kama mapato ambayo hayajakusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya vitabu ya shilingi 1,387,777,455.00 yanayotokana na malimbikizo ya Ushuru wa Forodha, yaliyokuwa yanadaiwa kwa Kampuni ya mafuta ya Majige Joseph Company, Mjini Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasara hiyo iliyosemekana kuwepo, inatokana na Hoja za Wakaguzi Na. 33/2002/2003 ambayo Wakaguzi waligundua kwamba, Kampuni hiyo ilikwepa kulipa ushuru wa Forodha baada ya kuingiza mafuta nchini toka nchi jirani ya Kenya mwaka 2002/2003. Aidha, sababu iliyopelekea Kampuni hiyo kukataa kulipa ushuru huo ni *TRA* kudai ushuru wa forodha kwa tani 24.5 za mafuta (kama nyaraka kutoka Kenya zilivyoonesha), badala ya tani 22.5 za mafuta ambazo muingizaji alionesa kwenye nyaraka zake. Ubishi huu ulisababisha muingizaji (*importer*) kuishtaki *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kesi kwisha na baada ya Mkurugenzi kufariki, Wakili wa Mlalamikaji aliondoa shauri la madai mahakamani. *TRA* ilifanya kila jitihada kukusanya kodi hii. Juhudi hizi zilikuwa ni pamoja na kutafuta mali ya muagizaji inayoweza kuuzwa ili kupata hizi fedha. Kwa kuwa uchunguzi uliofanywa na *TRA* na Wakaguzi ulibainisha kuwa, mmiliki wa Kampuni hiyo, Ndugu Majige Joseph aliye kwishafariki na Kampuni hawana mali za kulipa deni hilo; kuna umuhimu wa kufuta hasara hii ambayo tayari imeingizwa kwenye Vitabu vya *TRA* na ni hoja ya ukaguzi ili kuweza kufanya marekebisho kwenye vitabu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maelezo kutoka Serikalini, Kamati ilijadili na kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kama tulivyoeleza mwaka uliopita, Kamati haifurahishwi na zoezi la kufuta hasara/potevu za fedha na vifaa vya Serikali, kwani katika kuinua mapato ya Serikali ni vyema Watendaji wa Serikali wakawa makini katika kukuza mapato ya Serikali, badala ya kuruhusu upotevu wa fedha na vifaa hivyo na hatimaye kuja mbele ya Bunge kuomba kibali cha kufuta hasara/potevu hizo.

(ii) Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali ifanye juhudhi za dhati za kuhakikisha kuwa, haipati hasara/potevu za aina yoyote ile, hasa zile zinazosababishwa na uzembe au utendaji usiozingatia Sheria ya Watumishi wa Serikali. Nia iwe ni kuzuia hasara/potevu za aina yoyote zisitokee, isipokuwa zile ambazo ziko nje ya uwezo wa Watumishi wa Serikali.

(iii) Ni vyema Maafisa Masuhuli wakazingatia na kutilia maanani, maelekezo wanayopewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*), Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) na Hazina, kuhusu matumizi mazuri ya Fedha za Umma na umuhimu wa kuzingatia Sheria zinazotuongoza katika utekelezaji wa mipango ya Serikali ili kupunguza hasara/potevu za fedha na Vifaa vya Serikali.

(iv) Kwa hasara/potevu zinazotokana na uzembe wa Watumishi wa Serikali kwa kufanya malipo batili au yasiyo na manufaa/tija kwa Serikali, wahusika ni lazima wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria ili kuhakikisha kuwa, uzembe kama huu haujirudii na kuendelea kuitia hasara Serikali. Aidha, Kamati inashauri wakati tunafikiria mchakato wa kurekebisha Sheria ya Fedha ili iweze kuwabana Watendaji wanaoliletea Taifa hasara zinazoepukika; ni vyema Serikali ikawa inawashusha vyeo au kuwastaafisha kwa manufaa ya Umma, Watendaji wazembe na wanaokiuka Sheria za Fedha katika utekelezaji wa Mipango ya Serikali.

Aidha, Kamati inashauri kuwa, hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa wale waliohusika na upotevu wa shilingi 1,765,654,721 katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa ununuzi wa mitambo mitatu ya shindilia hewa kati ya mwaka 2000/2001 na 2003/2004.

(v) Ili kuhakikisha tunaboresha uendeshaji na usimamizi thabiti wa fedha za umma na hatimaye kupunguza au kuondoa kabisa hasara zinazoepukika, ni vyema Serikali ikapitia upya Sheria zinazohusu Sekta ya Fedha ili kuziba mianya ya Sheria inayosababisha kuwepo na mazingira yanayosababisha hasara/potevu hizi. Aidha, juhudhi hizi zitachangia na kuleta tija katika mpango endelevu wa Serikali wa kurekebisha/kuboresha mfumo wa Uendeshaji katika Sekta ya Fedha nchini.

(vi) Serikali iendelee kukusanya madeni na kufuatilia mali na fedha zinazodhaniwa kuwa zimepotea na Taarifa ya mafanikio ya ufuutiliaji huo, iwasilishwe kwenye Kamati na kisha mbele Bunge.

(vii) Serikali iongeze juhudhi ya kukusanya kodi kutoka makampuni mbalimbali, kwani kwa kutofanya hivyo ni kuitia hasara na kudumaza uchumi wa nchi.

(viii) Wizara na Idara za Serikali zinapoleta mbele ya Kamati ya Hesabu za Serikali, Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha husika, ziambatane na orodha ya upotevu wa fedha na mali za Serikali katika Wizara na Idara zao ili Maafisa Wahasibu watoe maelezo, badala ya kumwachia Mhasibu Mkuu wa Serikali, ambaye hawezu kuwa na maelezo ya kina kwa kila upotevu.

(ix) Katika upotevu wote unaoombewa kibali cha kufutwa, hasara/upotevu unaotokana na mapato/maduhuli yaliyoshindikana kukusanya na Serikali ni Sh. 11,415,115,538.80, ambayo ni asilimia 75.9 ya hasara/upotevu wote. Hiki ni kiashiria cha upungufu katika Sheria ya Fedha na udhaifu uliopo katika mifumo tuliyonayo ya

ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), kuhakikisha inapitia upya mifumo na taratibu za ukusanyaji mapato ili iweze kuweka mikakati mipy na madhubuti ya kuhakikisha ukusanyaji mapato unaongezeka na hasara zitokanazo na udhaifu uliopo zinapungua. Aidha, ni vyema *TRA* ikahakikisha inawajua vizuri wateja wake ili kusiwe na ukwepaji wa kulipa kodi, malalamiko ya walipa kodi na hasara zinazojitokeza kutokana na kushindwa kutaifisha mali pindi mteja anaposhindwa kulipa kodi. Vile vile ni vyema Watendaji wakawa makini katika ukusanyaji wa mapato kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba niwapongeze Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Maafisa wengine, kwa kuwasilisha Azimio hili mbele ya Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni hayo, Kamati katika ujumla wake, haina pingamizi juu ya kuridhiwa kwa Azimio hili na inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuliridhia Azimio hili ili kuondoa hoja za Wakaguzi, ambazo zimekuwa zikichafua Vitabu vya Hesabu katika Wizara na Idara za Serikali husika, kutokana na kutofutwa kwa hoja hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru tena, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, kwa maoni na ushauri walioutoa kwa lengo la kuhakikisha upotevu wa aina hii hautokei tena, isipokuwa kwa sababu zinazotokana na majanga ya moto na mengine yanayofanana na haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni haya, Kamati yangu, inaunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha. (*Makofit*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, kwa kutuwasilishia maoni haya kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Kwa hatua hii, sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kuhusiana na Azimio lililopo mbele yetu.

MHE. DKT. WILLIBROD P. SLAA (K.n.y. MSEMADI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Uchumi, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge, linalohusu kuridhia kusamehe madeni, madai ya kodi, pamoja na riba, hasara itokanayo na upotevu wa fedha, vifaa na maduhuli ya Serikali, kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, Kambi ya Upinzani inapenda kutamka kwamba, inaunga mkono kwa dhati na kukubaliana na mapendekezo ya Kamati ya

Hesabu za Serikali, ambayo imechambua kwa kina hoja iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu na inakubaliana na Azimio la Bunge na tunaliunga mkono Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono Azimio hilo, Kambi ya Upinzani inapenda kusisitiza ifuatavyo:-

(i) Kufuta madeni ni jambo moja ili kuondoa hoja isijirudie rudie katika vitabu na hivyo kufanya vitabu vyetu kuonekana vichafu kila wakati, kwa jambo ambalo haliwezi kukusanywa tena. Kwa maana hiyo ni kweli tunaunga mkono hoja. Kama alivyowahi kueleza *CAG* mbele ya Kamati zetu, kufuta ni jambo moja na kuchukua hatua za kiutawala na kinidhamu kwa wale waliohusika na upotevu huu au wizi huu ni suala lingine. Kambi ya Upinzani inapenda kusisitiza kwamba, hatua za kinidhamu ni lazima zichukuliwe hata baada ya kufuta madeni haya.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa ni lazima Serikali iwe na umakini mkubwa katika kutunga sheria, kuepuka mgongano amba kwa wakati mwingine ndiyo unaosababisha matatizo haya, mathalani kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Naibu Waziri na hata Kamati kwamba, mgongano uliotokana na Sheria Na. 13 ya Mwaka 1997 na GN Na. 13 ya Mwaka 2005 na *Finance Act* ya Mwaka 2006, ambayo imesababisha hasara ya shilingi bilioni 7.8, ambayo inahusiana na Mkataba kati ya *Group 5*, unaohusu majengo pacha. Hasara hii isingeweza kutokea au tatizo hili lisingeweza kutokea kama tungekuwa na umakini katika utungaji wetu wa sheria. Kambi ya Upinzani inasisitiza kwa mara nyingine kwamba; ni vyema wakati wa maandalizi, Serikali ikawa makini kusikiliza hoja mbalimbali ndani ya Bunge na ikaaoanisha Miswada mbalimbali inayowasilishwa ndani ya Bunge hata kabla haijawasilishwa. Tunaweza kuepuka athari kubwa na athari kubwa ambayo inatokea hapa ni shilingi bilioni 7.8, ambayo imeonekana mara kadhaa katika *Revenue Statement* yetu, haikuweza kufanya kazi ambayo imekusudiwa, lakini tukawa tuna bajeti na hatuwezi kutekeleza kwa sababu kumbe fedha hiyo ambayo ni maduhuli ya Serikali haikuweza kukusanywa.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inafikiria pia kuwa, tatizo kubwa ambalo hatujalifanyia kazi ni la kucheleva kuchukua hatua wakati mambo haya yanapoonekana. Leo tunazungumzia miaka kumi baadaye, matatizo yaliyotokea mwaka 2000/2001 na 2003/2004 na karibu yote ni mambo yaliyotokea nyuma pengine kwa miaka kama mitano iliyopita.

Vilevile tuna tatizo la Mahakama hazitoi maamuzi mapema, Vyombo vyaa Rufaa havichukui hatua mapema na matokeo yake ndiyo haya ambayo leo yanaonekana, kuna makampuni yamefilisika. Kwa hiyo, hatuwezi kukusanya kutoka kwao, watu wamefariki hatuwezi pia kukusanya chochote kutoka kwao, lakini tungelichukua hatua mapema sehemu kubwa ya fedha hizi zingeweza kurejeshwa.

Kambi ya Upinzani inasisitiza, Serikali ikae na vyombo hivi, hatusemi tuingilie Mahakama kwa maana ya maamuzi ya Mahakama, lakini utendaji kazi wa Mahakama ni pamoja na mambo ambayo yanapaswa kusimamiwa na Bunge hili na inapofika mahali maamuzi ya mahakama hayachukuliwi kwa zaidi ya miaka mitano hadi sita ni lazima

sasa ifikie mahali itoe majibu kwa Bunge ni kwanini maamuzi haya hasa pale uamuza unapokuwa umefikiwa lakini hautolewi hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la wizi na hili limesemewa vizuri na Kamati, sitaki kulirudia, lakini nataka kusisitiza kwamba, katika suala lililotokea la ununuzi hewa wa vifaa vya maji, Kambi ya Upinzani inasisitiza na inaungana na Kamati kwamba, wahuksika ni lazima wachukuliwe hatua za kinidhamu na tunataka kujuu hatua hiyo ni ipi katika Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya tumepeitiwa, nadhani kwa mara ya pili sasa *statements of reallocations* hazijadili. Kambi ya Upinzani, inapenda pia kutumia nafasi hii kupitia kwa kifupi sana *statement of reallocation*, ambayo hatujadili. Kitu kimoja tu ambacho tungependa kukiweka mbele ya Bunge na hasa Serikali iweze kutambua, kwenye *statement of reallocation* tumegundua mambo ambayo ni magumu na ni mazito kidogo. Tunapofanya *reallocation* kutoka kwenye kasma ambazo zinagusa maisha ya watu, kwa mfano, hospitali tukapeleka kwenye kasma ambayo inaandikwa *contingency*, Bunge lingependa kupata taarifa ya kina; hii *contingency* maana yake nini? Kwa sababu unaondoa kutoka hospitali kwenye uhai wa binadamu na Bunge ndiyo iliidhinisha hivyo, kupeleka fedha kwenye hospitali lakini inakwenda kwenye *contingency*; jambo ambalo Bunge halielewi tena!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano hiyo ipo mingi, ungeweza kuitoa hapa; shilingi bilioni 184 zimefanyiwa *reallocation* za namna hii na fedha ambazo zimetoka kwenye hospitali ni shilingi bilioni 2.4, ambazo ni fedha nyingi sana kwa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna maeneo mengine kwa mfano, barabara. Barabara ndiyo mishipa ya damu ya uchumi; unaondoa kutoka kwenye Barabara ya Same – Mkumbara – Korogwe shilingi bilioni 82, maana yake umesimamisha ile Barabara moja kwa moja, lakini unapeleka kwenye *contingency* ambayo Bunge halijui ni kitu gani. Kwa hiyo, tungeweza kuendelea kuonesha vitu vya namna hiyo, ikiwemo na *Agricultural Sector Development Programme* na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wetu wa Mifugo amepiga kelele, unaondoa fedha kutoka kwenye mifugo halafu tunaacha mifugo yetu katika hali ambayo hata nyama hatuwezi kuuza, kwa sababu hazina ubora. Kwa hiyo, tunasisitiza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako, kwa kutupa nafasi. Nisisitize tena kwamba, Kambi ya Upinzani inaunga mkono Maazimio ya Kamati na inaunga mkono Azimio la Kufuta Madeni haya kwa maana ya vitabu, lakini hatua zichukuliwe kwa wale wote ambao wanahusika na upotevu huu. (*Makofit*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dokta Slaa, tunakushuru sana, kwa kuwasilisha maoni hayo ya Kambi ya Upinzani, kuhusiana na Azimio lililopo mbele yetu. Nina mchangiaji mmoja tu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela; nimpe nafasi atuwakilishe sote na baada ya hapo Naibu Waziri atafuatia.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nikushukuru kwamba, umenipatia nafasi ya ghafla kuchangia hoja hii ya Serikali kuhusu kuridhia kufuta na kusamehe madai ya kodi, pamoja na riba, hasara itokanayo na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali na maduhuli kama ambavyo Naibu Waziri amewasilisha hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiambie Serikali kwamba, leo tumekubali, tumeridhia, lakini ni vyema Serikali ikafahamu kwamba, siku zijazo ipo siku tutasema hapana. Sisemi hivyo tu kwa sababu nasema, kuna hasara nyingine ambazo hazizuiliki kama zile za moto, maji na kadhalika, lakini kitu kama wizi au ununuzi hewa, naomba Serikali ieletee kwamba leo ni mara ya mwisho kukubali kufuta hasara za namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasara kwa vitu ambavyo vinazuilika, wizi au ununuzi hewa unazuilika; iwapo nchi yetu ambayo ni kati ya nchi 25 zinazojulikana ulimwenguni kwa umaskini tutaendelea kuruhusu wizi ama ununuzi hewa halafu Serikali ituletee hapa kutusihii sisi Wabunge tufute hasara; sisi ambao tunawakilisha wananchi maskini, hapana kuna siku Bunge hili litageuka na kusema hatukubali vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mambo ambayo ni ya msingi kama vile moto haizuiliki, vile ni vitu ambavyo binadamu ye yeyote anaolewa, lakini manunuzi hewa yalipofanyika Serikali ilikuwa wapi mpaka yanafikia hatua leo wanatuletea kuja *ku-write off* vitu kama hivi? Hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi siyo yetu ni nchi ya Watanzania zaidi ya milioni 40, wizi hatutakubali kufuta madeni yake, manunuzi hewa hatutakubali kufuta. Naomba Serikali ieletee kwamba, leo tumekubali na leo ndiyo mara ya mwisho kwa Bunge hili linalowakilisha Watanzania kukubali kufuta hasara zinazotokana na vitu kama wizi au manunuzi ambayo ni hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo Bunge hili linakubali tu kufuta hasara zinazohusu wizi na manunuzi hewa, basi manunuzi hayo yatakuwa mengi sana na wizi huo utakuwa mwangi sana. Kwa hiyo, sisi tutakuwa kama vile tunaweka mbolea kwa watu waendelee kuiba, waendelee kufanya manunuzi ambayo ni hewa, litakuwa siyo Bunge litakuwa gulio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusihii sana, Serikali ieletee kwamba leo tumekubali, lakini leo iwekwe katika historia ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba ni mwisho, hatutakubali siku nyingine kuja kufuta hasara zinazotokana na wizi na hasara zinazotokana na manunuzi hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naunga mkono kwamba, tumekubali lakini kwa mara ya mwisho. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa

niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa Kamati kuweza kupitia na kukubali kumuidhinisha Waziri wa Fedha kufuta. Pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na wao vile vile kwa kupitia na kukubali kumuidhinisha Waziri wa Fedha kufuta upotevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwataje waliochangia ili na wao waweze kuingia katika Hansard; Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, Mbunge wa Pangani; Mheshimiwa Dokta Slaa, Mbunge wa Karatu; na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki. Nasema maoni yao tumeyapokea, tunayachukua na tutayafanya kazi kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu kwa haraka haraka baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa watatu wamezieleza katika uwasilisho wao. Kwanza, nataka niwaambie kwamba, moja ya majukumu ambayo Mheshimiwa Rais amempa Waziri wa Fedha ni kuhakikisha kwamba, anakusanya mapato ya kutosha kwa ajili ya shughuli zetu za kawaida na shughuli zetu za maendeleo. Kwa hiyo, mtu wa kwanza ambaye anatakiwa awe na uchungu wa upotevu na wizi ni Waziri wa Fedha. Kwa maana hiyo, nataka nikuhakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba, Waziri wa Fedha, pamoja na Manaibu wake na Watendaji wa Wizara yake, tuna wajibu wa kuona uchungu zaidi hata ya ninyi Wabunge juu ya upotevu huu na kwa njia hiyo basi, sisi tutahakikisha kwamba, upotevu huu haujitokezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba, Kamati imesema haifurahishwi na mimi nakubaliana nao kwamba na sisi kama Viongozi wa Wizara hatufurahishwi. Vile vile nataka niseme kwamba, Waheshimiwa Wabunge ni lazima tukubali katika bilioni kumi na tano tunazoomba kufutwa ni shilingi milioni mia nne na sitini na mbili ndiyo zilizoibowi. Nakubali ni nyingi, lakini katika bilioni 15 tutahakikisha kwamba, hizi milioni mia nne na sitini na mbili hatufikii tena katika miaka inayokuja. Wale waliosababisha hili, nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba, hatukukaa kimya, kesi hizi zipo mahakamani na nyingine wameshachukuliwa hatua katika kuwajibishwa ili hali hii isijirudie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi *Tax Payers Money* zina wajibu wa kuonekana. Afya, maji, elimu na barabara zinahitajika zionekane huko. Kwa hiyo, tupo pamoja, kilichotukwaza hapa katika hizi bilioni kumi na tano ni zile ambazo tumeshindwa kuzikusanya kutokana na sababu mbalimbali. Hata hivyo, Waheshimiwa Wabunge waliochangia wamesema *TRA* ijiimarishe katika makusanyo na sisi tuna wajibu wa kuhamasisha *TRA* wasichelewe katika makusanyo ili kile tulichokubaliana tukikusanye kwa wakati na wale ambao hawalipi hiyo kodi ambayo tumekusudia, tuwachukulie hatua kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niweke rekodi sawa; zile *compressor* zilizonunuliwa Wizara ya Maji, hazikuwa *compressor* hewa, lakini tofauti yetu hapa ni bei. Vile vile wakati kesi ilipokuwa inaendelea, wale waliosushtaki, mahakama imeamuru tuwalipe hata zile gharama zao za tiketi na gharama zao za kukaa kwenye hoteli, hii

ndiyo iliyosababisha ikafikia shiligni bilioni 1.7. Nataka kusema kwamba, yale ambayo mmetusaidia, tutayafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nataka niseme Sheria yetu ya Manunuzi tumeona kidogo ina matatizo, tutaiteta hapa kwa marekebisho. Tayari tumeshaanza kuifanya mapitio na Baraza la Mawaziri limeshayakubali mapitio yale, tutaiteta ndani ya Bunge hili ili pamoja tuweze kuifanya marekebisho iweze kunusuru upotevu katika manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nataka nizungumzie hoja moja ambayo Mheshimiwa Dokta Slaa ameizungumzia ni uwiano wa sheria zetu. Sisi kama Wabunge, tuna nafasi kubwa sana katika kuondoa huo utata katika baadhi ya sheria zetu, tutajitahidi sana ili tuweze kuondoa huo utata katika baadhi ya sheria zetu na tuzilete hapa Bungeni ili tuweze kuzisawazisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Dokta Slaa amesema kwamba, tusichelewe kuchukua hatua. Mheshimiwa Anne Kilango vile vile amesisitiza kwamba, tusichelewe kuchukua hatua. Utakumbuka huko nyuma, hata Ripoti ya *CAG* ilikuwa inatoka baada ya miaka mitano, sita, zinapotoka zinakuwa hazina hata ladha, lakini sasa hivi tumeiimarisha Ofisi ya *CAG* na Ripoti zinatoka kila mwaka. Kwa hiyo, tutachukua hatua kila inapojoitokeza, lakini na Sheria yetu ya *Procurement* itaweza kuona mapema zaidi na hatua za mapema zaidi tutaweza kuzichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dokta Slaa, amezungumzia suala la *reallocation*; nataka niseme tu Mheshimiwa Sumari amepitisha Sheria ya *Appropriation Bill*, lakini katika hilo amezungumzia na *reallocation*. Bunge hili linaluhusu *reallocation*, lakini hoja yako ni thabiti kwamba, tutakapofanya zile *reallocation* kubwa ni wajibu wa Serikali kulitaarifu Bunge kwamba, hapa tumefanya *reallocation* hii, kwa sababu shughuli zote hizi ni zetu na fedha zote hizi ni zetu. Kwa hiyo, kuna haja ya kuarifiana kwa mambo ambayo Serikali imechukua juhudhi ya kufanya hiyo *reallocation*. Tumelipokea hili na Waziri wa Fedha amelisikia, kwa sababu Waziri yeyote anapotaka kufanya *reallocation* ni lazima apate kibali kutoka kwa Waziri wa Fedha. Tumelipokea na tutalifanya kazi kwa umoja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Kufuta na Kusamehe Madai ya Kodi pamoja na Riba liliridhiwa na Bunge*)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Kuchochera Maendeleo ya Jimbo wa Mwaka 2009
(*The Constituencies Development Catalyst Fund Bill, 2009*)

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana nilipoingia hapo mwanzoni hata maswali nilitaka kuyakata, kwa sababu nilikuwa naona tunachelewa. Mheshimiwa Waziri karibu. (*Makof/Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unapendekeza kutunga Sheria ya Mfuko wa Kuchochera Maendeleo ya Jimbo na kuweka utaratibu wa kusimamia na kuratibu miradi ya maendeleo itakayoanzishwa katika Majimbo ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunzishwa kwa Mfuko wa Kuchochera Maendeleo ya Jimbo, yaani *Constituencies Development Catalyst Fund (CDCF)*; ni moja ya hatua ya kuhamasisha maendeleo ya Majimbo ya Uchaguzi kwa Serikali kuchangia fedha moja kwa moja katika Miradi ya Maendeleo iliyoanzishwa na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakusudiwa kwamba, kuwepo kwa Mfuko wa Kuchochera Maendeleo ya Jimbo pia kutasaidia upatikanaji wa msaada wa haraka au dharura kwa shughuli za maendeleo hususan katika Miradi ambayo imepangwa na Kamati ya Maendeleo ya Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo ni kuimarika kwa shughuli za maendeleo katika ngazi ya Kitongoji, Kijiji, Mtaa hadi Kata na Jimbo kwa ujumla. Inatarajiwa kwamba, uanzishwaji wa Mfuko wa Kuchochera Maendeleo ya Jimbo, utawezesha ushiriki wa karibu wa wananchi kuitia Mbunge wao katika shughuli za maendeleo ya Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uanzishwaji wa Mfuko huu unategemewa kuinua ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo, kukuza ajira na kuongeza uwazi katika ugawaji wa rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu nne na kwa muhtasari ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza, inapendekeza kuweka masharti ya awali, ikiwa ni pamoja na jina linalopendekezwa, yaani Mfuko wa Kuchochera Maendeleo katika Jimbo (*The Constituencies Development Catalyst Fund (CDCF) Act, 2009*), ambapo matumizi yake yatakuwa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Tafsiri ya misamiati, ambayo maelezo yake yapo katika ukurasa wa tano mpaka wa sita wa Muswada huu.

Sehemu ya pili, inapendekeza masharti kuhusu uanzishwaji wa Mfuko wa Kuchocha Maendeleo ya Jimbo. Katika sehemu hii, inapendekezwa kuwekwa masharti kuhusu usimamizi wa Mfuko wa Kuchocha Maendeleo ya Jimbo, shughuli za Kamati, Uongozi wa Mfuko na taratibu za utoaji wa fedha kutoka katika Mfuko huu. Sehemu hii kwa ujumla, inaelezea *Management* ya Mfuko huu na ugawaji fedha kwa vigezo maalum. Vigezo hivyo ni pamoja na asilimia 25 ya fedha hiyo kugawanywa sawa katika Majimbo yote. Asilimia 40 itagawanywa kulingana na idadi ya watu, asilimia 20 itaangalia hali ya umaskini na asilimia 10 itaangalia eneo la kijiografia. Maeleo zaidi yako ukurasa wa saba mpaka wa kumi wa Muswada huu.

Sehemu ya Tatu, inapendekeza kuwepo kwa Kamati ya Maendeleo ya Majibu na kuainisha majukumu ya Kamati hizo. Sehemu hii inaelezea uanzishwaji wa Kamati ya Mfuko wa Kuchocha Maendeleo ya Jimbo, ambao utaitwa *Constituency Development Catalyst Committee*, ambao utakuwa na Wajumbe sita na wa saba ni Mwenyekiti; ikiwa Wajumbe hao ni pamoja na Mbunge, Mwenyekiti, Watendaji wawili wa Kata, Madiwani wawili, mmoja lazima awe mwanamke. Kwa upande wa Tanzania Visiwani, Shehia katika lile eneo la Watendaji wa Kata na Mwakilishi mmoja wa NGO. Maeleo zaidi yako katika ukurasa wa 10 mpaka wa 12.

Sehemu ya nne, inapendekeza kuweka masharti kuhusu kuandaa orodha ya Miradi ya Jimbo na kuweka utaratibu wa uwasilishaji wa orodha hiyo katika Halmashauri ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Aidha, katika sehemu hii, inapendekezwa kuwekwa masharti kuhusu vigezo vya Miradi kuweza kugharimiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Maeleo zaidi yako katika ukurasa wa 12 mpaka wa 13 wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano, inapendekezwa kuwekwa masharti kuhusu utekelezaji wa Miradi. Inapendekezwa kwamba, Miradi yote ya Majimbo itatekelezwa kwa kushirikisha Idara za Serikali. Inapendekezwa kuwekwa masharti kuhusu ununuzi wa huduma zinazohusiana na Miradi, ambapo huduma hizo zitapaswa kununuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sura Namba 410. Ili kuwepo matumizi na ununuzi mzuri wa vifaa vya mradi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, atakuwa na mamlaka ya kukagua hesabu za fedha ambazo zitatolewa na Mfuko kwa lengo la udhibiti. Kwa hiyo, katika sura hii msisitizo ni kwamba, *Public Finance Act*, Sura ya 348 na *Public Procurement Act*, Sura ya 410, vyote vitazingatiwa katika fedha hizi. Maeleo zaidi yako katika ukurasa wa 13 mpaka wa 14 wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita, inapendekeza kuweka masharti kuhusu aina za miradi ambayo inaweza kugharimiwa na Mfuko wa Kuchocha Maendeleo ya Jimbo. Hapo linalosisitizwa ni kwamba, Miradi hii lazima iwe ya kijamii, yaani *community based* na si vinginevyo. Isiwe Miradi ya Kidini wala ya Kisiasa. Maeleo zaidi yako katika ukurasa wa 14 mpaka 15 katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu saba, inapendekeza kuweka masharti kuhusu masuala ya fedha, uendeshaji, utawala na usimamizi wa Mfuko wa Kuchocha Maendeleo ya Jimbo; na hapa kinachosisitizwa zaidi kwamba, fedha hizi zitaingizwa

moja kwa moja kwenye akaunti ya Jimbo, chini ya usimamizi wa Halmashauri na Afisa Masuhuli ni Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya husika. Pia, watia sahihi katika fedha hizo ni Watendaji wa Halmashauri. Maelezo zaidi yako katika ukurasa wa 15 mpaka wa 17 katika Muswada huu.

Sehemu ya nane na ya mwisho, inapendekeza kuweka masharti ya jumla, hususan kumpa uwezo Waziri muhusika, kutunga kanuni zitakazosaidia usimamizi bora wenye ufanisi kwa Mfuko wa Kuchochea Maendeleoa ya Jimbo. Hapa pia inaainisha makosa yanayoweza kufanywa na mtu yejote katika uendeshaji wa Mfuko. Makosa haya ni pamoja na kutumia vibaya fedha za Mfuko, kumsaidia mtu au kusababisha mtu atumie vibaya fedha hizo na mali za Mfuko kinyume na madhumuni yaliyokusudiwa. Sehemu hii inaweka adhabu kali ya faini isiyozidi shilingi milioni kumi na tano au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo zaidi yako ukurasa wa 17 na wa 18 wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE (MWENYEKITI WA KAMATI KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(5), Toleo la Mwaka 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Muswada wa Sheria wa Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo wa Mwaka 2009 (*The Constituencies Development Catalyst Fund Bill, 2009*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijafanya hivyo, naomba nieleze kwa muhtasari, hatua iliyotangulia kabla ya kuujadili Muswada huu hapa tulipofikia. Kama unavyofahamu, Muswada ulio mbele ni wa Kihistoria katika Bunge na Nchi yetu kwa ujumla. Kutokana na hali hiyo, Muswada huo umegusa hisia za wananchi mbalimbali, baadhi wakiunga mkono na wengine wakiupinga vikali kutokana na sababu mbalimbali. Wapo wananchi waliota maoni kupitia vyombo vyao habari kuwa, Muswada huo unakiuka Katiba kwa maana kwamba, kuwepo kwake kutawafanya Waheshimiwa Wabunge, waingilie mamlaka ya utendaji. Aidha, wapo walioonesha wasiwasi kuwa, Wabunge kwa kutumia sheria itakayotungwa kutokana Muswada huu, watakuwa na mamlaka moja kwa moja kuamua matumizi ya Mfuko huo kwa utashi wao. Pia wapo waliodai kuwa, Halmashauri za Miji, Wilaya na Manispaa, zina udhaifu mkubwa kiutendaji, hivyo kuanzishwa kwa Mfuko huu ni kilelezo cha kuwepo kwa umuhimu wa Bunge kuongeza usimamizi wake. Wengine walikwenda mbali zaidi, kwa kutoa mifano ya nchi nyingine ambazo Mfuko kama huu haukuwa na mafanikio yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maoni machache tu, lakini yapo mengi ambayo mmeyasikia na Waheshimiwa Wabunge wengine mmeshiriki moja kwa moja katika vyombo vyao habari, kufafanua kwa kina maudhui ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo na maoni hayo, naomba nieleze kwamba, mchakato wa kuanzisha Mfuko huu ni wa muda mrefu. Ulitokana na hoja za msingi za Waheshimiwa Wabunge, kwa nyakati tofauti ndani na nje ya Bunge, wakielezea uzoefu wao katika kutekeleza majukumu yao ya kuwakilisha wananchi. Kufuatia hoja hizo, Serikali na Bunge kwa ujumla, viliunda Kamati mbalimbali kufanya utafiti wa kina ndani na nje ya nchi kuhusu umuhimu na utaratibu bora wa kuanzisha Mfuko huu. Mtoa hoja ameeleza jinsi Mifuko kama hii ilivyofanya kazi. Inatosha kueleza kuwa, Kamati hizi zililinganisha sheria mbalimbali zilizotumika katika nchi za wenzetu, ikiwa ni pamoja na kuangalia uzoefu wa nchi hizo kuhusu Mfuko huo na kuchukua mambo ya msingi ambayo yanaendana na mazingira ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha tafiti hizo zilizofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 114 (9), Kanuni za Bunge, Kamati yangu iliwaalika wadau tarehe 26 Julai, 2009 katika kikao kilichofanyika Ofisi ya Bunge Dodoma ili kupata maoni yao kwa lengo la kuisaidia Kamati kuboresha Muswada huu. Utaratibu huu wa kualika wadau (*Public Hearing*) si mgeni, ulikuwepo tangu zamani. Hata hivyo, Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, zimeuboresha zaidi na kuwa sharti muhimu la kuwahusisha wananchi karibu zaidi katika mchakato wa kutunga sheria na kuhusu mambo yanayohusu maslahi ya Taifa yanayoshughulikiwa na Bunge lako Tukufu kupitia Kamati zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza azma hiyo, Kamati iliwaalika Wadau wakiwemo asasi mbalimbali kama vile Policy Forum, CHAVITA, UVEJUTA, TASA, Chuo Cha Elimu ya Biashara Dodoma, Uongozi wa Vyuo Vikuu Dodoma, Dar es Salaam na Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa wadau kama nilivyoeleza hapo juu, Kamati ilimpa fursa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mheshimiwa Celina Kombani, kuwasilisha malengo na madhumuni ya Muswada huo, kama alivyoeleza wakati alipowasilisha hoja hii muda mfupi uliopita. Kwa ujumla, Kamati inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Serikali kwamba, yamezingatia mambo muhimu katika kuhimiza, kuhamasisha na kuchochea maendeleo ya Jimbo.

Pamoja na hayo, ukiacha masahihisho machache ambayo Kamati ilipendekeza yafanyiwe marekebisho hususan katika ibara ya tatu ambapo tafsiri ya neno *Committee*, Kamati imeshauri kuwa lifanyiwe marekebisho na kusomeka kuwa *Constituency Development Catalyst Committee*. Mapendekezo mengine ni kuondoa maneno ya pembeni, yaani *side note* yaliyojiteza katika ibara ya 12 ya Muswada yanayosomeka; *Member of Parliament to collect project proposals*, yababilishwe na kuwa *Member of Parliament to keep records* ili kuleta mantiki iliyokusudiwa katika ibara hiyo na kufanya masahihisho katika ibara hiyo kwenye neno *CDF* na kulifanya lisomeke *CDCF*; mapendekezo yake haya yalikubaliwa na Serikali na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mapendekezo haya, Kamati yangu inapenda kutoa ushauri kwa ujumla kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuelimisha wananchi kuhusu matumizi na manufaa ya Mfuko huu na namna Miradi yao itakavyoweza kusaidiwa. Hii ni pamoa na kuzingatia kuwa, Fungu la Mfuko huu si kubwa, ambalo litatolewa kulingana na mazingira ya Mradi ulioibuliwa na wananchi.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na vyombo vya dola, isimamie Kanuni za Fedha na uadilifu kwa watumishi wa umma waliopo katika Halmashauri za Miji, Wilaya, Manispaa na Majiji ili kufanikisha Miradi yote ya Maendeleo ukiwemo Mfuko huu.

Serikali iwe makini na *propaganda* zinazoenezwa na upotoshwaji wa makusudi, unaofanywa na baadhi watu au vikundi dhidi ya Mfuko huu. Ninalisema hili kutokana na uzoefu ambao Kamati yangu ilipokutana na wadau ambao walikuwa wengi, walionekana kuupinga bila kuzingatia uchambuzi na utafiti wa kina uliofanyika wakati wa mchakato wa kuandaa Muswada huu. Aidha, wapo wengine ambao hata hawakuusoma Muswada katika hali yake iliyopo sasa. Katika hali ya kawaida, tungetegemea kuwa, kama kweli wapo waliofanya utafiti kutembelea nchi za kigeni kuona jinsi Mfuko huu unavyofanya kazi, basi kwanza kabisa wangeanza kufanya utafiti kwenye Jimbo la Mbunge, wakajifungie huko na kukaa siku kadhaa, kuona jinsi Mbunge anavyowajibika kuchangia Miradi ya wananchi wake. Kwa kufanya hivyo, pengine wangejua nini maana ya Ubunge na haja ya kuwepo kwa Mfuko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzalendo wa kweli, anayefahamu maana ya maendeleo na aliyeusoma Muswada huu kwa kina, nitashangaa kama ataupinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa ujumla, kwa kuelewa nia njema ya Bunge lako Tukufu, kushawishi kuwepo kwa Muswada huu. (*Makofi*)

Aidha, nakushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge, ambao hawakuonesha itikadi zozote za kisiasa katika kuushughulikia Muswada huu katika hatua mbalimbali, kwa nia ya kuweka misingi ya uhamasishaji wa maendeleo. (*Makofi*)

Vilevile nawashukuru Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jonson Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watalaam wao, kwa kushirikiana vyema na Kamati yangu na kutoa maelezo ya kina, yaliyowezesha Wajumbe wa Kamati yangu kutoa michango yao. (*Makofi*)

Kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri waliyoonesha wakati wote wa kuchambua Muswada huu na naomba kwa heshima na taadhima niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani Maneno - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Benedict

Ole-Nangoro, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Yusuf Rajabu Makamba, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Rajab Hamad Juma.

Mwisho kabisa, nawashukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Charles Mloka, Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Athuman Hussein na Ndugu Elihaika Mtui na watumishi wengine, kwa kufanikisha shughuli za Kamati kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

MHE. HALIMA J. MDEE (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Willibrod P. Slaa, naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Chachu ya Maendeleo ya Jimbo wa Mwaka 2009 ama *The Constituencies Development Catalyst Fund Act, 2009 (CDCF)*.

Kwanza Kabisa, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa majaliwa yake ya uzima kwetu sote. Naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuwasilisha maoni juu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*Constituencies Development Catalyst Fund*), kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu Namba 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, kwa imani yao kwangu, kunipa nafasi hii ya kuwa Mnadhimu Msaidizi wa Kambi ya Upinzani (*Assistant Chief-Whip*). Pia natoa shukrani hizo kwa Viongozi wangu wa Chama changu cha Demokrasia na Maendelo (CHADEMA), kwa kunipa ushirikiano ndani na nje ya Bunge. Natoa ahadi kuwa, nitaendelea kukitumikia chama changu kadiri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unapendekeza kutunga Sheria ya Mfuko wa Kuchochera Maendeleo ya Jimbo na kuweka utaratibu wa kusimamia na kuratibu Miradi ya Maendeleo, itakayoanzishwa katika Majimbo ya Uchaguzi. Uzoefu katika nchi nyingine ambazo zinatumia utaratibu huu, unaonesha kwamba, Mfuko wa Jimbo kama ukitumiwa kwa umakini ni moja ya hatua za haraka za kuhamasisha Maendeleo ya Majimbo ya Uchaguzi. Mfuko huu utawasaidia sana wananchi kupata maendeleo, kwani uzoefu umeonesha kwamba, Miradi mingi ya Maendeleo inaishia katika Mikoa michache sana. (*Makofî*)

Mfuko huu ni muhimu kutokana na ukweli kwamba:-

(i) Serikali itachangia moja kwa moja katika Miradi ya Maendeleo iliyanzishwa na wananchi kwenye ngazi ya vijiji, mitaa au vitongoji, kwa jinsi na kadiri itakavyobuliwa na kutathminiwa kwa vigezo vilivyokubalika.

(ii) Mfuko husika utasaidia upatikanaji wa msaada wa haraka au dharura kwa shughuli za maendeleo hususan katika miradi ambayo imepangwa na Kamati ya Maendeleo ya Jimbo.

(iii) Uanzishwaji wa Mfuko husika utawezesha ushiriki wa karibu wa wananchi kupitia katika shughuli za maendeleo za Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumekuwa tukisoma kwenye vyombo vya habari, kuna hofu kubwa imejengeka mionganini mwa baadhi ya Watanzania, ambao ni wananchi tunaowatumikia, juu ya uanzishwaji na ufanisi wa Mfuko husika, hasa baada ya matamko mbalimbali kutoka kwa asasi zisizo za Serikali; nyingi zikipinga uwepo wa Mfuko husika, kwa maelezo kwamba uwepo wake unakinzana na matakwa ya ibara namba 63 na 64 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambazo zinalezea mipaka ya majukumu ya kikazi baina ya mihimili miwili ya dola, ambayo ni Bunge na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja na misimamo ya asasi hizo, zinadhahirisha kwamba, watusika ama hawajausoma na kuuelewa vizuri Muswada husika ama waliamua kupotosha kwa makusudi, hivyo kuua dhana nzima ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kama ilivyoainishwa na Sheria. Nimelazimika kutoa ufanuzi husika ili wananchi watuelewe kwamba, kinachofanyika hapa si kutunisha Mfuko binafsi wa Mbunge kama ambavyo baadhi ya asasi zinataka ieleweke, bali ni fursa ya kurudisha mamlaka kwa wananchi, kuweza kuamua vipaumbele vyao vya maendeleo na kwa msingi huo, kutekeleza dhana nzima ya kupeleka mamlaka vijijini kimatendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza na hoja nzima ya Kikatiba na mgawanyo wa mamlaka baina ya mihimili hii miwili ya dola; kifungu cha 4 cha Muswada kinachozungumzia uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, kinatanabainisha wazi kwamba, usimamizi na uendeshwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (kwa mantiki ya fedha zote zitakazotoka serikalini kwenda kwenye Majimbo ya Uchaguzi), utaratibiwa na Waziri mwenye dhamana ya kusimamia Serikali za Mitaa kwa Majimbo yaliyopo Tanzania Bara na Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano kwa Majimbo ya Uchaguzi yaliyopo Zanzibar. (*Makofi*)

Kwa ufupi ni kwamba, fedha husika zinaingizwa kwenye Bajeti na zinaratibiwa na Wizara hizo mbili na si vinginevyo! Kwa mantiki hiyo, ni upotoshaji wa hali ya juu kutaka ieleweke kwamba, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo unaendeshwa, kusimamiwa na kuratibiwa na Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kudhibiti matumizi mabovu ya fedha za umma, matakwa ya kisheria yanazitaka Kamati za Maendeleo ya Jimbo, kuwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa Mawaziri wenye dhamana ya usimamizi wa fedha

husika, ndani ya siku thelathini baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha. Kukosekana kwa taarifa husika, kutapelekea Jimbo kukosa mgawo wake katika mwaka mwingine wa fedha. Rejea kifungu cha 7(1), (2) and (3) cha Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaweza angalizo kuhusiana na kifungu cha 10(1) cha Muswada, kiwekewe utaratibu na misingi imara katika kanuni zitakazotungwa na Mheshimiwa Waziri juu ya uteuzi wa Wajumbe watakaouna Kamati ya Jimbo, isije ikawa ni kwa utaratibu atakaoupanga Mwenyekiti wa Mfuko. Jambo linaloweza kupoteza maana nzima ya uanzishwaji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu, itakuwa ni jambo la ajabu kwa fedha husika kutumika katika matumizi ambayo hayakukusudiwa, hasa ikizingatiwa kwamba, maamuzi ya nini kifanyike na wapi yanaibuliwa na wananchi wenye kipitia vipaumbele vya Kata. Rejea vifungu vya 10(4) na 12) na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Jimbo, inayowajumuisha Mbunge wa Jimbo, Afisa Mipango wa Wilaya, Madiwani wawili ambao ni Wakazi wa Jimbo husika, Maofisa Watendaji wa Kata kwa Tanzania Bara na Shehia kwa Tanzania Visiwani na Mwakilishi mmoja toka asasi zisizo za Kiserikali (*NGO*), atakayechaguliwa na Kamati ya Maendeleo ya Jimbo kutoka kwenye asasi isiyo ya Kiserikali iliyo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muundo huu, Mbunge peke yake hana mamlaka yoyote ya kimaamuzi, pasipo kuwashirikisha Wajumbe wengine wa Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria, fedha zote za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, zitaelekezwa kwenye akaunti ya Jimbo, ambapo Sheria imetambua makundi mawili ambayo yatakuwa na mamlaka ya kutoa fedha za Mfuko (*signatories*), kwa matumizi ya Maendeleo ya Jimbo. Rejea kifungu cha 22(3).

Makundi hayo ni kundi A, ambalo linajumuisha Mkurugenzi wa Halmashauri na Afisa Mipango wa Halmashauri na kundi B linalojumuisha Mweka Hazina wa Halmashauri na Mhasibu wa Halmashauri. Hali kadhalika, Sheria imetamka bayana kwamba, hakuna fedha yoyote itakayotolewa pasipo kuwepo kwa muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Jimbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya ni wazi kabisa, Mbunge kama ilivyo Wajumbe wengine, hana mamlaka binafsi na fedha husika. Jambo la msingi ni kila mmoja wetu kutekeleza wajibu wake, kuhakikisha kwamba malengo haya mazuri ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo yanafikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa hofu ambayo imejengeka mionganoni mwa Watanzania kuhusiana na Mfuko wa Maendeleo Jimbo, Kambi ya Upinzani inawataka wahusika wote wa utekelezaji wa Mfuko huu, kuwa na uwazi na ushirikishwaji wa karibu wa wananchi katika uendeshwaji wa miradi. (*Makofi*)

Hali kadhalika ili kuweza kutimiza lengo zima la kuhamasisha maendeleo ndani ya Jimbo, kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kwamba, kama kuna kandarasi zozote

za ujenzi ama kazi ambazo zinaweza kufanywa na wataalam toka ndani ya Jimbo husika, upendeleo maalum lazima ufanywe kwa wakazi wa eneo husika. Ni muhimu kwa kadiri itakavyowezekana, kuhakikisha kwamba, wananchi wenyewe ujuzi katika Majimbo husika, wanapata fursa ili pamoja na mambo mengine, waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba, kuna miradi mbalimbali inayoendelea Tanzania, ambayo kwa namna moja ama nyingine, inahusisha ushirikishwaji wa wananchi katika uibuaji wa miradi, kwa mfano, Miradi ya TASAF. Hivyo basi, ni muhimu wakati tunajadili suala la CDCF, tuangalie ni kwa namna gani tutaihusisha Miradi ya aina hii ili kuongeza uwezo na uwajibikaji. Suala hili ni muhimu sana kuliangalia kwa lengo la kuepuka kufanya kazi zile zile na au kuepuka *duplication*. Kama Kambi ya Upinzani inarudia kuwa, hoja ya msingi ni kuwa Mfuko huu hauna nia ya kuanzisha njia nyingine za kupeleka fedha kwa wananchi na hivyo kuwachanganya. Mfuko huu pia unalenga kukamilisha nguvu za wananchi, pale ambapo Mifuko mingine imefika mahali inashindwa kukamilika kwa sababu zinazokubalika, hasa kutokupatikana kwa fedha za kutosha kutoka kwa wahisani wa Mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu wa Chachu ya Maendeleo ya Jimbo, unaweza kufanya masuala mapana zaidi ya Miradi ya kawaida ya Maendeleo, kama ilivyo Kenya ambapo wanafunzi wengi wanapata udhamini wa kusoma katika shule mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Vyuo Vikuu kuitia fedha za CDCF, pale itakapoonekana na kukubalika na Kamati husika kuwa hicho ndiyo kipaumbele cha eneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwazi na uwajibikaji ndio silaha pekee ya kuhakikisha fedha za umma zinatumika vizuri. Ni jukumu letu Wabunge, tukiwa sehemu ya Wajumbe wa Kamati za Maendeleo za Jimbo, kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa kwa matumizi ya maendeleo ya Jimbo zinatumika kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Halima Mdee na hasa kwa kuunga mkono hoja. Mzungumzaji wetu wa kwanza atakuwa Mgana I. Msindai, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa na Mheshimiwa Simbachawene ajiandae.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza kwenye Muswada huu wa Mfuko Maalum wa Jimbo. Awali ya yote, namshukuru sana Spika wa Bunge. Naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tatu na ninawashukuru sana Mabalозi wa nchi mbalimbali, walioshiriki katika kuuweka sawa huu Mfuko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nalishukuru sana Bunge letu. Wabunge wote tumekuwa wavumilivu, Mfuko huu tuliupendekeza siku nyingi, lakini wenzetu wa pembeni walipoanza kusema sema maneno tukanyamaza na kuamua tujipange vizuri na

tukateua wenzetu wakatembelea maeneo mbalimbali, tukawashirikisha Mabalozi kuwaeleza umuhimu na ulazima wa Mfuko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa umefika wakati wa huu Mfuko kuanza. Vile vile nawashukuru sana wadau mbalimbali, asasi mbalimbali za kiraia ambazo walianza kuuzungumzia Muswada huu kabla hawajauona. Walianza kuleta hisia zao kabla ya kuona tunataka kufanya nini. Lengo la Serikali ya Awamu ya Nne, lengo la Bunge hili na lengo la watu wote wanaopenda maendeleo, tunataka kupeleka maendeleo karibu na wananchi wetu. Kupeleka maendeleo karibu na wananchi wetu ni kupeleka fedha za miradi wazipangie wao zifanye nini. Mimi nina uhakika, jinsi Mfuko huu utakavyofanya kazi nzuri, zile fedha nyingi zinazoletwa na wafadhili mbalimbali na zinazotolewa na Serikali, tunalalamika hapa Bungeni, zitapita kwenye Mfuko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaloomba, hawa wenzetu wenye asasi, sisi Wabunge na Serikali tumetangulia kule chini na wao wajitahidi tukutane, asasi zao zihame mijini ziende vijijini waliko walengwa. La sivyo, hata wale wanaowafadhili watabadili njia na hiyo hela yote ipite kuptitia Mfuko huu. Mimi nina uhakika kabisa, fedha hizi zitafanya kazi iliyokusudiwa, hakuna Mbunge asiyependa watu wake wapate maendeleo. Sasa hivi tunajikamua vimishahara tunavyopata na posho zetu, tunakwenda kuchangia miradi ya wananchi wetu.

Kwa hiyo, nina imani sana na sisi tunaishukuru sana Serikali yetu iko makini, kuna wafadhili walikuwa wanapeleka fedha zao moja kwa moja kwenye miradi wanayoitaka wao na maeneo wanayotaka wao, Serikali ikawaambia hapana zipite Serikalini. Serikali ndiyo iseme itapeleka wapi, ndiyo maana tukaanzisha *Basket Fund* na hela zote za afya na miradi mingine inapita huko na hizo hela tunakuwa na uwezo na usimamizi zinakaguliwa kwa njia inayokubalika. Sasa hivi tunawaambia wenzetu wa asasi za kiraia, CAG ataanza kukagua fedha zao, kwa sababu hatujui zinafanya nini. Ukienda Iramba Mashariki, hatuna asasi hata moja na Wilaya nyingi hapa Tanzania. Mimi nipo kwenye Kamati ya LAAC, tumetembea nchi nzima, unakuta mambo ya ajabu sana; kwanza asasi hazipo, unakuta wananchi wameanzisha Mradi, shule imefikia kwenye renta, Halmashauri haina uwezo! Mfuko kama huu ndiyo kazi yake kusaidia zaidi wananchi, wanapochimba maji wamekwama Mfuko huu unasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nina imani kubwa sana, huu Mfuko utafanya kazi na sisi Wabunge wa Bunge hili, chini ya Mheshimiwa Sitta, tunaiga nyendo zake za usafi na tutasimamia sawa sawa na kule kwenye Halmashauri zetu kama Muswada ulivyosema; wale watendaji wetu wa Halmashauri wapewe semina za kutosha waelekezwe na zile *regulations* zikitoka ziende moja kwa moja kule.

Mtu wa kwanza wa kusimamia huu Mradi na matumizi ya hii hela ni wananchi wenyewe, kwa sababu hakuna wananchi watakaopelekewa Mradi na Mfuko wa Jimbo umechangia halafu wauchezee. Mbunge ndiyo mkombozi wa wananchi na vilio vyote vya wananchi vinakwenda kwa Mbunge.

Pili, Mfuko huu utawashirikisha Madiwani wetu wa Kata, kwa sababu miradi yote iko kule kwenye Kata zao, kwenye vijiji na kwenye vitongoji. Kwa hiyo, tutashikana bega kwa bega na Madiwani wetu na ndiyo maana kwenye Kamati watakuwepo. Nina imani kabisa na sina wasiwasi. Niwaambie Madiwani wangu na Wananchi wa Iramba Mashariki na Wananchi wote wa Tanzania kwamba, wamepata ukombozi. Wale watakaojaribu kwenda kupeleka maneno, wananchi wawakatae wanawapotosha wachukie mambo mazuri yanayokwenda kwao kwa maendeleo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Wilayani tuna Wakaguzi wetu wa Ndani, tunaomba muda mwangi wawe wanafutilia hii Miradi na Miradi mingine inayokwenda. Wao ndiyo jicho la Mkurugenzi, wao ndiyo jicho la *External Auditors*, wao ndiyo jicho la Bunge hili na taarifa zao ziwe zinatoka kwa makini. Hakuna hela itakayotolewa bila kukaa kikao na kupitisha mihtasari na mihtasari hiyo itakwenda Wilayani na itafika mpaka kwenye Kamati zetu za Bunge, kuhakikisha kwamba, kule kwa Dkt. Slaa kule Mangola, kazi zilifanyika, Mradi ultengeneza mtaro wa umwagiliaji na tutakwenda kukagua. Kwa hiyo, nirudie kusema hawa wenzetu wa asasi za kiraia sasa watulie, watupe muda, baada ya miezi sita au mwaka ndiyo waje waseme tuliwaambia hamtofanya vizuri, lakini wataogopa hawatakuja kwa sababu kazi itakayofanyika itakuwa ya maendeleo kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali yetu ni kupeleka madaraka kwa umma na nashukuru Serikali imeona umuhimu wa kutumia njia hii ndiyo iwe ya kwanza. Kila siku tunalalamika hapa, hela za UKIMWI hazifanyi kazi inayokusudiwa, hela za UKIMWI haziwafikii wananchi wanaohusika. Sasa nina imani wataona Mfuko huu unavyofanya kazi. Wakishaona usimamizi wa Mfuko huu, zile fedha ambazo zinatakiwa zifike kule kwenye vitongoji na vijijini, zitapitia chini ya Mfuko huu. Mbunge na Diwani, ndiyo wanaojua matatizo ya wananchi wa kule chini, asasi ziko mjini tunazona, sasa njoooni mfungue ofisi kule Mwangeza, Matara, Meatu na Kongwa Vijijini. Hameni mijini, la sivyo hizo hela zitawahama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimeridhika na huu Mfuko na naomba niishie hapa, nirudie tu kusema, kweli Serikali ya Awamu ya Nne inataka kuwapelekea wananchi wake maendeleo bila kujali upande. Mfuko huu upo Zanzibar na Tanzania Bara; hauna itikadi na hiyo ndiyo itakayotuletea maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. DKT. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. Jambo lolote jipya linakuwa gumu, linaleta hisia na watu wanakuwa na mashaka, lakini mashaka huondoka wanapolielewa. Vile vile jambo lolote jema, haliwezi kuachwa kutekelezwa kwa sababu kuna Upinzani. Unahitaji ujasiri kutekeleza jambo ambalo kwa dhamira yako unadhani ni la kweli, ni sahihi, lina manufaa kwa wananchi na linamnufaisha yule ambaye tunataka kumhudumia, yaani mwananchi wa chini kabisa na kwa hilo huna sababu ya kuwa na woga kwa sababu kuna Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uzoefu pia kwa wale ambao hawafahamu pale Kigoma, CHADEMA tunaiendesha Serikali ya Wilaya ya Kigoma Mjini, kwa ushirikiano kati ya CCM na CHADEMA. Tulipoanzisha jambo hilo tulipigwa vita, tulipokuwa tunajadiliana tulitaka kufukuzwa. Tulipokuwa tunajadiliana katika ngazi ya Makatibu Wakuu, tuliambiwa kwamba, tutafukuzwa hata kwenye Chama, mnauzza Chama. Leo watu wa Kigoma ni mashahidi, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma, imeendeshwa kwa ushirikiano; na Tanzania ni mfano kwa Afrika nzima, kufanya Serikali ya mseto ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha CHADEMA na hakuna vita wala mgogoro wowote wanafurahi.

Bahati nzuri, nadhani Mheshimiwa Ngwilizi yupo hapa, kwa sababu ndiyo tuliotaka kufukuzwa wakati ule. Kama mimi na Ngwilizi tusingekuwa na ujeuri wakati ule wa kukaa chini na kukubaliana mambo fulani fulani, tukasema ni ya kutoa *give and take*, leo tusingekuwa na amani kwa sababu mnajua kilichotokea, Madiwani walikwenda kuchukuliwa mpaka hospitalini kwa *drip* kwenda kupiga kura, kwa sababu kulikuwa na mtafaruku mkubwa. Sasa historia hiyo ni ndefu, sitaki kuisema, lakini nimeitumia kwa mfano wa kitu unachohitaji kukiamini na kukitekeleza, kwa sababu dhamira yako ni safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia la pili, historia ya Mfuko huu, kwa Waheshimiwa Wabunge waliokuwepo Bunge la 1995 mpaka 2000, Kamati ya Fedha sitaki kutaja majina, watakumbuka hoja hii ilivyokuwa inajitokeza mara kwa mara. Ninawashangaa leo wanaposema eti imeletwa leo au sasa kana kwamba ni kitu kimeshtukizwa. Bunge lina utaratibu wake wa kufanya kazi, mchakato huu ni wa zaidi ya miaka 11-12, lakini hatuendi kupiga kelele huko nje, hatuendi kuwaambia wananchi na hakuna Muswada wowote katika hatua za awali, wananchi wamekwenda kuulizwa. Ndiyo maana *Public Hearing* inakuja, Muswada umeshatangazwa umekuwa *document* ya umma, *Public Document*. Sasa ukishakuwa *public document*, kila mmoja yuko huru.

Wenzetu wameanza kuujadili kabla haujawa hata *public document*, kila anayejua Kanuni za Bunge anajua ni kwa nini na labda niweke vizuri kwa nini hata hatukujib; hatukujib kwa sababu sisi Kanuni za Bunge hazituruhusu kuzungumzia Muswada ambao upo kwenye mchakato haujawa *gazetted*; ni Sheria. Kwa hiyo, siyo kwamba tulikuwa tunaogopa au tulimhofu mtu, tunafuata Kanuni na Bunge linafanya kazi kwa Kanuni. Kwa hiyo, tunajaribu kufuata Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu yoyote kwamba, kuna kitu labda kilifichwa, kuna kitu kimeharakishwa, mchakato ni mrefu sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na wenzangu, tuliokuwa chini ya Kamati ya Ndugai toka 1999, bado tukarudi kulifuatilia kwenye Kamati ya Ndugai Mwaka 2007.

Mwaka 2007 mpaka leo si jana, ni kazi iliyofanywa, imetafitiwa na tumeona nchi mbalimbali. Wenzangu wamesema, sihitaji kurudia. Niseme tu, nitumie Sheria hii kwa yale mambo ambayo wenzangu walionitangulia hawajayasema, kuwaondolea Watanzania hofu. La kwaza, lipo kwenye kifungu cha nane cha Muswada, lipo kwa Kiingereza, naomba nitafsiri labda Kiswahili changu kitakuwa cha Kimbulu hakitakuwa vizuri

nisameheni. Inasema hivi: Mradi au sehemu yoyote ya Mradi huu, haitahusu zawadi binafsi *in cash*, yaani kwa fedha au *in kind*, yaani kwa vitu. Hiyo inapigwa marufuku na haitahusishwa vitu hivyo, zawadi hizo hazitakuwa kwenye *list* itakayowekwa inayopelekwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo. Maana yake ni kwamba, ile hofu ya kwamba wakati wa kampeni sasa tukishaondoka hapa kampeni mwaka kesho Wabunge watatumia hii kama takrima, kama zawadi, kama nini, imepigwa marufuku na Sheria hii, kifungu cha nane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtu yejote aliyesoma hii, hawezi tena kwenda kuzunguka Tanzania kuwaambia wananchi ambao hawaajaona na juzi nimeona Kiteto wa Osimajiro, jana nimeona Wahanang, watu ambao huu Muswada hawajauona wanasema tunaukataa. Sasa unakataa kitu ambacho hukijui? Mimi nafikiri Watanzania twende mbele zaidi ya ubinafsi na ushabiki, tunahitaji kwenda kisayansi. Ukikataa, kataa kitu kwa sababu una sababu ya kisayansi ya kukataa. Ukikataa kitu, usilete hisia ya kisiasa au ya kiitikadi.

Mimi niko Chama cha Upinzani, ambacho kinaunga mkono; kinajua kwamba, manufaa ya Mfuko huu ni mwananchi ambaye hana hela. Tungekuwa vyama vya ajabu na hatuna sababu ya kuwepo kama vyama kama hatutakuwa tunamfikiria mwananchi, badala yake tunafikiria manufaa ya vyama. Siasa inakuwa *rendered* bila mafanikio, tukiifikisha hatua hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe tena kifungu kingine cha pili, ambacho ni muhimu Watanzania *wakielewe*; Mfuko huu ambao leo tunaupitisha, tunaambiwa kwamba, tumekuja vyama vyote pamoja kwa sababu ni maslahi yetu. Kama Wabunge hawa tungejua ni maslahi yetu, tusingejiwekea masharti magumu kama haya ninayoyasoma sasa. Kifungu cha 28 kinasema hivi; kwanza, kinakwenda kwenye taratibu; yejote atakayetumia vibaya, atakayeiba, anafanya kosa la jinai. Kifungu chake kidogo cha pili kinasema; mtu yejote atakayepatikana na kosa la kuutumia vibaya Mfuko huo, atachukuliwa hatua za Kisheria na akithibitika amefanya kosa, adhabu yake ni faini ya shilingi milioni 15. Hivi ni Mbunge gani asiyetaka maisha yake akalipa hiyo shilingi milioni 15 tu hivi hivi? Haiishi pale au kifungo kisichozidi miaka mitano au yote mawili kwa pamoja. Hivi kweli Mbunge upo tayari kwenda kufungwa miaka mitano? Kwa maana hiyo, hii ni tahadhari kwa Mkurugenzi na Timu yake, wanaosimamia hizi fedha, wakichezea wakikubali kuyumbishwa, basi adhabu hii inawasubiri wao na sisi tutakuwa makini kuhakikisha haichezewi ili yejote atakayehusika, basi tusimamie adhabu hii iwakabe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge ndiyo kazi yetu kusimamia na wajibu wetu wa kusimamia haujaondoka kwa kuwa sisi tunapita tunaangalia. Niseme tu, kazi ya Mbunge ya kusimamia wenzetu wameipotosha kwamba, hakuna mgawanyo wa kazi. Nitoe mfano; Wabunge wote tunafanana katika hili; Mbunge yejote anapotembea kwenye vijiji vyake, sasa kama hatambe immoja au wawili hii ni bahati mbaya, lakini Wabunge wanapotembea kwenye maeneo yao, wanakutana na matatizo ambayo hayashughulikiwi. Mifuko yote ambayo wenzetu wanasema kuna hela nyingi na kuna Mifuko mingi; natoa mfano, Mifuko yote iliyopo hakuna hata immoja unaosaidia watoto

wa akina mama wajane, walemavu, maskini, ambao hawawezi kulipa ushuru na karo ya shilingi 20,000; wanakijiji wakiamua wanasema kipaumbele chetu ni ada. Hakuna mfadhili yejote Ulaya, anayekuuuliza kwa nini umetumia hizi fedha kulipa ushuru?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa haya yanaamuliwa pale na hakuna Mbunge yejote atakayeamka asubuhi nyumbani kwake, hakuna foleni kama hospitali utafikiri pale ni hospitali. Sasa haya matatizo tusaondoe kwa Mbunge mmoja mmoja kuchangia, tuyaondoe kwa mfumo ambao utasaidia kero hizi ziondolewe kwa njia zilizo wazi na taratibu ambazo ni za Kisheria, ndiyo lengo la Mfuko, hakuna lengo lingine zaidi ya pale. Tumekubaliana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema kwamba, kama tungetaka kujinufaisha mbona siku zote hiyo Katiba hawakusema? Pale Karatu, Wananchi wa Karatu ni mashahidi, Miradi ya Maji yote katika vijiji 35, mimi ndiye nimeandika *write-up*, nime-negotiate na wafadhili, nimekwenda kuitafuta, nimesimamia ujenzi, wakati huo sikuambiwa kwamba, ninakiuka Katiba! Sasa leo, hata hizo fedha zilipopatikana Waziri wa Fedha anafahamu, kuna siku alisema bwana wewe nikusaidie nini, akaniletea alama ya Serikali kushirikiana na wafadhili tuliyowaleta sisi. Baada ya hizo fedha kufika, haziendi kwa Dkt. Slaa, zinakwenda kwa Mkurugenzi wa Halmashauri na ndiye anayesimamia miradi yote. Leo Dkt. Slaa hata kwenye maji hapati chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika jambo hili, ambalo kwa kweli limekuwa na upotoshaji mkubwa na sijui sababu yake ni nini, lakini nadhani pengine kuna mgongano wa maslahi kati ya Mfuko huu na wenzetu wanaoupinga wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotoshaji wa kwanza kabisa ambao umesemwa sana katika Mfuko huu ni namna ambavyo wanaubatiza jina ambalo siyo la Sheria yenye. Wanauita Mfuko wa Wabunge au Mfuko wa Mbunge. Huu Mfuko ni wa Jimbo siyo Mfuko wa Mbunge. Mbunge kwa mujibu wa Sheria hii, anaweza akawa hayupo kwa sababu yoyote ile ama amekufa au Ubunge wake umesitishwa kwa sababu za kiuchaguzi au zozote zile na bado maamuzi yakafanyika na shughuli za Mfuko huu zikaendelea. (*Makofii*)

Kwa hiyo, huu Mfuko siyo wa Mbunge ni Mfuko wa Wananchi wa Jimbo. Wananchi wa Kibakwe wanansikia, maana yangu ni kwamba, Mfuko huu na fedha zitakazowekwa katika Mfuko huu, zitakuwa ni za Wananchi wa Jimbo la Kibakwe, siyo wangu Simbachawene kama Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe; hapana. Ndiyo maana katika upotoshaji huo, wanasema Mfuko huu hautatumika vizuri, huu ni ufisadi mwingine utatumika kwa takrima; siyo kweli. Sheria hii inasema Mfuko huu utatumika kwa Miradi ya Maendeleo. (*Makofii*)

Sasa Miradi ya Maendeleo tafsiri yake ni miradi ambayo inapangwa na inakuwa katika orodha ya taratibu za mipango ya Halmashauri. Kwa hiyo, huu ni upotoshaji mwingine ambao wanataka tu wananchi wa vijijini na wao waunge mkono mawazo yao ya hofu ya nafasi ya NGO, ambao wanakaa mijini hawaendi kule vijijini na wanaomba fedha kwa wafadhilli kwa kutumia wananchi wetu walioko vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana; kitu kizuri kama hiki, Serikali makini na Serikali nzuri kama hii ya CCM, inapoamua kupeleka fedha kwa wananchi wake, kwa maana ya dhana ya *decentralization by devolution*, tunataka kwenda zaidi. Huu Mfuko kwanza kuishia tu hapa mimi ningesema hazitoshi, twende zaidi mpaka kuwe na Mfuko hata wa Kata, Mfuko hata wa Kijiji, hayo ni maendeleo zaidi na kwamba wananchi wanakutana na fedha yao. Sasa huyu mtu anayewaambiwa wananchi kwamba waukatae wakati wanapelekewa fedha, mimi nasema wewe utakuwa ni mwananchi wa ajabu sana, hutaki fedha inayokuja kwako kuitia kwa Mbunge wako ambaye umemchagua, maana mwakilishi wa mwananchi ni Mbunge na wala siyo NGO. (*Makofi*)

Sasa huyo mwananchi utakayemwambia kwamba, Mfuko huu hatuukubali, maana yake unakataa Mfuko ambao uko chini, ambao Mwenyekiti wake ni Mbunge anayejua shida zako za kila siku; wewe utakuwa mtu wa ajabu kidogo! Naomba wananchi muwashangae sana hawa wanaokataa huu Mfuko; siyo watu wenye nia nzuri hata kidogo katika nchi yetu. Hawajui shida zilizoko kule kijijini, hawajui shida zilizoko Malolo, Idodoma, Mang'alaiza na Galigali. (*Makofi*)

Kumewahi kutokea NGO ikaenda Lufi? Hata siku moja, wakijitahidi sana wanaishia Dodoma hapa, wakijitahidi sana Mpwapwa, halafu wanapiga kona na hela walizopata kwa Wazungu zinaondoka. Fedha za UKIMWI wanazipokea nyingi zinapitia kwao, lakini mtu aliyeathirika au anayehitaji kupewa msaada wa chakula, wanampeleke na ndizi moja kwa miezi sita. Nimewahi kukutana na mtu anapelekewa ndizi moja; NGO hiyo! Sasa unasema kwamba Mfuko huu haufai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani kwa kweli huu ni upotoshaji wa hali ya juu na Watanzania wawakane hawa watu, hawana nia nzuri nao. Halafu wanajenga hoja ya ajabu sana, wanadai kwamba eti Mfuko huu unakiuka Katiba; Katiba ipi hii ya Tanzainia au ya kwao nyininge ambayo wameitengeneza wao? (*Makofi*)

Katiba hii inatambua Mamlaka kwamba, msingi mkubwa wa Utawala na Uongozi wa nchi hii na Mamlaka ya nchi hii ni Wananchi. Haya makodi tunayokusanya yote haya ambayo anayakusanya Bwana Mkulo pale, yanatakiwa kwenda kwa Wananchi na hii ndiyo njia tunayowapelekea kwamba, ilikuwa katika ngazi ya Halmashauri sasa inakwenda katika ngazi ya Jimbo. Ubaya uko wapi? Unakiuka Katiba ipi; eti *separation of powers*; hivi wanajua maana ya *separation of powers?* *Separation of powers* maana yake nini? Angalia wanasema eti umekiuka msingi wa mgawanyo wa madaraka. Sheria hii imeweka vizuri sana katika eneo hili, wewe kama Mbunge siyo *signatory*, husaini *Cheque* ya Mfuko huu; huwezi kutoa pesa Benki; umeingilia wapi shughuli za kiutendaji? Mfuko huu kwa mujibu wa Sheria hii, utakuwa chini ya Sheria zifuatazo: *Public Finance Act*, *Public Procurement Act* na *Local Government Financial Laws*. Hizi

ndizo zita-control Mfuko huu na shughuli zote za maendeleo zilizopangwa kutokana na Mfuko huu.

Hatujatunga Sheria nyingine yoyote ya kwetu inayosema, Mbunge ndiye atakayekuwa anapanga vipaumbele, Mbunge ndiye atakayekuwa anatoa fedha; Mbunge hagusi hizo fedha. Pia sehemu ya tatu, ibara ya 10, inawataja watu wanaohusika na Mfuko na Kamati ya Maamuzi juu ya fedha hizi. Kamati tu ya Maamuzi, lakini wao hawatoi fedha.

Inasema, kwanza, Mbunge atakuwa ndiye Mwenyekiti. Pili, anasema Afisa Mipango wa Wilaya, atakuwa ndiye Katibu wa Kamati hiyo. Kipengele (d) kinasema kwamba, Madiwani wawili watakuwa Wajumbe wa Mfuko huo, Madiwani wanaowawakilisha wananchi.

Kwa Tanzania Bara, WEOs wawili nao watakuwa ni Wajumbe wa Mfuko huu, *Ward Executive Officers*, hakujawahi kutokea katika historia ya nchi hii. Inasema hata wao NGO wenye nguvu sana, watakuwemo katika maamuzi haya. Sasa kama wao wanawapenda wananchi na wana nia njema na nchi hii, waje kule waunde NGO. Jimbo la Kibakwe hakuna NGO yenye nguvu. Kwa hiyo, waje huku sasa tushirikiane, tuwapelee wananchi maendeleo kwa sababu na wao msingi wao na uwepo wao ni wananchi hawa hawa. Wasipate shida kwamba, nafasi yao waliyokuwa wanajidai nayo hapo bila kuulizwa na mtu itapotea. Sisi hatuna haja na nafasi yao. Waje tushirikiane katika huu Mfuko. (*Makofit*)

Sisi hatuna haja hata ya kuomba hela zao zipitie kwenye Mfuko huu, wao waendelee lakini wakiendelea kufeli, hao wanaowapa fedha wakiona Mfuko huu umefanya vizuri, nasema ziingie kwenye Mfuko huu. Kwa hiyo, wao wajipange tu wahakikishe kwamba, wanafanya vizuri katika shughuli ambazo wanaombea fedha kutoka kwa Wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana madai mengine kwamba, eti Mfuko huu utawasababisha Wabunge waliopo waendelee kubakia madarakani; wao wanaumia nini na hilo? (*Makofit*)

Yaani kuna ubaya gani katika hili? Kuna ubaya gani au wao wanataka kuja kugombea, lakini tunawafahamu, wengi wao wanaodai hawa tena wanapambana kweli kweli, wanataka kuja kwenye Majimbo, sasa wanaona hali hii inawapa nafasi finyu kweli kweli. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si kweli, kwamba hata Kenya ambako walitumia vibaya Mfuko huu Wabunge wengi waliondoka kwa sababu ya Mfuko huu. Sisi Mfuko huu tumeuwekea Sheria nzuri kweli kweli. Mfuko huu mantiki yake kwa wananchi wetu wa chini kabisa, muuelewe kabisa, una nia nzuri. Yako mambo kule Majimboni hayawezi hata kufikiwa hata na mipango ya Halmashauri. Ziko barabara ambazo hazipo hata katika ramani za barabara za Halmashauri lakini ni muhimu kweli. Unapofika katika hali kama hiyo, ukakuta barabara kwa mfano ya kutoka Chobola kwa mfano kule

Kibakwe, Chogola kwenda Galigali haimo hata katika ramani ya Halmashauri. Kwa hiyo, kwa Sheria yetu ya Barabara, haiwezi kutengewa fedha lakini ikiwa ndiyo kipaumbele na Kamati ikaridhia, basi mnanyofoa vifedha hizi zinakwenda kusaidia pale, kuna ubaya gani? Naamini ni upotoshaji mkubwa na mimi naamini kabisa wananchi wa leo nilikuwa nasikia maoni yao asubuhi kwenye kipindi kile cha Jambo Tanzania wengi wanasema Mfuko huu wanaukubali na wengine wanadai kwamba hawajauelewa tu lakini wanaamini ni kitu kizuri kwa sababu sisi Wabunge wote humu ndani hatujawa wasaliti wao na hatutakuwa wasaliti wao hata mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kubwa kwamba wananchi watauelewa Mfuko huu, wananchi wataona matokeo ya Mfuko huu, wananchi wataufurahia Mfuko huu maana ni fedha kwa mapenzi iliyonayo zinapelekwa na Serikali yao na wao kupitia kwenye Kamati hii, kupitia kwenye Mfuko huu wa Jimbo ambao utakuwa na Kamati inayowakilishwa na Madiwani na Watendaji wa Kata na watu wa NGO lakini kazi kubwa iliyotajwa katika Sheria hii, kazi ya Kamati ile ni kukusanya mapendekezo ya miradi kutoka kwenye Kata zote na ndipo wakae na kuweza kuamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa George Simbachawene. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Jenista Mhagama ndiye anayefuata na nitamwomba Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, kwa dakika zitakazokuwa zimebakia ajipange kuzitumia hizo hata kama zitakuwa dakika 10. Mheshimiwa Mhagama.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi lakini pia nitangulize kwa kusema naanza kwa kuunga mkono hoja hii. Lakini ninaomba niunge pia mkono kwa nguvu zote hoja ya Taarifa ya Kamati na hoja kutoka kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, naziunga mkono kwa asilimia mia moja. Halafu naunga mkono hoja ya Msemaji wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge, naiunga mkono pia kwa asilimia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu waliotangulia wamesema mengi na wamejaribu kwa kiasi kikubwa sana kujibu hoja ambazo zimejengwa na watu wengi kuhusu Mfuko huu. Lakini mimi niwaombe Watanzania wafahamu kitu kimoja. Sisi Wabunge tuko humu ndani ya Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na itakuwa vigumu sana sisi Wabunge ambao tuko kwa mujibu wa Katibu kuanza kuvunja Katiba tena ndani ya Bunge sisi wenywewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata Kanuni zinazoongoza shughuli zetu za Bunge, Kanuni ya 1, inaelezea Bunge lakini Kanuni Na. 2(1), inasema hata Kanuni zetu ndani ya Bunge zitakuwa ni Kanuni ambazo haziathiri masharti yoyote yaliyomo katika Katiba ya nchi yetu ya Tanzania. Sasa iweje tena leo sisi Wabunge tukakaa humu ndani na tukaanza kukiuka Katiba wakati sisi tuko kwa mujibu wa Katiba yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaomba niseme Watanzania wafahamu kwamba wote sisi tunamwamini Mwenyezi Mungu na kama tunamwamini Mwenyezi Mungu, hatuanzi shughuli humu ndani bila Kanuni Na. 31 ya kuomba Dua, ya kuomba Bunge lifanye kazi zake kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania. Tunapofanya ile dua kila siku asubuhi tunasema ili tufanye maamuzi sahihi yenyе manufaa kwa watu wote na ustawi wa wananchi wetu wa Tanzania. Wote tunamaliza kwa kusema amina, kwamba yale tunayoyafanya humu ndani ni kwa manufaa ya ustawi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye hoja. Mfuko huu unasema kwamba ni Mfuko wa wachachu ya kuleta maendeleo katika Majimbo yetu. Ninaomba niwaambie Watanzania wote na hasa hata wale wananchi wa kawaida kabisa wanaelewa maana ya chachu ni nini, chachu inafafananishwa na hamira. Maana hamira, ukiiweka kwenye chakula inaumua chakula kiwe kikubwa zaidi na kitosheleze. Hata kama mama anapika chakula nyumbani, anafanya utaratibu wa kukifanya chakula kiwe kingi na kitosheleze halafu anaingia mtu mwingine, hii lugha nyepesi tu Mheshimiwa Mwenyekiti, anaingia mtu mwingine anahoji kwa nini unajitahidi kuhakikisha chakula kitosheleze, mtu huyo anahoji kitu cha msingi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitumie hii lugha nyepesi ili watu waielewe, kwa sababu wakati mwingine labda tunatumia lugha nzito, kuna watu wanashindwa kuelewa. Tunaposema chachu, ni suala zima la kuhakikisha tunaongeza ili angalau hiki kinachopikwa kiweze kumfikia kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba wananchi, waelewe nia njema na kama nilivyo sema tunafanya kwa kiapo na tunafanya kwa kumwamini Mwenyezi Mungu kwa manufaa ya wananchi wetu na sio kitu kingine chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini sasa naunga mkono hoja hii? Hoja hii imekaa katika misingi imara kabisa ya kutusaidia. Sasa hivi Watanzania tuanze kuwa na muundo wa kufanya maamuzi sahihi, kwa wakati unaofaa na maamuzi yenyе tija kwa wananchi wa Tanzania na si vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuendelee kuwa na utaratibu wa kuamini katika kile tunachokiamua na ndiyo maana sisi Wabunge tumeamini kwamba Mfuko huu kwa sababu unabeba zana nzima ya kuleta chachu ya maendeleo na sisi Wabunge ndiyo tuna kiu kubwa ya maendeleo ya Watanzania basi Mfuko huu utasaidia sana kuwapeleka Watanzania katika yale wanayoyataka lakini yameshindwa kufikiwa na Mifuko mingine. Tunaamini katika hilo, sasa kama tunaamini katika hilo ni lazima Watanzania watunge mkono. Ni nia njema na iliyothabiti na imani ni kuwa na uhakika na kile unachokifanya, tuna uhakika na hiki tunachokifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee, niseme mambo yafuatayo Watanzania wayafahamu. Ninasema haya kusudi tuweze kuwa pamoja. Haitusaidii katika nchi hii ambayo tumelalamika kuwa tegemezi kwa muda mrefu, tunapotafuta njia mbadala ya kutuondoa katika kuwa wategemezi, kuanza kutafuta njia za kujitegemea, halafu ionekane ni nia mbovu, Watanzania tunajipotosha wenywewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wale wanaounga mkono Mfuko huu wameelewa. Ninasema wameelewa kwa nini, kwa sababu wanataka sasa tujifunze kwa kutumia uwezo wetu wa ndani tulionao. Tumesema Mfuko huu hautafungamana na masharti yoyote ya utegemezi kutoka nje ya nchi yetu ya Tanzania. Imejengwa hoja hapa, ambayo inasambaa kwamba Mfuko huu tukiupitisha leo eti walipa kodi wataongezewa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti tumeshaipitisha hapa na tulipokuwa tunapitisha bajeti na hiki kiko ndani ya bajeti hiyo. Sasa kwa Sheria za nchi yetu tukishapitisha bajeti hata ukitaka uongeze kodi kwa mamilioni, huna nafasi. Kwa hiyo, dhana ya kusema kwamba kodi hapa inaongezwa haipo. Suala la msingi hapa tunataka kujenga uwezo wetu wa kujitegemea kupitia ndani ya nchi yetu wenyewe kwa kutoa dhana shirikishi lakini tunataka pia kuongeza mwamko wa jamii yetu kutofautisha dhana mbalimbali za utegemezi katika kufanya wanajamii kupata fursa mbadala za kujiletea maendeleo kwenye maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko unatuambia sasa tutaanza kuwatumia mafundi kwenye Majimbo kule waweze kutekeleza miradi. Nani anakataa dhana hii ya ajira kwa mafundi wale wadogo wadogo kwenye Majimbo yetu? Ana nia njema na Watanzania? Hana nia njema! Lakini Mfuko huu utaipa jamii nafasi zaidi ya kujitafiti, kujipima na kujijengea tabia ya kujiimarisha kwa njia zinazoweza kufikika kwa uharaka zaidi. Hii ni azma nydingine nzuri kabisa ya Mfuko huu. Anayepinga, hataki azma hii njema itekelezwe ndani ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kujenga tabia ya kuchochea ari na Mfuko wenyewe ni wa uchochezi, Waheshimiwa Wabunge tunesema, utachochea ari ya kuwezesha wanajamii, kubuni, kupanga mipango yao ambayo itawaletea maendeleo kwa haraka zaidi. Sasa mnataka wananchi wa Tanzania waendelee kutokuwa wabunifu na bila ubunifu kuna maendeleo kwenye Taifa lolote? Anayepinga hili, hataki maendeleo ya Watanzania katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mfuko huu utajenga mahusiano, umeona sehemu ile ya tatu, inaeleza kabisa Wajumbe watakaokuwa wanao-manage ule Mfuko. Mbona ni mahusiano, hata hizo NGO wamo tena kama Wajumbe. Sasa sijui kama na hilo wanakataa, mimi siwezi kuelewa, wamo kama Wajumbe. Kwa hiyo, ule ni mpango mwingine nzuri wa kujenga mahusiano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi. Hata hapa Bungeni kwa takriban miaka mitano sasa wenzetu haya mashirika yasiyo ya Kiserikali wanakuja kila siku hapa Bungeni kutafuta kujenga mahusiano. Sasa tunayajenga wapi, mahusiano hayo tutayajenga kwa kuwasaidia wananchi wa Tanzania na hasa wale wa vijijini ambao hawajapata kufikiwa na rasilimali zozote za kuwaletea maendeleo. Kwa hiyo, anayepinga hilo anataka nchi hii isishiriki pamoja katika dhana ya kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho, mnakumbuka siku moja katika Kikao katika Kijiji kimoja, niliulizwa

Mheshimiwa Mbunge hapa umechangia milioni tatu, Mfuko wa Jimbo unaanza lini ungetuongeza hapa tukamaliza *project* hii ya hosteli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona wananchi wanaelewa, lakini yuko mtu anaamua kutoa maelekezo ya kuwapotosha, lakini wanaelewa. Mimi hilo swaliliulizwa, utaanza lini Mfuko wa Jimbo ukusaidie hapo ulipofikia na sisi tulipofikia tumalize mradi wetu? Wanaelewa kabisa, swaliliulizwa kwenye mkutano wa hadhara na ukitaka nilete ushahidi mbele ya Bunge leko, nitauleta Mheshimiwa Mwenyekiti, kuthibitisha kwamba walioko huko wanaelewa Mfuko huu kuliko wale wanaochukua agenda hii bila utaratibu unaotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Watanzania, Mfuko huu hauna picha ya takrima, Mfuko huu hauna picha ya kumnufaisha Mbunge, tena ni mtego mzito sana kwa Mbunge ambaye hatakuwa makini anawenza kuanguka hata kabla ya muda wa miaka mitano. Ni mtego mkubwa sana Mheshimiwa Mwenyekiti na ninaomba niseme Mfuko huu ukianza hata mwakilishi wa NGO pesa yake ailette kwenye Mfuko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama. Sasa mzungumzaji wetu wa mwisho asubuhi hii ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji.

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Ninaposimama hapa mara nyingi watu hunishangaa, huanza na maneno yanasema “*Bismillah Rahman Rahim*”. Maana maneno haya ni kwamba naanza kwa jina la Mwenyezi Mungu. Sasa nataka nianze kuchangia mada hii kwa kuanza na *Bismillahi Rahman Rahim*” kubwa zaidi kuliko hata yote ambayo siku zote nimekuwa naitoa. Kwa nini nasema hivyo? Mwenyezi Mungu sasa anatufungulia neema na neema hii ninadhani ni mtihani kwetu. Niwashukuru sana wananchi wa Zanzibar na hasa wa Jimbo la Muyuni kwamba sikusikia kusema kwamba wanapinga Mfuko huu. Kwa hiyo, hii ni pongezi na ningeomba wananchi wote ambao leo wanatusikia hapa waamini na wajue kwamba wananchi wa Zanzibar kwa jumla na hasa wananchi wa Jimbo la Muyuni, tunaunga mkono kwa asilimia mia Mfuko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu kwa kweli ni ukombozi, na watu husema umechelewa kufika lakini Wazungu wanasema *better late than never*. Kuchelewa kwa kuja kwa Mfuko huu ni kwa sababu ya kusubiri kupata utaratibu na mpango mzuri na utaratibu na mpango mzuri umefika na leo tunashukuru uko mikononi mwetu. Kwa hiyo, ninawaomba sana wananchi waelewe kwamba madhumuni ya Mfuko huu ni kuja kuwakomboa. Ni neema tulioletewa na Mwenyezi Mungu baada ya kuhangaika kwa muda wote leo imetufikia na hatuna budi kuitekeleza kama itakavyokuwa inastahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu hauzingatii itikadi, hauna dini, hauna chama. Ni Mfuko ambao umekuja kwa ajili ya kuwaletea manufaa wananchi na kama tunakumbuka katika sehemu nyingi watu wanakuuliza, ukishindwa kidogo tu Mbunge

wanakuambia, Mheshimiwa Mbunge mbona tunasikia kwamba kuna pesa huko za Jimbo? Kwa hiyo, tulikuwa tunapata tabu sana ya kuwaeleza wananchi hali halisi ya Mfuko. Kwa hivyo sasa tunataka tuwaambie wananchi kwamba ile Sheria ambayo tulikuwa tunaingojea na masuala ambayo walikuwa wanatuuliza sasa yamepatiwa ufumbuzi na ufumbuzi wao ni huu wa kuleta Sheria mbele ya Bunge na sasa tutaamini wazi tutajua ni jinsi gani Mfuko tutautumia kwa manufaa ya kutuletea maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kushangaza sana kuona kwamba kuna baadhi na hasa vijana, kwa kutokuelewa maskini, kwa kutokuelewa kwao ningeshauri sana na kama ingekuwa inawezekana kuvitumia vyombo vyahabari kwa maelezo ambayo yametoka leo tokea tumeanza kuchangia Mfuko huu, irudiwe kwenye vyombo vyahabari ili wananchi wazidi kusikia na kuufahamu ni nini madhumuni hasa ya Mfuko huu. Kwa hiyo, nawashauri sana wale Waandishi wa Habari amba kwa wakati mwingine walikuwa wanachangia kuwaongezea maneno ambayo yalikuwa si sahihi haya maneno ambayo yanatoka leo hapa mbele ya Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Mwenyekiti ndiyo maneno sahihi yanayohusiana na Mfuko huu wa kuchochea maendeleo ya Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile muda uliokuwepo ni mdogo na mimi sikutaka kuzungumza mengi isipokuwa kuwathibitishieni tu mbele ya Bunge hili Tukufu, wananchi wa Jimbo la Muyuni na ninaamini kwa wananchi wote wa Zanzibar tumefarijika kwa kuletewa Mfuko na ninaamini tutautekeleza vizuri sana kwa kadri ya ulivyokuja. Nataka nisiwe na mengi Mheshimiwa Mwenyekiti. Nashukuru kwa kunipa muda huu na natamka rasmi kwamba tunaunga mkono kwa asilimia mia. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji. Kwa vile nina dakika 10 naamini Mheshimiwa Ponsiano Nyami anaweza akazitumia dakika hizi. Yeye ni Mbunge mzoefu, Mheshimiwa Nyami.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimejitu umeniambia jioni. Sasa looh! Nianze kwa kukushukuru na kuanza kuunga mkono Muswada huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Serikali ambayo kwa nyakati tofauti iliweza kufanya kazi nzuri sana ya kufanya mchakato wa Muswada huu. Katika miaka ya 1997/1998 ndipo mawazo kwa Wabunge yalipoanzia kufikiria jambo hili lakini katika nchi nyingine walikwenda haraka zaidi. Kwa mfano, nchi iliyoanzisha katika maeneo haya ya Kusini, ni Kenya mwaka 2003 wao iliweza kutunga Sheria hiyo. Waliofuatia ni Uganda mwaka 2005. Lakini pia kuna nchi nyingine kama vile Malawi, Zimbabwe, Zambia nazo zina Mfuko huu na kwa Tanzania sio kwamba tumekurupuka, hatujakurupuka kwa sababu kwanza mwaka 2003 Kamati ya Bunge iliweza kuundwa kujaribu kutazama jambo hili na wakajaribu kuzunguka katika baadhi ya nchi wakaona kwamba inawezekana. Halafu mwaka 2006 Kamati ya Ushauri iliweza kuundwa na

ikazungukia katika nchi mbalimbali Kenya, Zambia, India na Uganda kujaribu kutazama, je, mambo yakoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndipo Kamati ya Wataalam, April, mwaka 2007, hii ni ya Serikali, iliweza kuundwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ikiwemo TAMISEMI, ikiwepo Wizara ya Fedha na wakati huo Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji nao pia waliweza kuingia kwenye Kamati hiyo. Lakini mimi mwenyewe hapa nilijaribu kufanya utafiti kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka huu nilijaribu kutembelea Majimbo kadhaa katika nchi, kwa mfano Malawi, nilitembelea Jimbo la Mzimba Solola na Mzimba West, Chitipa Wenya, Mzuzu City halafu Nkatta Bay. Zimbabwe nilitembelea Jimbo la Siolo halafu na Madze. Zambia nilitembelea Kasama, Bweengwa, halafu Mpulungu, Mbala na Mambwe na Kenya vile vile niliweza kutembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda nitaje yale ambayo wenzetu kule wamefanya. Kwa mfano, Malawi wao kila Jimbo walikuwa wanapewa Malawi Kwacha milioni tano lakini kutokana na uchumi ulivyoenda mwaka huu mwezi wa tano nilikuwa huko na wa sita wao wametenga shilingi milioni tatu kwa kila Jimbo kule Malawi. Milioni tatu ni pesa nyingi sana. Wakati ambapo kwa upande wa Zambia wao wametenga Kwacha 240 milioni kwa kila Jimbo. Huko ni Zambia kwa kila mwaka. Lakini kwa upande wa Uganda wao walitenga shilingi bilioni tatu kwa Majimbo yote, lakini wa kila Jimbo kwa mfano mwaka huu, Mbunge amepewa shilingi milioni 10 zile za Uganda, tofauti yao ni kwamba wao wanaweka moja kwa moja kwenye *account* ya Mfuko wa Mbunge binafsi, tofauti ya Uganda na nchi zingine zile. Lakini upande wa Kenya, wanaharakati wale wanaojiita wanaharakati walipokuja hapa walipotosha wakasema Kenya Mfuko huu umefutwa. Haujafutwa, bado Mfuko huu upo na kwa nyuma walikuwa wanapewa Kenya shilingi kwa kila Jimbo 60 milioni sawa na dola 750. Lakini kwa sababu Mfuko ule umefanya vizuri, mwaka huu kila Jimbo la Kenya limepewa Kenyan shillings milioni 183 sawa na dola milioni 2.3. Sasa wale wote wanaopita kupotosha kwamba Mfuko huu tunapouanzisha Tanzania ni mbaya ni wakorofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini waelewe kwamba Ma-RC tumekuwa tukiwapa takribani shilingi milioni 20 kwenye bajeti hii ambazo wao wanapotembelea vijihi na maeneo mbalimbali wanaposema nitachangia kiwango fulani pesa ile haitoki mfukoni mwake, ni pesa ambayo tumekuwa tukiwapa hapa. Mwaka huu tumeongeza kutegemea na Mkoa pesa zimetolewa kati ya shilingi 45 hadi milioni 50 kule Mikoani kwa maana kwamba hata ma-DC kwa mara ya kwanza tumeanza mwaka huu wao pia watapewa kutokana na pesa hii ili wanapokwenda vijijini nao pia wanaweza wakachangia. Kwa hiyo, wale wanaobeza kwamba Mfuko wetu huu tunapouanzisha, ni Mfuko ambao haufai, si kweli. Ni Mfuko ambao ni wa wananchi kabisa na wananchi wanapaswa kuufurahia Mfuko huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nitoe angalizo moja, kuna Halmashauri nyingine zina Majimbo zaidi ya mawili, matatu na kadhalika. Pale tunaposema Katibu atakuwa ni Afisa Mipango wa Wilaya peke yake, pengine anaweza akapata kazi kubwa sana. Kwa hiyo, eneo hilo mimi napendekeza kwamba kuwepo na nyongeza ile ambayo

ya kwamba Afisa mwingine anaweza akateuliwa na Mkurugenzi lakini kwa ridhaa ya Mwenyekiti wa Kamati ile ili kusudi baadhi ya Majimbo mengine ambayo yapo mengi kwenye Halmashauri yawefe kuwa na Katibu wao katika utendaji wao wa kazi. Nadhani hii itaweza kidogo kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika mgawanyo wa pesa kwamba kutakuwa na asilimia ishirini na tano kwa kila Jimbo la Tanzania na ile asilimia 75 inayobakia itagawanywa kwa vigezo ambavyo Mheshimiwa Waziri alisema, 45 kutegemea na idadi ya watu, 20 kiwango cha umaskini uliyopo katika Jimbo na asilimia 10 ya mwisho ukubwa wa Jimbo. Napendekeza katika ukubwa wa Jimbo badala ya asilimia 10 iwe ni asilimia 15 na kwa ujumla wananchi naomba watuelewe sisi Wabunge kwamba tunapopita katika maeneo yao kuna miradi ambayo haifikiwi na Halmashauri yenye wala Serikali Kuu. Tumekuwa tukiombwa kuchangia fedha ile tunayochangia Mbunge, Diwani anachangia, ni pesa inayotoka mfukoni mwake kama walivyoeleza hapa, mara nyingi imekuwa haitoshelezi. Kwa wale ambao wana kipato kikubwa au ana biashara kwa kutoa pesa mfukoni inaweza kuwa ni chanzo cha kuchochea rushwa zaidi lakini kwa maana ya Mfuko huu ni Mfuko ambao unaeleweka. Miradi inabuniwa na wao wenye, inapitishwa na vikao maalum kama vile *ODC* kwamba ndiyo vipaumbele vyao na vinatoka moja kwa moja kwenye Mfuko huu kwa kutumia hundi. Sasa tatizo liko wapi? Pesa hii haiwekwi kwenye Mfuko wa Mbunge na wala Mbunge hatashika hata hiyo senti tano yako bali pesa hizi zitakwenda moja kwa moja katika mradi unaolengwa kwa kupeleka hiyo cheki. Mradi ule unasimamiwa na wananchi wenye, tatizo liko wapi? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono na nawaomba Wabunge wote mkaelimishe Majimboni. Ahsanteni sana. (*Makofit*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawashukruni sana kwa michango ambayo bado inaendelea. Niseme tu kwamba jambo hili tutaendelea nalo jioni na wachangiaji jioni ya leo watakuwa wanne, niwataje tu wote, atakuwa ni Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella. Baada ya hapo, taratibu zingine zitaendelea jioni ya leo.

Tangazo ni moja kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma kwa Wabunge, Mama Kippa, anaomba niwajulisheni Wabunge wote kwamba Chuo Kikuu cha Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi inayoitwa *TAS Tanzania Albino Society* wameleta DVD inayohusu mauaji ya albino. Hivyo Wabunge wote wapitie mapokezi pale jengo la utawala ili mjipatite DVD hiyo.

Baada ya tangazo hilo, naomba nisitishe sasa shughuli za Bunge hadi saa 11 leo jioni.

(*Saa 6.58 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni*)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati Mwenyekiti anasitisha shughuli za Bunge hadi jioni hii, nimearifiwa kwamba walibakia wachangiaji wanenye, ambao ni Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Dokta Getrude Mongella na mimi ninaongeza mmoja, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, yeze ndio atahitimisha. Kwa hiyo, naanza na Mheshimiwa Godfrey Zambi, ajiandae Mheshimiwa Beatrice Shelukindo. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, niwe mchangiaji wa kwanza jioni ya leo kuhusu Muswada ambao uko mbele yetu wa *CDCF*.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii, kama walivyoanza wenzangu kwa kweli, niipongeze sana Serikali na hususan Mheshimiwa Rais, kwa kukubali Muswada huu kwanza uendelee kutayarishwa na pili uje ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina hakika kabisa Mheshimiwa Rais, anajua umuhimu wa Mfuko huu. Yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais, amewahi kuwa Mbunge, kwa hiyo, anajua matatizo au adha ambazo Wabunge wanakumbana nazo wanapokuwa kenyetumaini. Kwa hatua hiyo, kwa kweli, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, pamoa na Serikali yake yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nikushukuru sana wewe mwenyewe na Kamati yako yote ya Uongozi, kwa kuona umuhimu wa kuendelea kuzungumza na Serikali bila kukata tamaa kuhusu Mfuko huu kuja ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Mabalozi. Huko nyuma tulitaka kukata tamaa hasa baada ya kuambiwa kwamba Mabalozi hawaoni umuhimu wa Mfuko huu. Lakini kwa sababu ya jitihada zako, kama nilivyosema na Kamati yako ya Uongozi, mmeendelea kuzungumza na Mabalozi na hatimaye na wenye wameona umuhimu wa Mfuko huu kwa Wabunge wa Tanzania, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatukukurupuka au Bunge halikukurupuka kuanza jitihada za kuanzisha Mfuko huu. Kama walivyoza wenzangu, jitihada zilifanyika kujua wenzetu katika Mabunge mengine wanafanya nini, ndipo Mfuko huu ulipofikia hatua hii. Bunge lilifanya kazi kubwa na Bunge likaunda Kamati, kama tunavyojua imetembelea nchi mbalimbali na Bunge likajiridhisha kwamba kuanzishwa kwa Mfuko huu, kuna faida kubwa sana. Nasema hivyo kwa sababu ukiangalia maudhui ya Muswada wenye, hupati shida ya kuhofia kwamba pesa zikienda kwa wananchi zitatumwi vibaya.

Mheshimiwa Spika, wanaharakati, ni kweli walikaribishwa, wakaja kutoa mawazo yao lakini ambacho mimi nilishangaa, badala ya wenzetu kuja tujadili Muswada, wao wamekuja na ajenda ya kuukataa Muswada. Sasa huwezi ukakaribishwa kwenye *public hearing* badala ya kuupitia Muswada, wewe unaukataa Muswada, kwa vyovyote vile ni lazima uone kwamba huyu mtu hakuja na nia nzuri, hawakuja na nia nzuri. Ndio pale tuliposema, nadhani hawakusoma Muswada, lakini nia yao kubwa ilikuwa ni kukataa Muswada na wengine hata wakasema wao ndio wawakilishi wa wananchi. Wengine tukawa tunashangaa, hiyo *mandate* ya kuwawakilisha wananchi wao wameipata wapi? Maana wawakilishi wa wananchi ndio sisi; sisi ndio tumechaguliwa na wananchi, ndio tunajua shida za wananchi, wenzetu wakawa wanajipa madaraka ya kwamba wao ndio wawakilishi wa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nikawa ninawashangaa, ni Watanzania gani hawa ambao wanakataa pesa kupidia Halmashauri, ziende kwenye Majimbo kutatua matatizo ya wananchi? Watanzania ambao hawawatakii Watanzania wenzao maendeleo! Ni lazima wawe watu wa ajabu sana. Mimi ninaomba wanapokwenda kwa Watanzania kufanya kampeni zao, Watanzania wawapuuze, kwa sababu pesa hizi zinaenda kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Muswada upo *clear* na mimi kwanza ninaishukuru sana Kambi ya Upinzani, ninaishukuru sana Serikali kwa sababu wameainisha hatua ambazo zitafuatwa mpaka pesa ziende kwenye maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kule Mbozi, nina miradi ambayo Serikali kama Serikali imeshindwa kuitekeleza, ni miradi midogo midogo kwa kweli. Kuna mahali unaenda kutoka kijiji kimoja kwenda kingine, pengine unahitaji tu kununua karavati mbili tatu, unaenda kwenye Halmashauri, wanakwambia hii barabara ni ya kijiji na sio ya Halmashauri; kwa hiyo, wanakuomba Mbunge usaidie pale na kwa kweli wananchi wanaonisikia, Watanzania wote na wale wa kule Mbozi, kwenye Kata na vijiji vyake mbalimbali, wanajua maeneo ambayo wamemuomba Mbunge wao kwamba, tunaomba utusaidie hapa tutengeneze karavati, lakini Mbunge wao wakati mwengine nguvu imepelea, nguvu haikutosha pengine tumeziomba Halmashauri tukasaidiana, lakini wakati mwengine Halmashauri zinakosa uwezo. Sasa Mfuko huu kama tunavyojua, hauwi mbadala wa shughuli za Serikali kama mlivyo sema, unakwenda kuchochea shughuli za maendeleo za wananchi, pale ambapo nguvu za wananchi zimeishia, ndipo Mfuko huu sasa ufanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe mfano. Nina bajeti ya Serikali ya Kenya na kwa ridhaa yako ukitaka ninaweza nikakupa nakala; bajeti kuu ya Serikali ambayo iliwasilishwa tarehe 11 June. Wenzetu wa Kenya, wameenda mbali zaidi na mimi ninaomba niseme hapa, wanaharakati walipokaribishwa walisema kwamba Mfuko huu umetumika vibaya Kenya na ndio sababu wenzetu wa Kenya wameamua kuusimamisha. Sasa mimi nikawashangaa wale wanaharakati waliokuja, hata hawajui mambo yanavyokwenda katika dunia ya leo, hawajui. Kwa sababu kwa kupidia bajeti ya Serikali ya Kenya, ambayo ilisomwa na Mheshimiwa Uhuru Kenyatta, Waziri wa Fedha na Naibu Waziri Mkuu wa Kenya; kwa ruhusa yako, kwa sababu imeandikwa kwa Kingereza lakini univumilie, ninaomba tu nisome kipengele kimoja. Kwa ruhusa yako, kinasema hivi:-

“We have achieved tremendous progress in taking development to the people through CDF, wao wanaita CDF, to scaleup the good work and ensures wananchi to continue to benefit from this fund, I have, this year, allocated Kenyan shillings 12 billion. With this amount, each Constituent will now receive on average of Kenyan Shillings 60 million,” milioni 60 za Kenya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hizi ukizi-convert kwa hela za Tanzania, ni shilingi bilioni moja na milioni 200. Lakini Mheshimiwa Waziri, anaendelea:-

“In addition, as I said earlier, I will be proposing amendments to The Roads Maintenance Levy Act and Kenya Roads Board Act, to allow for 22% of the road maintainance fund to be used for the maintanance of the Constituents roads.”

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanataka wababilishe sheria waruhusu pesa zinazokwenda Wilayani, 22%, zitumike kwa ajili ya kutengeneza barabara katika majimbo ya nchi hii. Anasema:-

“I have also propose the aproprate ammendments to allow this amount totaling Kenyan shillings four billion, to be channeled directly to the Constituents through the Constituents Fund Board. With this ammendments, I have increased significantly resources channeled through CDF for development and road maintainance from Kenyan shillings 10 billion in year 2008/2009 to about Kenyan shillings 18 billion on an average of Kenyan shillings 86 million per Constituent.” (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanazipandisha tena zaidi kutoka zile shilingi milioni 60 kwenda shilingi za Kenya milioni 86 na sasa ukipiga hesabu maana yake Majimbo hayo yatakuwa yanapewa shilingi bilioni moja na milioni 700 za Kenya. Hii ni hotuba ya Kenya na ni hotuba halali kabisa. Lakini nimalize, anasema:-

“I expect these Boards and historical measures will go a long way to measurable improve the conditions of our roads, promote commerce and consequently improve the welfare of our people”. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiendelea, kama nilivyo sema nitakukabidhi; hapa mbele anaendelea kwamba wanataka waendelee kuchukua hatua zaidi za kuuimarisha Mfuko huu ili maendeleo yafike zaidi kwa wananchi. Wanataka ikiwezekana wafike mpaka Kenyan shillings milioni 105 kwa miaka inayokuja. Hizi zitakuwa karibu shilingi bilioni mbili za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wenzetu hawa wanaharakati wanasema Wakenya wamesimamisha pesa zinazokwenda kwa wananchi na wao wenzetu wanasema hii ndio njia pekee ambayo pesa zinaweza zikaenda kwa wananchi, ndio njia pekee na sahihi. Sisi hatusemi kwamba huu utakuwa mbadala na tufanye kama wenzetu wa Kenya, lakini hapa ndipo tunapoanzia.

Mheshimiwa Spika, kama sheria inavyosema, Mbunge yeote atakayejihusisha na vitendo vya kula pesa hii, hatua ipo, kali kabisa, tumesomewa na kwa Muswada ni karibu shilingi milioni 15. Mbunge gani atakuwa hataki kazi yake aende kula hela hizi? Hela zenyewe karibu shilingi milioni tano pengine sita, saba kwa mwezi. Kama tulivyosema, wananchi na wanaharakati tunaomba watuelewe kwamba Serikali ina nia nzuri na mimi nina hakika kama Serikali ingeona hili sio jambo jema, kwa kweli wasingekubali, wangekataa hata hoja hii isingekuja hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ninaomba niseme kwamba, kama nilivyosema wenzetu wa Kenya wana mfano huo, lakini ukienda kwa nchi ya Wazambia amba wao na ninajua kupitia kwenye vyombo vya habari wenzetu wa Zambia, unapoenda kwenye uchaguzi usipozungumzia utapata vipi hela kwa ajili ya maendeleo ya Jimbo, na hasa hela zile za *CDF* zinazokwenda kwenye Halmashauri, huwezi kupata Ubunge au hata kwenye ngazi ya Urais, huwezi. Sasa na wananchi kama nilivyosema, wanafurahia sana pesa ambazo zinapita kwa Wabunge, kwa sababu wanaona ukweli Mbunge, ndio kimbilio pekee, hakuna mtu mwingine ambaye wanaweza wakamfuata kwa urahisi kwa ajili ya zoezi hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme kwamba hawa wanaharakati unaweza pia na wenyewe ukawa-*doubt* au ukawashangaa! Baadhi ya hizi *NGO* na hizi *forum* na zenyewe zimekuwa zinapewa pesa na pesa hizo wanazitumia vibaya. Wengi wao sio waaminifu hata kwenye pesa ambazo wanapewa au zinazopitia kwao kwenda kwa wananchi. Wanatumia umasikini wa wananchi ili waweze kujinufaisha wao wenyewe. Hawana Katiba zozote zinazowalinda, hakuna mtu yeote anayewakagua, lakini hizi pesa za Waheshimiwa, ambazo zinapita kwa ajili ya kwenda kuchochea maendeleo Majimboni, wanaona aah, Waheshimiwa Wabunge watakuwa wanavunja Katiba, Katiba inavunjwa wapi? Hakuna mahali popote ambapo Katiba inavunjwa, tumesema pesa hizi wasimamizi watakuwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, ndio wasimamizi. Wasimamizi kwenye pesa zenyewe kwa maana ya Mhasibu, atakuwa ni *District Treasury*, Mhasibu wa Wilaya, huyu Mbunge, pesa anaziona kwenye makaratsi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninadhani jinsi Muswada huu ulivytengenezwa, unatupa nafasi nzuri zaidi ya kuusimamia Mfuko, lakini pia na kuwawajibisha watumishi wa Halmashauri amba wanaaweza wakautumia vibaya Mfuko huu. Kwa hiyo, tayari Muswada wenyewe sisi umetupa nafasi nzuri sana ya kuusimamia Mfuko wenyewe kinyume na wenzetu wanavyodhani. Ninadhani kwa sababu tayari Serikali imeshakubali na kama tunaweza tukaanza watu wakaona matokeo yake, mimi ninadhani watakuja kusema tulikuwa wapi? Mimi nadhani tumechelewa, tunganeza mapema zaidi, kwa sababu manufaa yake yataonekana mapema na ninaamini hata matatizo madogo madogo ya wananchi yatakuwa hayapo.

Mheshimiwa Spika, mimi, wananchi wa Mbozi wananielewa na ninajua Wabunge wenzangu, wananchi wanawaelewa, kwamba wako kwa ajili yao na wangependa kwa kweli, matatizo madogo madogo yale ya wananchi yaishe. Hakuna Mbunge, ambaye angependa aongoze Jimbo maskini wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunawaomba wenzetu wanaharakati waelewe nia nzuri ya Serikali na wasiende kufanya kampeni kwa wananchi. Unajua unapoenda kufanya kampeni, maana yake una nia yako, hata sijui wanakoeleka! Unaenda kumshawishi mwananchi unasema eti uukatae Mfuko wa Jimbo! Kama nilivyosema awali, hivi unamshawishi mwananchi, usikubali wewe uletewe maendeleo, wewe una njaa nyumbani kwako, mtu anataka kukuletea chakula unasema sitaki chakula! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono Muswada huu kwa 100%. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu, najua ni wengi walitaka kuchangia. Nitachangia kwa kifupi sana, lengo langu kubwa na mimi ni-*register* kwamba ninaunga mkono suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitoe pongezi sana kwa Serikali, kwa sababu moja kubwa. Utakumbuka mwaka 2007, ultuteuwa chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Ndugai; Mheshimiwa Mkono, Mheshimiwa Slaa, Mheshimiwa Mwakyembe, Mheshimiwa Janguo na mimi mwenyewe, pamoja na kuangalia masuala mengine mengi, mojawapo ambalo tulienda kuliangalia ni hili la wenzetu wanaita *CDF*, kwa hiyo, mimi naelewa fika na yale mapendekezo tuliyokuja nayo kwa kweli, kimsingi dhana ilikuwa ni ile ile. Ila niseme tu, ninaishukuru sana Serikali, imeyaangalia upya na baada ya Kamati nyingi na vikao vingi vipyta, tumeweza angalau sasa kuja na kitu ambacho kinafanana na hapa Tanzania. Kwa kweli mimi ninaunga mkono na ninapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu vitu vichache, unajua jambo geni mara nyingi ni gumu, wengine wameshasema. Wakati tunasema kwamba *White Paper* inapitishwa kwa ajili ya Vyama Vingi, wengi walikataa, lakini sasa hivi tunaona manufaa kwamba tumethubutu, vyama vingi viro na tunakwenda pamoja na wote tunakwenda kwa maslahi ya Mtanzania na kwa kiasi kikubwa, ingawaje sisi ni chama imara sana, lakini na wenyewe wanajitahidi pale ambapo wanaona pengine labda tumepruka, kuweka msimamo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili jambo ni geni, tutarajie ambayo yametokea na yatatokea mengine zaidi mpaka pale itakapoeleweka. Elimu wakati kama huu hata ukiitoa mara nyingi wengine ni mpaka waone vitendo, tena vitendo vyenye manufaa. Kwa hiyo, mimi ninadhani tumechukua hatua nzuri kama wasemaji na wawakilishi wa wananchi kuweza kuupitisha Muswada huu lakini vilevile baada ya hapo ninadhani katika utekelezaji wengi wataunga mkono jitihada hii kubwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitake kusema kwamba mchango huu kwa kweli kuna wengi wameupongeza na wapo wengine ambao wameukataa, lakini niseme moja, tofauti na Wabunge wengine wengi, mimi ninawapongeza sana hawa wanaharakati. Kazi waliyoifanya ndio kazi ya wanaharakati, wao huwa wanakuwa kama vichocheo, wanawenza wakazungumza vitu kwa kupinga lakini ukiangalia sana nia yao aidha huwa ni

kupata uelewa sahihi au kutoa tahadhari pale ambapo jambo linaweza likatokea. Kwa hili, kwa kweli ninawapongeza, wameweza kusema waliyoyasema, wana haki ya kuyasema lakini nilikuwa ninajiuliza, pamoja na nia njema ya waliyoyasema, walipokuwa wanazungumza kuna mengine ulikuwa unayaangalia unajiuliza, hii ni ajenda yao kweli? Haya ni mawazo yao? Maana wanayazungumza kwa nguvu sana na kwa umahiri mkubwa. Sasa unajiuliza kweli ni ya kwao?

Mheshimiwa Spika, vile vile jana asubuhi, nilipata bahati ya kuondoka kwenda Nairobi kutoa *paper* mahali fulani kwenye mkutano mmoja na kurudi jioni. Nilipofika *Airport* ya Nairobi, nashuka, naona kijana mmoja ambaye alikuwa na wale wanaharakati, nikamwambia, *Hallow, how are you? Are you Kenyan?* Akasema ndio, nikamwambia *I thought I saw you in Dodoma?* Akasema ndio, tulikuja kuunga mkono wenzetu. Jaman! Ya kwetu mpaka Nairobi? Wao walipokuwa wanaanzisha *CDF* yao, walikuja kuwachukueni nyie wanaharakati wa Tanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ni lazima tuijilize, wanaendelea na *CDF*, wanaendelea na mambo yao mambo yanaenda, lakini unashangaa sisi tunaenda kuwachukua mpaka wao waje tupinge maendeleo yetu kwa ajili ya wananchi wetu. Kwa kweli mimi hii nadhani sio jambo jema, tuangalie pia yale maslahi yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile Tanzania tuna mambo mengi ambapo hawa wanaharakati wenzangu wangeweza kutusaidia mbali na hii *CDCF*. Sasa mimi naomba pia waweke hiyo nguvu waliyonayo kwenye hayo masuala mengine ambayo ni ya mwananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile niseme kwamba kimsingi kabisa tulipoenda Lusaka kama miezi miwili iliyopita, nakumbuka nilienda na Mheshimiwa Owenya, Mheshimiwa Sanya na Mheshimiwa Chana, tulienda pale tukaoneshwa mafanikio ya *CDF*, Lusaka. Walianza na milioni 40 kwa fedha zao, mwaka huu wana milioni 600; kwa jinsi mafanikio yalivyo na tukapata fursa ya kuwahoji wananchi na wananchi walikuwa wanasema kwa kweli hiki kitu kimeletwa tunashukuru, kimetukomboa sana. Sasa mimi ninaomba Tanzania tusiwe waoga, tunaanza na kiwango kidogo lakini ninadhani kwa jinsi ambavyo tunaendelea kitaendelea kuwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile niseme kwamba ninamshukuru sana Mheshimiwa Shally Raymond. Unapowatuma wajumbe kwenye mikutano mbalimbali kwa kweli tunapata manufaa mbalimbali, yeye anapata *news letters* za kila mwezi kutoka katika Shirika moja, *African Parliamentary Poverty Reduction Network*. Hapa limeonesha uchambuzi wote wa hizi fedha, *CDF* na miradi ambayo imefanyika katika nchi mbalimbali za Afrika. Sasa mimi nilikuwa ninasema, wenzetu wanaharakati ni vema kabisa mkafanya kazi pamoja na sisi, twende pamoja kwa maslahi ya Mtanzania, bila kuangalia kwamba ni mama Shellukindo atafaidika au ni nani atafaidika, tuangalie maslahi. Kwa sababu ukichukua *document* kama hii, ungekuwa umekuja umeuliza, pengine ungepata vitu kama hivi ambapo vinakupa utafiti wa maeneo mengine. Kwa hiyo, mimi ninasema ni vema kabisa hawa wenzetu pamoja na kwamba wanafanya kazi nzuri; ni lazima niseme ni kazi nzuri ambayo wanaifanya, wanapoteza muda wao na

wengi ni vijana ambao wana uelewa. Ninadhani sasa ni vizuri mkageuza mtizamo wenu mkawa mnafanya *research*, mnakuja kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho. Katika kipengele cha 9, linazungumziwa suala la ukagazi wa fedha hizi. Kwa kweli wengi walikuwa wanahoji hizi fedha zitatumika vibaya na nini, lakini hapa tunaambiwa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu, ndio ambayo itashughulika katika kipengele hicho cha 9 cha Muswada. Hapa ndio ninahitimisha kwa kusema, dhana ya hawa wanaharakati na wadau wengine, ni kweli fedha za Mtanzania lazima zidhibitiwe. Tumeshuhudia wakati mwingine kunakuwa na matumizi sehemu mbalimbali ambayo sio sahihi, lakini hili hapa wanachokisema ni sahihi na bahati nzuri Serikali imekwishaona na ndio maana wakasema ukagazi utafanyika, kama yalivyo mahesabu mengine na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mimi niombe ili twende vizuri na kama wana nia njema na kutaka ukagazi, tukubaliane kuanzia sasa na mahesabu yote ya *NGOs* zote yakaguliwe na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu. Tukifika hapo tutakuwa tunaongea sauti moja, kwa sababu isiwe wakati Serikali na sisi Wabunge wawakilishi tunataka kufanya matumizi tunakuwa tunahojiwa, kuna mengi ambayo pia yako huko, magumu na yanatisha. Mengine siwezi kuyazungumzia mahali kama hapa yanaweza yakaleta hali ya utisho, lakini ninachosema ni kwamba ni vema sasa kama kweli wana nia madhubuti basi wakae chini, wapange na wao mahesabu yao sasa yaanze kukaguliwa yaletwe ndani ya nyumba hii tuyatizame. Tuone sasa ni nani ambaye kwa kweli ana matatizo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesema na mimi nimetaka ku-*register* kwamba ninaunga mkono hoja hii, ninaomba niishie hapo. Nilitaka kusemea na vyombo vyta nje vya Kimataifa vinavyojaribu kuingilia kati, lakini naona wapo wenye sauti zao za kusema hilo labda watapata fursa. Mimi niishie hapo nikisema naunga mkono hoja. Ndugu zangu Watanzania ni jambo geni lipokeeni, manufaa yake yakishaanza mtatuambia tuongeze kiwango. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niseme machache juu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kuishukuru sana Serikali na wewe pia, pamoa na Kamati uliyoichagua kufanya kazi hii nzuri sana na kutuletea leo tuje kujadili hapa Bungeni kuhusu Mfuko huu. Ninadhani ingekuwa ni suala ambalo linahusu Bunge hili, nadhani tusingechangia tena kwa sababu imeelewka na imekubalika. Kuanzia mchangiaji wa kwanza leo asubuhi, Mheshimiwa Job Ndugai na Dokta Slaa, walipohojiwa leo asubuhi nadhani wametoa ufanuzi mzuri sana na hata watu waliokuwa wakiwasikiliza nadhani wamekubaliana na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu machache. Bunge hili ndilo Bunge la kwanza kutumia Mfuko huu, ni sisi ndio tumeanzisha. Ningombaa tufanye vizuri wananchi waone kwamba Mfuko huu ni wa kuwasaidia wananchi. Kwa sababu ni sisi ndio tutaonesha kwamba Mfuko huu unafanya kazi nzuri kwa wananchi au sisi ndio tutaharibu. Kwa hiyo, ninadhani kwa utaratibu huu uliowekwa na jinsi muundo ulivyo,

kwa kweli ninadhani Mfuko huu utatumika vizuri kwa miradi ya wananchi. Ninafurahi kabisa kwamba Mbunge mwenyewe sio *signatory*, kuna Kamati ya kuangalia hizi fedha, kuna Kamati ya kupanga miradi, kwa hiyo, Mbunge hana sehemu yoyote ya kuweza kutumia hizi fedha au kufoji, ni kusimamia tu kama wanavyosimamia miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, hata nikitoa mfano tu, fedha za Halmashauri, kuna Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye ndiye anayeweka saini kwa fedha zote zinazotumika, hivi ni kwa nini tusimhofu huyo lakini Mbunge anakuja kuhofiya kwa fedha kidogo sana, sijui milioni ngapi? Wala bado hatujui ni milioni ngapi tutapata katika kila Jimbo. Kwa hiyo, ninafurahi sana kwa utaratibu huu na huu Mfuko, hawa wajumbe waliowekwa, ni wajumbe wanaofahamika kwenye Kata, sio wajumbe waliotoka maeneo mengine ni wajumbe kutoka Jimbo hilo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu limeanza ukame muda mrefu, kuna miradi iliyosimama kwa muda mrefu. Wananchi wakawa wananiuliza, hivi ule Mfuko wa Mbunge bado haujaanza tumalizie kazi hii? Kwa hiyo, wao wameanza mapema kuutaka huu Mfuko, ni tofauti na watu wengine ambao bado wanahoji.

Mheshimiwa Spika, mimi niko mpakani, ninapakana na Wabunge watatu wa Kenya, kwa hiyo, ninaufahamu Mfuko huu wanavyoutumia. Kila Kata huko Kenya, wanachagua mradi ambao ni fedha za Mbunge, wao wanaita fedha za Mbunge, kwamba mwaka huu fedha za Mbunge, sisi tumechagua mradi huu. Mbunge akishatoka bBungeni anapita kila mahali katika maeneo yake na kuona miradi ambayo wananchi wameichagua na baadaye fedha zinapotoka zinapelekwa katika miradi iliyochaguliwa na wananchi. Hata hizi, sio Mbunge tu anakwenda kukaa na kusema ziende sehemu fulani ziende sehemu fulani, ni Kamati. Kwa hiyo, ninadhani baada ya muda, hizi fedha za kwanza tu zikienda, wananchi wataridhika wataona kwamba huu Mfuko una manufaa. Mimi wasiwasi wangu ninaouona tu, ni fedha kuwa chache kulingana na miradi watakayoibua wananchi katika maeneo yetu, ni uchache tu wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika Majimbo yetu, kwa sababu ni sisi ndio tunatoa fedha ku-*support* miradi kutoka mifukoni mwetu, tunatofautiana kutokana na uwezo wa sisi wenyewe. Kuna wengine ambao ni wazito kidogo, anaweza akaenda akachangia milioni tano katika mradi mmoja na wengine akichangia laki tano, amejitahidi, nadhani kila Mbunge sasa atakuwa ana uwezo wa kusema huu mradi tutaweza fedha kadha. Kwa hiyo, hata wale ambao hawana uwezo, nao wataweza ku-*support* miradi ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba tu jambo moja, fedha hizi zinapotoka, zitoke kwa wakati mmoja, ili zinapofanya kazi kwenye Jimbo lile, hata na Jimbo lingine zifanye kazi kwa wakati mmoja kwa sababu zikichelewa kwa Jimbo moja, wananchi wata-*query* kwamba mbona sisi hatupati hizo fedha isiwe kama hizi fedha za wenzangu wanasesma JK lakini niseme isiwe kama hizi fedha za mikopo ambazo mpaka sasa wengine wamechukua awamu ya kwanza na ya pili wengine bado hawajapata. Fedha za Mfuko huu zikifanya hivyo, itakuwa tunaharibu kabisa kwa sababu wananchi wengine wataona faida ya Mfuko huu na wengine hawataona faida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, wenzangu wamechangia Muswada huu vizuri sana na mimi niseme tu naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi mwanzoni sikutaka kuzungumza lakini nikapata ushuhuda wa kuzungumza kutokana na kilichotokea leo Bungeni. Huko nje watu wamekuwa wakifikiria kwamba Wabunge tulioko humu tunapingana katika mambo ya msingi ya Taifa letu, leo imeonekana wazi, sisi wote ni Watanzania inapofika kwenye mambo ya msingi hakuna CHADEMA, CCM, CUF, hakuna chama chochote, ndicho kimetokea leo, naomba kiandikwe katika vitabu vya historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kwa mwendo huu ya kwamba itakapokuwa tunafika mahali mambo ya msingi ambayo hayatofautiani kifalsafa katika vyama vyetu, tunapaswa kusimama kama Watanzania. Kwa hiyo, waliokuwa wanafikiria wanawenza kutumia vyama vyetu kutugawanya kama Watanzania katika Bunge hili wamefeli kabisa, wamepata ziro.

Mheshimiwa Spika, ninapenda niseme kitu kimoja imetokana na kujitolea, siku zote ndugu Degera, Mheshimiwa Mbunge wa Kondo analalamika juu ya mtaro wa Ntomoko, mtaro wa Ntomoko watu tumejitolea kutoka maeneo mbalimbali katika nchi hii ili kuujenga lakini sasa hivi Mheshimiwa anakosa hata nyenzo ya kuongezea pale ili kuweza kufanya ule mtaro uweze kuendelea kufanya kazi kama ulivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, tuna mifano mingine katika historia yetu, wakati tunapata uhuru, mimi nilikuwa bado mtoto mdogo, lakini niliwahi kwenda Dar es Salaam kusalimia ndugu, Magomeni yote ilikuwa makuti, lakini imejengwa kwa njia ya kujitolea.

Mheshimiwa Spika, mifano ni mingi, kinachotokea sasa ni ile dhana ya kujitegemea. Katika *debate*, tumesikia watu wanasema wafadhili walikataa, wafadhili hawakupenda, sawa hawawezi wakapenda kuiona Tanzania inaanza kupiga hatua ya kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku moja Mwalimu alisema ukiona unasifiwa na shetani utakuwa una matatizo, sasa tukisifiwa kupita kiasi na wale ambao wamezoea kutufadhili basi tuna matatizo, sasa tunaanza njia ya kujitegemea.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mimi ninapenda nitoe mifano michache tu, kama wenzangu walivyosema, Mfuko huu sio ule utakaojenga daraja kama la Rufiji, hiyo sio kazi yake lakini kujenga makaravati kwenye kibarabara cha kijijini ama kinachounganisha Kata na Kata, hii ndiyo itakuwa kazi yake. Kwa hiyo isije watu wakaenda kusema wamepewa Mfuko imekuwaje, Mbunge haleti pesa, amekula, watadanganya wananchi, wananchi popote mlipo, mjue ni kichocheo. Kama Nibuye, mmeomba karavati tatu, barabara mmeshalima, kazi yake ni mimi nirudi, nikae na Kamati, sio niamrishe mimi, nikae na Kamati niseme jamani wale watu wameshalima

barabara mpaka mahali fulani, wanashindwa kuvusha kwa sababu kuna mto unaowazuia, hapo tunawaongezea nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mifano mingine, watu wanachimba wenyewe visima, wanavijengea, wanakosa *pump*, ndiyo kazi ya Mfuko huu. Lakini vijana wetu ambao wakati mwingine wanafanya kazi kwa mikono yao wanahitaji wasaidiwe tu kamashine kadogo kakushindilia barabara, hii ndiyo kazi ya Mfuko ili waweze kuvuka. Pendekeso langu ni kwamba twende kwa vijana, twende kwa kina mama, wanakwama vitu vidogo vidogo ambavyo vinawazuia.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikwenda nchi ya Uchina mara nyingi tu, kitu ambacho kilinifurahisha ni kimoja na hiki nakitoa ili wale vijana wanaojiona wamebobeia katika harakati wakifahamu. Wachina walipokuwa katika hatua zao za kuendelea, walihakikisha kila kijana msomi kwenye miji mikubwa anakatwa mshahara kupeleka nyumbani kusaidia ujenzi wa kazi hizi ambazo zitafanywa na Mfuko. Je, wanaharakati wamechangia kiasi gani katika sekondari za kata? Je, wanaharakati wamechangia kiasi gani kujenga barabara za vijiji? Je, wanaharakati wamechangia kiasi gani kusaidia kusomesha vijana wenzao ambao wanahangaika hawana kazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza hapa tuje na Muswada, Serikali itunge, tuwakate hawa walio na uchungu wa maendeleo katika mishahara yao, turudishe katika vijiji vyao na tuweke kwenye Mfuko wa Jimbo kusaidia kuunenepesha. Kwa sababu tusiwe mafundi wa kusema na hatusaidii wananchi, kule vijiji wanahangaika jamani, mara mchango wa barabara, mara mchango wa darasa, mara mchango wa zahanati na humuoni msomi yejote ambaye anarudi kwenye vijiji kuwasaidia, leo Serikali imehangaika pamoja na Wabunge na Spika, kutafuta pesa hizi, wanasema tunavunja Katiba na kutishia tupelekwe Mahakamani, mimi siku hiyo naingoja kwa hamu ambayo Bunge la Tanzania linapelekwa Mahakamani kwa kutafuta uwezo wa kuwapelekea watu wa Nebuye waliokosa makaravati, eti kwa sababu tumevunja sheria, hiyo siku naiongoja kwa hamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine, Afrika imeharibika kwa watu wa namna hii, wepesi wepesi tu kuiba na kutumiwa, wanachochea, wanavuruga hali ya hewa na sisi tunatizama. Mimi nadhani suala hili tuje tulizungumze kwa sababu hizi vurugu zinaweka sumu, sumu mpaka inafika mahali badala ya kuwasaidia wananchi wetu tunawachanganya akili wananchi kwa sababu ya haya mambo ya mchezo mchezo ambayo watu wanayazungumza.

MBUNGE FULANI: Waeleze!

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Hiyo kengele ya mwisho?

WABUNGE FULANI: Ya kwanza, endelea.

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, ninapenda niseme jambo lingine, kwa Waandishi wa Habari.

MBUNGE FULANI: Eeh!

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, tumelalamika mno juu ya kutokuwa na *agenda* inayotupeleka kwenye maendeleo, mmepeata *agenda*, tutakapokuwa tunajenga miradi hii, pigeni picha mnavyotaka muweke wananchi waone, mambo ya blabla na kutafuta vijisenti yaachwe. Sasa hivi kama tulikuwa hatujawapa *agenda* ya kutosha, hii ndiyo *agenda* ya kwamba muandike Ukerewe kijiji fulani wamepata kisima kutohana na Mfuko wa Kichocheo, wamepata *pump*, Mafia, wanakochokoa pweza, wamesaidiwa kiasi hiki kuweka pweza wao katika hali nzuri, hiyo ndiyo *agenda* sasa ya Waandishi wa Habari, nyie ni Watanzania mtusaidia katika kulieleza suala hili. Sisi tutaeleza Majimboni kwetu kwa vitendo na nyie endeleeni kueleza kwa kalamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, katika mjadala huu unaoendelea Bungeni, Serikali imepokea na kufuutilia manung'uniko ya baadhi ya Wabunge, kuhusu kutoridhishwa na tabia ya wageni ambao wako nchini wakiwemo baadhi ya Mabalozi kuingilia shughuli ya ndani za nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba shughuli za Mabalozi wanaowakilisha nchi zao nchini kwetu na shughuli za mabalozi wetu wanaowakilisha Tanzania kule Duniani, zinatawaliwa na kuongozwa na Mkataba wa Kimahusiano wa Viena, yaani *The Vienna Convention* ya mwaka 1961.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa faida ya Mabalozi wapya na wageni ambao hawaelewii sheria hizi, kujaribu kulitumia Bunge hili ku-*communicate* na kujaribu kuwaeleza wenzetu nini wanachotegemewa kukifanya.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 41(1) cha *Viena Convention* ya mwaka 1961, inasema na ningependa kunukuu kwa Kiingereza:-

"Without prejudice to their privileges and immunities, it is the duty of all persons enjoying such privileges and immunities to respect the laws and regulations of the receiving State. They also have a duty not to interfere in the internal affairs of that State". (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa Kiswahili chake cha kawaida inasema kwamba:-

"Bila kuathiri kinga na haki za Mabalozi au za kibalozi katika nchi hizo wanazowasilisha, ni wajibu wa Mabalozi hao na watumishi wao katika Ubalozi huo, kuheshimu sheria na taratibu za nchi ambazo wanaziwakilisha au za wenyeji. Pia ni

wajibu wao kutokuingilia katika masuala ya mambo ya ndani au mambo ya ndani ya nchi wanazoziwasilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kifungu cha 41(2) kinatamka pia kwamba:-

"In case, any diplomatic or any officer working in the diplomatic mission has a complaint or is not satisfied with anything, he has the duty to report that matter to the Ministry of Foreign Affairs where will be dealt accordingly".

Mheshimiwa Spika, hapana kwenda mitaani, kama wewe Balozi huridhiki na shughuli za nchi yetu, hutakiwi kwenda kuwaambia wananchi nini cha kufanya, unatakiwa uende kwenye Wizara ya Mambo ya Nje, ukiwa umeandika, kule sisi tutakushauri. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Una akili sana!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya kistaarabu sana, inaheshimu haki na uhuru kwa Watanzania ni kitu ambacho hakina mjadala. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Waeleze!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuwaonya na kuwataka Mabalozi ambao wanautumia au wanatumia nafasi yao ya uongozi vibaya, waache kushinikiza wananchi kwa hali na mali ili kufikia malengo ambayo wao wanayafahamu zaidi kuliko Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunawataka waheshimu sheria na taratibu za nchi yetu na waache kuingilia mambo ya ndani ya nchi yetu. Wizara yangu ya Mambo ya Nje, haitasita hata siku moja, kumvumilia Balozi ambaye tukipata ushahidi kwamba anatumia pesa zake kushinikiza watu wawe wa nje au wa ndani ili kuwafanya Watanzania washughulikie mambo anayoyataka yeeye, tutachukua hatua za mara moja za kidiplomasia kumwajibisha mtu huyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania waachwe wafanye na kuamua mambo yao wenyewe bila kuingiliwa na mtu yoyote. Ni wajibu wao kuheshimu sheria za nchi na kwamba kitendo cha kushinikiza wananchi wetu kuchukua hatua wanazositaka wao, ni kuwatukana Watanzania ambao wana akili timamu za kuamua mambo yao wenyewe kama suala hili la *CDF* ambalo Serikali inaliunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kupigilia msumari kwenye jeneza la hoja potofu. Kwa hiyo, nadhani kazi ya mtoa hoja ni nyepesi kabisa. (*Makofi/Kicheko*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mabalozi mbalimbali waliohusika kwenye mchakato mzima wa kuanzisha Mfuko wa Jimbo. Shukrani zangu za dhati kabisa ziende kwa Mheshimiwa Lowassa aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo na pia shukrani za dhati kabisa ziende kwa Mheshimiwa Pinda, Waziri Mkuu wa sasa. Hawa ndugu zetu kwa nyakati tofauti wamefanya kazi kubwa sana ya kuanzishwa kwa Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu utasaidia sana kuleta maendeleo kwenye maeneo yote kuanzia kwenye Vitongoji, Vijiji na Kata. Wananchi wetu wanaanzisha miradi mingi sana ya maendeleo lakini wanakosa misaada ya kumalizia miradi yao. Mfuko huu utasaidia pia kuwawezesha Madiwani wetu kuchangia miradi iliyoko kwenye Kata zao kwani Diwani na Mbunge kazi yao ni moja ya kuwasaidia wananchi kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana kwani Mfuko huu utakuwa na Kamati Maalum ya kuidhinisha miradi ya kuchangiwa, Mbunge atakuwa msimamizi tu, lakini Mfuko huu utakuwa kwenye uangalizi wa Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya, pia atakuwepo Afisa Mipango, Madiwani ambao watachaguana wenyewe na Mwakilishi wa Asasi za Kiraia zilizopo Jimboni. Hapa kuna baadhi ya Majimbo yatakosa Uwakilishi wa Asasi kwani hazipo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu ndio utakaozifanya Asasi nyingi sasa zihame mijini na kwenda waliko wananchi maana maendeleo yatakayoletwa na Mfuko wa Jimbo, wasipobadilika umaarufu wa Asasi hizo utakwisha.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Ofisi yako itoe elimu ya kutosha nchi nzima ili viongozi na wananchi kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Vitongoji, waufahamu Mfuko wao huu ambao Mbunge ni msimamizi tu. Kwa kuwa Mfuko huu tunataka uwe kioo cha mifuko mingine kwa uzuri, Wakurugenzi wa Maendeleo lazima wahakikishe miradi inayofadhili na Mfuko huu inafuatiliwa na kukaguliwa na Mkaguzi wa ndani na taarifa zake zinapelekwa kwa Wakurugenzi na Wakaguzi wa Mkoa (*External Auditors*).

Mheshimiwa Spika, sasa umefika wakati wa fedha zote zinazoingia nchini kupitia Asasi za Kiraia, zianze kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*). Pia tunakokwenda, ni lazima uanze kupitia kwenye ‘*Busket Fund*’ kama fedha zingine kama za afya, barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu katika kuchochea maendeleo ya Taifa letu. Ninao ushuri katika maeneo machache.

Kwanza kabisa, katika Sehemu ya I, Ibara ya 3, inayohusu tafsiri, ninapendekeza iwepo tafsiri ya ‘*The Member of Parliament*’ kwani haya yanajitokeza Sehemu ya IV, Ibara ya 12(2).

Mheshimiwa Spika, ushauri wa pili ni kuhusu Sehemu ya II, Ibara ya 10(1)(c). Hapa tumeambiwa ya kuwa watakuwa Wajumbe wasiozidi sita lakini ukihesabu idadi pamoja na Mwenyekiti watakuwa Wajumbe saba. Lakini hata hivyo, kifungu kidogo cha (c) hakijatajwa atakuwepo Mjumbe gani (imeachwa wazi). Napendekeza aongezwe Afisa Maendeleo ya Jamii kwani miradi inatakiwa kuibuliwa na jamii na bila shaka kabisa itakuwa ni miradi ya kijamii. Hivyo, Afisa Maendelo ya Jamii, ni mtu muhimu katika Kamati ya Mfuko.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa tatu, unahusu sehemu ya VI, Ibara ya 19. Ninashauri kwamba baada ya 19(1), kiongezwe kifungu kingine kitakachoelezea kwamba angalau asilimia 50% ya miradi iwe ile inayowalenga walemavu, wajane, watoto walioko katika mazingira hatarishi, wanawake na wale walioathirika na virusi vya Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza hivi kwa sababu hawa ndio kundi ambalo Serikali hailipatii fungu la moja kwa moja kiasi kikubwa ikilinganishwa na maeneo kama elimu, miundombinu ya barabara na afya. Ukichukulia maeneo haya niliyoyataja, maendeleo yake yanapimika na ni makubwa. Kiwango cha umaskini wa kukosa chakula, tunaweza kusema kwa kiasi kikubwa, kinachangiwa na makundi niliyoyataja awali (wajane, walemavu, waishio na virusi vya Ukimwi na watoto walioko katika mazingira hatarishi). Kwa hiyo, makundi haya yakiwezesewa kufanya miradi ya kupunguza umasikini, Majimbo yetu yataongeza kasi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ninawapongezeni sana nyote kwa kutuletea huu Muswada muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya mwananchi wa Tanzania na utakuwa mkombozi wa matatizo yale ya kada ya chini sana isiyofikiwa na Serikali na hivyo kutimiza ile ahadi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya “Maisha Bora kwa kila Mtanzania”.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Peter Kayanza Pinda, Waziri, Mheshimiwa Celina Kombani na Naibu wake, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi zao na pia kwa ajili ya Muswada huu wa *CDCF*.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa sehemu kubwa ya wananchi wa Tanzania, wanaishi vijiji ambako huduma mbalimbali hasa za jamii ikiwemo maji, umeme, barabara, hospitali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imejaliwa kuwa na fursa nyingi za kiuchumi hasa kutohakana na kuwa na ardhi kubwa na nzuri, maliasili kama vile misitu, mito na mabonde, maziwa madini na maumbile ya dunia yenye mvuto wa kipekee. Kwa bahati mbaya, fursa hizo bado hazitawenza kugeuzwa kuwa chanzo cha kuinua uchumi au utajiri inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zetu zimejitahidi kutimiza wajibu wake, pamoja na kuwepo kwa watumishi wengi, bado hawatoshelezi kuwafikia wananchi wote kwa wakati. Vile vile ili kuharakisha maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla, ni vema kuzidi kuamsha nguvu ya wananchi katika kujilettea maendeleo yao wenywewe.

Mheshimiwa Spika, Mbunge anayewajibika, ni mtu ambaye anasikilizwa sana na wananchi wake, ni mshawishi muhimu na mwelekezi, anastahili kuhamasisha kwa vitendo hasa kwa kuchangia baadhi ya mambo madogo ambayo yapo nje ya uwezo wa mwananchi au yatapelekea mradi kuchukua muda mrefu kukamilika na kupoteza dira. Hali ya sasa, Mbunge hulazimika kutumia ziada au sehemu ya kipato chake. Katika hali hiyo, ndipo uwezo wa Wabunge hao hutofautiana na hivyo kupelekea rushwa za aina kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini basi pamoja na kuunga mkono Muswada huu, nashauri yafuatayo:-

Kwanza, kuwe na taratibu ya kila Mbunge wa Jimbo, kutolea taarifa Bungeni kwa kila Mkutano (*progress report*) na angalau nusu mwaka ili kuona kasi ya mafanikio ya Mfuko huo.

Pili, Wabunge wa Viti Maalum, kazi zao ziainishwe si tu ndani ya Chama, bali hata Kibunge ili kujua au kuweka wazi mipaka yao katika kazi na maeneo na jinsi watakavyohusika katika Mfuko huo. Hali ya sasa ya uwakilishi wa Wabunge wa Viti Maalum, ukiacha katika kazi za vikao vyta Kamati za Bunge na Mikutano ya Bunge, katika maeneo tunayotoka, tunafanya kazi katika hali ya kuogopana na hisia za aina mbalimbali. Hii yote ni kwa kuwa mipaka au (*jurisdiction*) ya Mbunge wa Viti Maalum haiko *transparent*.

Mheshimiwa Spika, ni vema basi utaratibu wa sasa uboreshwwe kwani hata Wabunge wa Viti Maalum, wanatumia mishahara ya kodi za wananchi basi majukumu yao yawe wazi. Mfano hata Kamati zilizokuwa zimeshughulikia Mfuko huo, hazikuwa na Wabunge Viti Maalum. Pia tunashauri Wabunge wa Viti Maalum kuwemo katika Kamati husika za Mfuko huo ili kusaidia katika usimamizi wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda niipongeze Serikali kwa kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo wa mwaka 2009. Muswada huu, kwa ujumla, umechelewa sana kuletwa kwa kuusoma, kuujadili na kuupitisha.

Mheshimiwa Spika, kwa miezi kadhaa hivi sasa, bila hata kuuona Muswada wenyewe, vyombo mbalimbali nya Habari na Asasi za Kiraia, zimekuwa zikieneza maneno ya kuupotosha umma wa Tanzania kuwa nia na madhumuni ya Mfuko huu, ni kuhalalisha takrima na hivyo kumnuifaisha Mbunge katika matayarisho ya Uchaguzi Mkuu wa 2010. Wengine wakieleza kuwa kwa kuhalalisha Mfuko huu, Bunge litakuwa linachukua nafasi ya utendaji badala ya usimamizi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema, upotoshaji na uzushi huu, hauna hoja ya msingi. Mfuko huu pekee ndio ambao unaweza kugawa misaada kwa uwiano mzuri bila upendeleo wowote.

Mheshimiwa Spika, kwa zile Asasi za Kiraia zinazodai kuwa zinafanya kazi ya maendeleo ya wananchi, napenda kuweka bayana kuwa zina agenda iliyofichika ambayo inalenga kuendeleza ubadhilifu wao wa misaada inapotolewa na wadau wa maendeleo mbalimbali wakiwemo wa nje, kwani uwepo wa Mfuko huu utawaamsha wananchi na kuwawezesha kutambua jinsi ambavyo wamekuwa wakiibiwa na Asasi hizo. Kwa upande wa Majimbo ya Vijijini, hizo Asasi za Kiraia wala hazijawahi kufika, hivyo hazina haki ya kuongea lolote juu ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi, ambao kitu`Asasi za Kiraia` hakijawahi kukanyaga ardhi yake, wanaunga mkono asilimia mia moja hoja hii, kwani hata muundo wa usimamizi na uendeshaji wake ni wa uwazi na ukweli mtupu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu kwa wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi, ni chanzo muhimu cha uchochezi wa maendeleo yao. Hivyo basi, udumu Mfuko wa kuchochaea maendeleo ya Jimbo.

MHE. JOHN PAUL LWANJI: Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha Mfuko huu muhimu sana. Ni kweli kabisa kuwa Wabunge na Madiwani ndiyo wanaojua wapi kwenye matatizo ya maendeleo. Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu umekuja wakati muafaka wa kuchochaea maendeleo na hapo ndipo dhana nzima ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya inapokuwa ya kweli kwa Mfuko huu kuchochaea maendeleo. Mfano, Mheshimiwa Gadaffi, anapanga kuja na utaratibu mzima wa Libya kuwa na mfumo wa bajeti utakaoruhusu Wabunge mara wanapomaliza kuitisha bajeti wanaondoka na *cheque* za Halmashauri zao moja kwa moja na kusimamia matumizi yake kwa kushirikiana na mamlaka ya Halmashauri yake, hakuna kusubiri. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwashukuru Wabunge waliochangia hoja hii. Muswada huu ni mzuri sana, unafanana sana na Sheria inayotumika huko Kenya, Uganda na Zambia. Tatizo ninaloliona, ni jinsi gani Mfuko utatumika. Ninashauri Waziri atoe *Subsidiary Legislation* mapema iwezekanavyo ili ifafanue jinsi fedha hizo zitakavyogawiwa. *Implementation rules must be clear* ili *abuses* zisijitokeze. Napenda pia kujua ni jinsi gani Madiwani Viti Maalumu watashiriki.

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kujua Mfuko huu utagawanywaje kwa kuwa Majimbo tulyonayo nchini hayalingani. Ninapenda kuona *a level playing field in terms of population size of the wards etc.* Nasema hivyo kwa kuwa Majimbo yetu hayalingani, ninapenda *Subsidiary Legislation* itakayotungwa ifafanue kwa undani ili kuziba mianya mbalimbali ambayo Sheria yenyewe haikuzingatia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo niliyoandika, naunga mkono Muswada huu.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru Mungu kupata fursa hii. Nampongeza Mheshimiwa Celina O. Kombani (Mb), Waziri Tamisemi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri (Mb), Naibu Waziri Tamisemi, Katibu Mkuu, Bibi Maimuna Tarishi na Watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Muswada umekuja wakati muafaka. Muswada utachochea shughuli za Kimaendeleo na kuboresha hali za Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya III ya Muswada, inayozungumzia Kamati, sehemu inayotaja Wajumbe wa Kamati, pale kipengele 10(e), Wajumbe ambao ni *Ward Executive Officer* toka kwenye Kata, napendekeza badala ya kusema Mjumbe ni *Ward Executive Officer (WEO)* isomeke *two Ward selected within Constituency represented with Ward Executive Officers hold the office.* Hii itasaidia iwapo utatokea uhamisho wa *WEO* toka Jimbo moja kwenda lingine badala yake yule atakayerithi Ofisi ya kata ambayo ni Mjumbe aendelee kuwa Mjumbe kwa jina la ujumbe wa Kata aliyoteuliwa.

Mheshimiwa Spika, fedha za Mfuko huu zitolewe kwa wakati ili kuepuka usumbufu wa Kamati kuitisha miradi bila utekelezaji kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, upande wa *signatory group (b)*, ninapendekeza *Council Treasurer* na *Council Accountant*, waondolewe kwa kuwa wamewakilishwa na Afisa Masuhuhuli ambaye ni *Council Director* na badala yake wawe ni wale *two Councilors* ambao watawakilisha upande wa watunga sera.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali, kwa kuwasilisha Muswada huu ambao una lengo la kuchochea maendeleo ya wananchi kwa kuunga mkono michango yao wanayojitolea kwa kidogo walichonacho ili kuinua maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kuridhia kuanzishwa kwa Mfuko huu. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri, Kamati na Wabunge wote walioshiriki kuandaa na kuukamilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ili Mfuko huu ufanye kazi na kutimiza malengo yake vizuri kwa manufaa ya wananchi, Serikali ichukue hatua za haraka kuelimisha jamii ili waulewewe na kutambua namna utakavyowanufaisha wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali izichunguze kwa makini Asasi zisizo za Serikali, zilizokuwa mstari wa mbele kuupinga Mfuko wa Jimbo ili kubaini malengo yao ambayo yana kila dalili za kupingana na dhamira ya kweli ya Serikali ya kuwawezesha wananchi kusaidia kutimiza miradi waliyoibua.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Asasi zisizo za Serikali zina akili timamu, kupinga kwao nia nzuri ilio wazi ya Mfuko huu, ina maana zinaipinga Serikali kuchochea maendeleo ya wananchi! Swali la kujiuliza ni kwa nini wapinge nia hii?

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, ninadhani baadhi ya Asasi zisizo za Serikali zinatumwa na watu au taasisi za ndani au za nje ya Tanzania, wenyewe nia au lengo la kutudumaza na kutuharibia mshikamano baina ya Bunge, Serikali na wananchi wake. Nia za aina hii zinapenyezwa kijanja kama hivi. Ni lazima, tuzidhibiti haraka Asasi kama hizi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mikumi, ninaomba Mungu aibariki hoja hii, ninayoiunga mkono asilimia 100% kwa kuamini kabisa kuwa utawachochea wananchi kutekelezwa kwa miradi waliyoibua wao wenyewe.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, shukrani nyingi kwa kuleta Muswada huu. Kimsingi, Muswada hautoi nafasi hata ndogo ya ubadhirifu kwa jinsi Kamati ilivyoundwa na kudhibiti. Kwa Zanzibar, mifuko inayosaidia jamii ukiondoa msaada wa Serikali, ni Mfuko wa *TASAF* na Mfuko wa *ACTION AID* tu. Kwa hali hii, Mfuko huu utasaidia sana kutatua matatizo madogo madogo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kimsingi nakubaliana na Muswada huu. Hata hivyo, napendekeza kipengele cha 10(7), kinachozungumzia Mwenyekiti wa Kamati pale Mheshimiwa Mbunge asipokuwepo, nashauri awe Diwani na siyo Sheha. Hasa kwa kuwa Diwani, ni Kiongozi wa Kisiasa wa kuchaguliwa na wananchi wakati Sheha ni Mtendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nakuombea kila la kheri na naunga tena mkono hoja.

SPIKA: Sasa namwita Mtoa hoja aweze kuhitimisha hoja yake.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI: Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema, kazi yangu ni nyepesi sana. Kwanza, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao na kwa kutoa ufanuzi wa kina katika suala hili. Kwa kweli siku ile niliyokutana na wale ndugu zetu wa *Policy Forum*, tuliwaelimisha na baadhi yao walituelewa na leo mmefanya kazi ya ziada kuelimisha

umma wa Watanzania. Nafikiri Watanzania wote sasa hivi wanaelewa ni nini maana ya Mfuko huu, kazi zake, madhumuni yake na kadhalika. Kwa hilo, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue Wabunge wote ambao walizungumza kwa maandishi pia na waliozungumza kwa kuchangia moja kwa moja. Naomba kutambua mchango wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Bernard Membe, hao wote walichangia kwa kuzungumza. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutambua mchango wa Waheshimiwa Wabunge waliochangia kimaandishi ikiwa pamoja na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Dkt. Lucas Siyame, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa na mwisho Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, ni machache tu ambayo nitayapitia moja kwa moja na la kwanza ambalo lilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, ni kuhusu marekebisho mbalimbali. Kama utaona tulileta *Schedule of Amendment*, imejieleza na yote ambayo waliyasema kwenye Kamati, tumeyafanyia marekebisho, nafikiri Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ameridhika nayo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili lilichangiwa na Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Halima Mdee na Waheshimiwa Wabunge wengine. Wanasesma Serikali iwe na mkakati wa kuwaelimisha wananchi kuhusu matumizi na manufaa ya Mfuko huu. Kama nilivyosema, mmeshafanya kazi ya ziada kuwaelimisha wananchi na sisi kwa upande wa Serikali, tutahakikisha kwamba tunatoa elimu kuanzia kwa Wakurugenzi, watendaji wa Halmashauri pamoja na wananchi kwa ujumla. Hilo tumelipokea na tunalifanya kazi. Aidha tutaandaa kipindi cha elimu kwa umma, kuwaelimisha wananchi kuhusu Mfuko huu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ilikuwa Serikali isimamie kanuni za fedha na uadilifu wa watumishi wa umma, hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati na Waheshimiwa Wabunge pia. Tunasema ushauri huu unazingatiwa, watumishi wa umma watakohusika, wataelimishwa na kuaswa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma kwa sababu fedha hizi ni kama fedha nytingine, kwa hiyo, watumishi wanastahili kufuata sheria na kanuni kama ilivyo kwa fedha nytingine. Kwa hiyo, hilo tumelipokea na tutalizangatia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, suala la nne lilikuwa ni suala la ufanuzi tu, Mwenyekiti wa Kamati alisema pia kuhusu elimu kwa umma, nafikiri hilo limeelewaka.

Suala la tano, lilikuwa kanuni zieleze utaratibu wa kuteua wajumbe wa Kamati, hili lilitolewa na Mheshimiwa Mdee, tunasema kwamba kanuni zitaelezea taratibu za kuteua wajumbe wa Kamati pamoja na masuala yanayohusu Mfuko huu. Hilo limepokelewa na litafanyiwa kazi kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hoja namba sita, ilikuwa uendeshaji wa mfuko huu izingatie misingi ya uwazi na uwajibikaji, pia lilitoka kwa Mheshimiwa Halima Mdee, tunasema ushauri umezingatiwa uendeshaji wa Mfuko huu utazingatia sheria na misingi ya uwazi na uwajibikaji. Kwa kuwa wananchi watashirikishwa moja kwa moja, kwa hiyo, tuna uhakika kwamba misingi ya kidemokrasia, uwazi na uwajibikaji, vitakuwepo katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, suala la saba, ni Wabunge Viti Maalum nao wafikiriwe katika Mfuko huu, hilo lilitolewa na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, tunasema ushauri ni mzuri, tunaupokea na tutaufanyia kazi. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya alisema Wabunge wa Viti Maalum wawe wajumbe wa Kamati ya kuchochea Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo, tunesema kwamba hilo nalo tumelipokea, tutalifanyia kazi na tukishalifanyia kazi, tutawaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeweza kuliweka kwenye kanuni au vipi, tutawapa ripoti hiyo.

Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, pia alisema Wabunge watoe *progress report* Bungeni kwa kipindi cha miezi sita, tunasema utaratibu wa kutoa taarifa Bungeni unamtaka Waziri mwenye dhamana na suala husika ndiyo awasilishe taarifa Bungeni ili Wabunge wapate nafasi ya kuhoji kwa urahisi zaidi Mbunge mwenyewe akitoa *progress report*, nani atamhoji? Kwa hiyo, hilo tunesema Waziri mwenye dhamana ndiyo anatakiwa kutoa taarifa Bungeni kama atatakiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, namba tisa, Waziri atunge kanuni ambazo zitaeleza vigezo vya kugawa fedha kwa kuzingatia ukubwa wa Majimbo na idadi ya watu, hiyo tayari tumeshaiweka kwenye sheria na ipo katika *section 24*.

Mheshimiwa Spika, kumi kigezo cha ukubwa wa Jimbo kiongezwe kutoka asilimia 10 kwenda asilimia 15, hilo ni wazo la Mheshimiwa Ponsiano Nyami. Tunasema kwamba kwa kuanzia vigezo vitabaki kama vilivyo. Hata hivyo, endapo itaonekana haja ya kufanya mabadiliko, utaratibu wa kubadilisha vigezo hivyo utafuata. Mimi nasema kwamba, tuanze na vigezo hivi vilivypo, pale ambapo tutaona kwamba kuna ulazima wa kubadilisha basi katika utekelezaji, tutaona ni jinsi gani tutabdalisha lakini ni vyema kwanza tuanze halafu baadaye tutaona, je, ni matatizo gani yametukabili, ndio tuweze kubadilisha vigezo hivyo.

Mheshimiwa Spika, lilitolewa pendekezo na Mheshimiwa Anastazia Wambura amesema kwamba sehemu ya 1(3) inayohusu tafsiri ya maneno, the *Member of*

Parliament, amesema kwamba ni vyema tafsiri hiyo ikawekwa kwenye tafsiri ya maneno mbalimbali. Tunasema kwamba *Member of Parliament* haitaji tafsiri kwa kuwa ni *common knowledge*, hasa kwa kuwa kipo kifungu cha 10(1) kinachoeleza ni Mbunge yupi, kifungu hicho cha 10(1) kinaeleza kwamba *elected Member of Parliament*, kwa hiyo, hapa inajieleza kabisa kwamba tukisema *Member of Parliament* hapo tuna maana gani.

Pia alipendekeza sehemu ya 3 ya kifungu 10(1)(c), hakijatajwa katika ukurasa wa 10, tunasema kwamba hiyo tayari imeshakuwa *taken care* kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, pia alitoa pendekezo kwamba idadi ya wajumbe kwa mujibu wa kifungu namba 10(1) ni saba na sio sita, ni kweli kama alivyosema, wako wajumbe saba ukiunganisha pamoja na Mwenyekiti wa Kamati. Kwa hiyo, marekebisho hayo yatafanyika.

Mheshimiwa Spika, pia alitoa mapendekezo kwamba Afisa Marekebisho ya Jamii aongezwe kwenye Kamati ya Mfuko. Tunasema kwamba katika muundo wa Halmashauri, Afisa Mipango ndiyo msimamizi mkuu wa shughuli zote za miradi ya maendeleo na kwa kuwa kuongeza idadi ya wajumbe, kunaongeza gharama za Kamati, ni vyema kwa sasa wajumbe wakabaki kama walivyopendekezwa kwenye Muswada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia alisema baada ya kifungu 19(1), kiongozwe kifungu kingine kitakachoeleza aina ya miradi itakayofadhiliwa na Mfuko. Tunasema kwamba ukianza kueleza aina ya miradi itakayofadhiliwa na Mfuko, ni hatari kidogo kwa kuanzia kwa sababu kitakuwa kinamfunga Mbunge na Kamati yake. Miradi tunayosema, ni kama miradi ya shule, zahanati, maji na kadhalika. Kwenye miradi ile, tumeelezea kabisa isiwe miradi ya kisiasa wala ya kidini, tukiwafunga hapa, tuweke kwenye sheria kwamba miradi itakayohudumiwa ni miradi fulani, tunatofautiana kimajimbo, kila Jimbo lina matatizo yake na kila Jimbo lina vipaumbele vyake. Kwa hiyo, tukasema kwamba tukiwafunga, kwa kweli tutakuwa hatuwatendei haki, ni vyema tukaiachia ile Kamati ambayo tunaamini kwamba itafanya kazi yake ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ilitolewa hoja na Mheshimiwa Juma Killimbah, amesema Mweka Hazina na Mhasibu wa Halmashauri, waondolewe katika orodha ya watia saini, sisi tunasema kwamba Mweka Hazina na Mhasibu wa Halmashauri, ndiyo wanaosimamia fedha zote za Halmashauri, hivyo kuwaondoa katika orodha ya watia saini, kutadholofisha usimamizi wa sheria, kanuni na taratibu za fedha. Kwa sababu tunafahamu kabisa wao ni *signatories* kwa mujibu wa Sheria za *Local Government Finance*. Kwa hiyo, si vema kuwaondoa katika kutia saini kwenye fedha tu za Mfuko wa *CDCF* kwa sababu fedha zote, hao ndiyo wanaweka saini, tuliona kwamba si busara kuwaacha au kuwatoa katika kusaini fedha hizo.

Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, ye ye alizungumzia Ibara ya 10 (7), kwamba Mbunge anapokuwa hayupo kwa upande wa Zanzibar badala ya Sheha, Diwani

ndiye awe Mwenyekiti. Mimi nasema suala hili limepokelewa na limefanyiwa kazi kwenye *Schedule of Amendments*, ilikuwa tu ni makosa ya kiuchapaji.

Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, ye ye anasema fedha hizi zitolewe kwa mkupuo. Kama tunavyofahamu ni kwamba bajeti yetu inakwenda kwa mtindo wa *cash budget* lakini hata hivyo kama utaangalia vizuri kwenye kifungu nadhani cha 24, tulisema kwamba tutatoa katika awamu mbili. Kwa hiyo, tutakuwa tunadunduliza awamu ya kwanza tunatoa kwa mkupuo halafu awamu ya pili tunamalizia. Hali ikiwa nzuri, kwa kweli kwa kuwa fedha zenyewe ni kidogo sana sehemu nyingine shilingi milioni 20 na sehemu nyingine shilingi 40, kwa hiyo kuzitoa kidogo kidogo hilo tumeliona na tutalifanya kazi ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatolewa kwa mkupuo au kwa awamu mbili kama tulivyojielekeza wenyewe kwenye maandishi.

Mheshimiwa Spika, natambua mchango mzuri ambao umetolewa na Mheshimiwa Bernard Membe, ameелеzea vizuri sana.

Mheshimiwa Dr. Getrude I. Mongella, ye ye alitusaidia sana hata kwenye kikao hicho cha *Policy Forum*, kwa hiyo anaelewa ni nini ambacho kilielezwa ndani ya kikao kile.

Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo kutokana na ile *exposure* yake ambapo amekwenda sehemu mbalimbali, naye ameona kwamba Mfuko hauna matatizo, kwa hiyo tunatambua mchango wake.

Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, pia tunatambua mchango wake na ninawashukuru sana kwa uchangiaji wenu kwa kweli mmenifanya mimi kazi yangu iwe rahisi.

Mheshimiwa Spika, niliona nitoe hayo machache lakini mengi tutaendelea kuelimishana. Nawashukuru wote na ninasema tena ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kwa majumuisho hayo mazuri na pia umeturahisishia kazi ile inayofuata.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo wa Mwaka 2009 [*The Constituencies Development Catalyst Fund Bill, 2009*]

Sehemu ya 1

Ibara ya 1

Ibara ya 2

(Ibara zilivyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 3

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Sehemu ya 2

Ibara ya 4

Ibara ya 5

(*Ibara zilichotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 6

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 7

(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 8

Ibara ya 9

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Sehemu ya 3

Ibara ya 10

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu marekebisho ya Serikali ndiyo yaleyale ambayo nimeyapendekeza, naomba kuondoa marekebisho yangu ili yabakie yale ya Serikali.

MWENYEKITI: Safi sana!

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 11

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Sehemu ya 4

Ibara ya 12

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 13

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Sehemu ya 5

Ibara ya 14

Ibara ya 15

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Sehemu ya 6

Ibara ya 19

Ibara ya 20

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Sehemu ya 7

Ibara ya 21

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 22

(*Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Sehemu ya 8

Ibara ya 26

Ibara ya 27

Ibara ya 28

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Jedwali la 1

(*Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

(*Bunge lilirudia*)

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuanzisha Mfuko wa Kuchochea
Maendeleo ya Jimbo wa Mwaka 2009 [The Constituencies Development Catalyst
Fund Bill, 2009]**

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja ilihamuliwa na kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Uisomwa Mara ya Tatu na kupitishwa*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada huo umesomwa mara ya tatu, kwa hiyo, utaandaliwa kwa utaratibu wa kawaida na kufikishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa hatua nyingine zinazofuata.

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana kwa kufanya kazi kwa *speed* inayohitajika hasa kwenye mambo ya msingi kama haya.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia kwenye Muswada unaofuata, naomba nisome maamuzi yangu kuhusu hoja mbili ambazo zimekaa kiporo kwa muda.

MAAMUZI YA SPIKA

Maamuzi ya Spika kuhusu hoja ya Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega, ya kutaka iundwe Kamati Teule ya Kuchunguza Wizara ya Miundombinu kuhusu kuingia mikataba ya ujenzi wa barabara ambazo fedha zake zilikuwa hazijapitishwa na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 29 Juni, 2009, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, alileta ombi kwangu la kutaka iundwe Kamati Teule akiwa anarejea tangazo la Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kuwakaribisha Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu na wengine wa Mikoa ambapo barabara zilizotajwa zingewekwa saini mikataba ya kuzijenga. Mheshimiwa Lucas L. Selelii, alihoji uhalali wa Serikali kuingiza mikataba ya ujenzi wa barabara hizo na makampuni ya ujenzi kabla ya Bunge halijapitisha makadirio ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu tarehe 2 July, 2009.

Nilipokea maelekezo ya Serikali kama ifuatavyo:-

Kwamba barabara ambazo mikataba ya ujenzi wake ilitiwa saini siku hiyo zilikuwa ni kumi, fedha za ujenzi wa barabara ambazo mikataba yake ilitiwa saini zilipitishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Hatua ya kutia saini mikataba, ilikuwa ni sehemu tu ya maandalizi kabla ya ujenzi kuanza. Aidha, mikataba ya miradi hiyo, ilitiwa saini baada ya Bunge kuitisha bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010 mnamo tarehe 19 June, 2009.

Niliielekeza Ofisi yangu ifanye uchambuzi ili kuhakiki maelezo ya Serikali kwa kufanya rejea kwenye *Hansard* ya hotuba ya Waziri wa Miundombinu wakati anawasilisha maombi ya fedha ya bajeti ya mwaka 2008/2009 kuhusu matengenezo ya barabara za Mikoa yaani *Regional Roads. (Makofi)*

Uchambuzi uliofanyika unaonyesha kuwa wakati huo ulikuwapo mtandao wa barabara kitaifa wa tangu mwaka 2007 ambao ulilenga baadhi ya barabara zijengwe kwa kiwango cha lami. Barabara mpya ambazo hazikuwa katika mpango huo wa awali zilibuniwa katika mwaka wa fedha uliokwisha na kupangwa kujengwa haraka haraka tena kwa kiwango cha lami hivyo inaonyesha kwamba kuna mkanganyiko wa upangaji wa madaraja ya aina za barabara yaani *classification of roads* kwani kuna barabara kuu ambazo ziko katika kiwango cha changarawe na zipo barabara za Mikoa, Wilaya na hata Mitaa ambazo ziko katika kiwango cha lami. Kwa hiyo, hakuna vigezo rasmi vya kupanga vipaumbele vya utekelezaji wa miradi ya barabara na viwango vya barabara hizo.

Pamoja na kutambua kwamba barabara ambazo siyo barabara kuu baadhi ya wakati zimejengwa kwa kiwango cha lami kutokana na umuhimu wa barabara husika. Hata hivyo, vigezo vya umuhimu huo navyo havijawekwa wazi.

Waheshimiwa Wabunge, uamuzi ni kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, barabara zinazolalamikiwa ambazo mikataba ya ujenzi wake imetiwa saini hivi karibuni, ni za Mkoa na ambazo awali zilipangwa kujengwa kwa kiwango cha changarawe pamoja kufanya usanifu lakini mikataba ya ujenzi wake inaonyesha zitajengwa kwa kiwango cha lami tofauti na maombi ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka uliopita.

Kwa kuwa, katika hotuba yake ya maombi ya fedha za matengenezo ya barabara hizo, Mheshimiwa Waziri hakutaja kama zitajengwa kwa kiwango cha lami wakati huo yaani zitajengwa kwa lami kwa mwaka unaofuata na kwa kuwa hakuna utaratibu maalum ambao umewekwa wa kutambua ni barabara zifi zinapewa kipaumbele kujengwa kwa lami na hata kwa changarawe, kilichotokea kwa baadhi ya brabara zile 10 na hata kuonekana zinapewa upendeleo kinaeleweka. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa siku za usoni basi, nashauri mipango ya ujenzi wa barabara za Mikoa na za Kitaifa, iwe inafafanuliwa wazi na gharama za ujenzi wake zionyeshwe kwa kila barabara na taarifa ya mpangilio huo iwasilishwe kwenye kila Mkutanowa Bunge la mwezi Februari wakati litakapokuwa linakaa kama Kamati ya Mipango. Lengo ni kuwa na mpango wa utekelezaji wa miradi ya barabara ulio na uwazi na wenyе vipaumbele vilivyokubaliwa na Bunge.

Kwa hiyo, sikubaliani na pendekeso la kuunda Kamati Teule. Mwisho wa uamuzi. (*Makofi*)

MHE. OMARI S. KWAANGW': Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Mheshimiwa Kwaangw'!

MHE. OMARI S. KWAANGW': Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7) inasema:-

“Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa”.

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na uamuzi wako ambao unataka kuweka utaratibu mzuri wa namna ya kupanga vipaumbele vyetu hasa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Sasa ufanuzi ninaouomba ni kwamba umesema mipango na vipaumbele viletwe Bunge linapokaa kama Kamati ya Mipango kila mwezi Februari kabla ya Bunge la Bajeti. Sasa ninaumba mwongozo kwamba mipango itakapokuwa inaletwa au utaratibu huo utakapokuwa unaletwa kama hakuna Kanuni inayotuongoza au Sheria inayotuongoza kwamba iletwe kila mwaka ili tukubaliane wote kwa pamoja kwamba miradi ipi iwekwe

kwenye bajeti kufuata vipaumbele, kama hakuna Sheria au Kanuni, nadhani jambo hilo halitatekelezwa vizuri.

Kwa hiyo, ninaomba mwongozo wako kwamba, je, Serikali itafanyaje jambo hili sasa, itaweka kwenye Sheria au Kanuni ili tuwe tukielewana kwa sababu mambo haya kidogo katika bajeti ya mwaka huu yameleta kutokuelewana lakini tukiyawekea utaratibu wa kisheria, nadhani itakuwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimeomba mwongozo wako kwa Mujibu wa Kanuni hiyo hiyo ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya *ruling* yako ulioitoa pamoja na mambo mengine, umebainisha wazi kwamba barabara iliyokuwa imeombewa fedha iliombewa fedha mwanzoni kwa kiwango cha changarawe na ni barabara ya Mkoa lakini hatua zote za kuweka saini mambo haya yamefanyika na yanahuus fedha na mamlaka ya matumizi ya fedha ni ya Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa mgawanyo wa madaraka. Jambo hili linapotokea na hasa hatua hizo zinapokuwa zimefanyika katika maeneo ambapo ndipo viongozi hao waliofanya hayo wanakotoka na ambalo kimsingi linaelekea kuwa na dalili zote za uvunjaji wa Katiba na taratibu, nilikuwa nafikiri kwamba jambo hili halistahili kuendelea kuachwa liendelee hivi hivi vinginevyo mwingine kesho ataamua kufanya hayo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako juu ya jambo hili kuelekezwa katika Kamati nyingine yoyote ili undani wa jambo hili uweze kufahamika vyema kwa afya ya umoja na kuheshimu mgawanyo wa madaraka kati ya mihimili hii na hili litawenza kuliwekea Bunge letu Tukufu heshima kuliko tukaiacha tu, kukiri kwamba kuna mambo ambayo yamefanyika kinyume cha Katiba yetu halafu tukanyamaza hivi hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozi wako kama kwa kuelekeza jambo hili lishughulikiwe na Kamati yoyote utakayoiona ikiwemo Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kama litakuwa limekwenda kinyume na *ruling* uliyokuwa umeitoa.

SPIKA: Nitaanza na hilo, kwanza hakuna uvunjaji wowote wa Katiba, hilo ni dhahiri kabisa. (*Makofi*)

Lakini pili, kama nilivyoeleza, Ofisi yangu ilipochambua, imeona, nadhani tangu labda nchi yetu ijitawale, hatuna utaratibu hasa ambao unaweka vipaumbele, mara nyingine ni maagizo ya kiongozi na kadhalika basi yanakwenda hivyo. Vijana wangu wamechambua sana, wameona kwa mfano baadhi ya Manispaa, barabara zake nyingi zinajengwa kwa lami na kuna baadhi hakuna kabisa yaani *TANROADS* inajenga. Sasa ndiyo yote hayo nimesema kwa kuwa kulikuwa hakuna utaratibu, si haki kuwaadhibu watu hata kuwafuata katika mazingira ambayo hayana utaratibu. (*Makofi*)

Watani zangu Wayao wanayo methali inasema hivi “Ukishamjeruhi Faru usimfuate kwenye kichaka.” Kwa hiyo, inatosha tu maana yake akikurupuka hapo utakayeumia ni wewe. Nadhani Serikali ina macho na masikio, wameelewa yote yaliyotokea. Kwa hiyo, ombi la Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka nalikataa.

Narudi kwenye mwongozo aliuomba Mheshimiwa Omari Kwaangw’. Ni juu ya Wabunge sasa ninyi kusema, inawezekana kabisa kwamba mkapitisha Azimio katika wakati muafaka maana yake Februari bado mbali, zipo taratibu nyingi. Lakini pia, kwenye nyongeza ya Kanuni kwenye kazi za Kamati, tunaweza kuongeza kwenye Kanuni likafanyika hivyo. Mimi wajibu wangu ni kutoa *ruling* ya utaratibu ambaa naona unafaa, sasa ni juu yenu kama mnataka kuweka utaratibu rasmi basi uje ama kwa pendekezo la Azimio ama kwa mabadiliko ya Kanuni. Lakini mimi naamini Serikali ina nia njema na ni jambo zuri tu tusiwe tunapata mikanganyiko kila mwaka. Kwa hiyo, nawaachia ninyi Waheshimiwa Wabunge muamue la kufanya. (*Makofî*)

La pili sasa, uamuzi wa Spika kuhusu malalamiko ya Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba na Mheshimiwa Salum Salehe Londa, Mstahiki Meya wa Kinondoni dhidi ya kauli ya Mheshimiwa Halima J. Mdee, aliyoitoa Bungeni tarehe 7 Agosti, 2008.

Waheshimiwa Wabunge, uamuzi wangu wa leo, unatokana na malalamiko yaliyowasilishwa kwangu na Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, Mbunge wa Kuteuliwa ambaye katika uamuzi huu ataitwa mlalamikaji wa kwanza na Mheshimiwa Salum Salehe Londa, Mstahiki wa Manispaa ya Kinondoni, mlalamikaji wa pili dhidi ya kauli ya Mheshimiwa Halima J. Mdee ambaye nitamwita mlalamikiwa, aliyoitoa Bungeni tarehe 7/8/2008 wakati akichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Halima J. Mdee, alitoa madai kwamba:-

(a) Mheshimiwa Luteni Yusuf R. Makamba, akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alimlinda Mstahiki Meya Salum Londa kwenye sakata la uuzaji wa viwanja namba 695 na 696 vilivyopo Kawe Amani, Wilaya ya Kinondoni.

(b) Mheshimiwa Yusuf Makamba na Mstahiki Meya Salum Londa, walishiriki kwenye vitendo vya rushwa kuhusiana na uuzaji wa viwanja hivyo.

(c) Watendaji wa Halmashauri walihamishwa baada ya hapo ili kuficha ukweli wa mambo hayo.

Kutokana na kauli ya Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba na Mstahiki Meya Salum Londa, kwa nyakati tofauti, waliwasilisha malalamiko yao kwangu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Mheshimiwa Makamba alikanusha taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Halima J. Mdee, kuhusu viwanja hivyo na kuniomba nichukue hatua ili Mheshimiwa Halima J. Mdee athibitishe madai yake.

Mheshimiwa Salum Salehe Londa, naye alikanusha tuhuma zilizotolewa dhidi yake na akaniomba nichukue hatua ili Mheshimiwa Halima Mdee, aliyedai kuwa amemkashifu kwa kulitumia Bunge, athibitishe madai yake na akishindwa kufanya hivyo, amuombe radhi vinginevyo atamchukulia hatua nyingine za kisheria.

Baada ya kupokea malalamiko hayo, niliyapeleka kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 71(1) na (2) na Kanuni ya 4(1)(b) ya nyongeza ya 8 ya Kanuni za Bunge toleo la 2007 ili Kamati iyafanyie uchambuzi na kutoa mapendekezo kwangu.

Tarehe 31 Desemba, 2008, kabla ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge haijaanza kazi ya kusikilisha shauri hili, nilipokea barua kutoka kwa mlalamikaji wa kwanza, Mheshimiwa Luteni Yusuf R. Makamba, akiomba kuyaondoa malalamiko yake na kutoa sababu kuwa amekwishayasahau machungu aliyoyapata kutowana na kauli ya mlalamikiwa.

Hoja ya msingi katika suala hili ilikuwa ni kudhibitisha iwapo madai yaliyotolewa na mlalamikiwa Bungeni tarehe 7Agosti, 2008 dhidi ya walalamikaji hayakuwa ya ukweli?

Alipoitwa mbele ya Kamati mlalamikaji wa pili yaani Mstahiki Meya Londa, alikanusha madai yote yaliyotolewa Bungeni na mlalamikiwa na kusisitiza kuwa mchakato mzima wa umilikishwaji wa viwanja hivyo, ulifanywa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kisheria. Aidha, katika kudhibitisha maelezo yake aliwasilisha vielelezo mbalimbali vilivyohusika na umilikishwaji wa viwanja husika. (*Makofi*)

Mlalamikiwa naye alipoitwa mbele ya Kamati, alisema kauli aliyoitoa Bungeni ni ya kweli hawezi kuifuta na hataomba radhi kwa mlalamikaji wa pili wala wa kwanza na katika kuthibitisha madai yake aliwasilisha nyaraka mbalimbali za kuonyesha na kama alivyodai kuthibitisha madai yake aliyoyatoa Bungeni.

Kamati ilibaini pia kuwa taarifa ilioandikwa na Wataalamu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu sakata la viwanja hivyo vya Kawe ilihuisha baadhi ya Maafisa waliosababisha tatizo lenyewe tangu mwanzo na hivyo ikawa haina uzito.

Tarehe 7 Januari, 2009 baada ya Kamati kupokea maelezo na ushahidi wa mdomo na nyaraka kutoka kwa mlalamikaji wa pili na mlalamikiwa, nilipokea barua kutoka kwa mlalamikaji wa pili Mheshimiwa Salum Salehe Londa, naye akaniarifu kuwa anaondoa malalamiko yake.

Baada ya kujtoa kwa walalamikaji wote wawili, Kamati ilikamilisha kazi yake kwa maelekezo yangu hadi hapo walipofikia, niliwaelekeza kwamba hapo walipofikia wakamilishe kilichopo wanilettee. Basi Kamati ilikamilisha kazi yake kwa hatua waliyofikia na kuwasilisha taarifa yake yenye mapendekezo yake kwangu.

Baada ya kuzingatia taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na hususani ushauri walioutoa kuhusu suala hili na kwa kuelewa hali halisi kwamba walalamikaji wote wawili walijiondoka katika kuendeleza malalamiko yao dhidi ya mlalamikiwa, nimeridhika kwamba Mheshimiwa Halima J. Mdee halazimiki kuyafuta madai yake aliyyoatoa Bungeni tarehe 7 Agosti, 2008 wala kuwaomba radhi Bungeni Waheshimiwa Luteni Yusuf R. Makamba na Salum Salehe Londa. Kwa hiyo, maelezo aliyyoatoa Bungeni Mheshimiwa Halima Mdee, tarehe 7 Agosti, 2008, yanabaki kama yalivyo. (*Makofi*)

Naishukuru Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kwa kufanya kazi kwa umakini mkubwa na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Bunge katika kulishughulikia suala hili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nahitimisha kwa kusema kuwa, kwa taratibu za Kibunge, suala hili sasa limefikia mwisho wake, ahsante sana. Nawashukuru sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill 2009]

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

MHE. JOHNSON P. M. MWANYIKA – MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill 2009*], kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa jedwali la marekebisho sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza uniruhusu...

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge Walisikika wakiongea Bungeni*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Kanuni ya 66, inatutaka kama tunawasiliana humu ndani, basi tunong'one, siyo tuongee tu kama hivi inavyoanza kujitokeza. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, endelea.

MHE. JOHNSON P. M. MWANYIKA – MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza uniruhusu kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa yote, kwa kutupa afya njema na kuendelea kutulinda na kutuwezesha kutimiza majukumu yetu na kufikia hatua hii ya leo ambayo ni siku moja kabla ya kufikia mwisho wa Mkutano wetu huu wa bajeti ya 2009/2010 wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuingia katika maudhui ya Muswada, naomba nitumie fursa hii, kuwashukuru watumishi wenzangu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ndugu zetu wa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa ushirikiano mzuri tulionao katika kutimiza majukumu yetu. Pia nawashukuru kwa jinsi ambavyo kwa kipindi kirefu wamekuwa wakifanya kazi zao katika mazingira magumu. Kwa msingi huo, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakisikitishwa na matatizo ya wafanyakazi hao na hivyo mara kwa mara wamekuwa wakiishauri Serikali kuyatafutia ufumbuzi matatizo hayo yanayoikabili ofisi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii, kumshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Serikali kwa ujumla, kwa kuyaona na kuyaelewa matatizo hayo yanayoikabili Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuamua kuyapatia ufumbuzi kwa kadri uwezo wa Serikali ulivyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mwenyezi Mungu awajaze Baraka tele watumishi wote ili waendelee kuchapa kazi na pia waendeleze ushirikiano ili kwa pamoja tuendelee kutoa huduma iliyotukuka kwa Watanzania wenzetu wakiwemo Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya salaam hizo, naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2009, unaokusudia kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge. Katika kufanya hivyo, nianze kwa kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpawa kwa kuupitia na kuuchambua Muswada huu na kwa ushauri mzuri walioutoa. Ushauri huo umetusaidia sana kuboresha na hivyo kuuwezesha kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Tunawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kazi nzuri waliofanya na kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Wilaya, Sura ya 287, Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Miji, Sura ya 288, Sheria ya Mipaka ya Bahari na Maeneo Tengefu kwa Biashara katika Bahari, Sura ya 238 na Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Sura ya 283.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge, ultangazwa katika Gazeti la Serikali tarehe 30 Juni, 2009. Madhumuni ya Muswada huu, ni kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali zilizoainishwa ili kuboresha utekelezaji wake, kwenda na sera ya sasa ya Serikali na pia kuondoa upungufu ambao umedhihirika wakati wa utekelezaji wa masharti ya sheria hizo. Aidha, malengo ya marekebisho haya ni kuweka masharti ambayo yatawezesha kukuza na kulinda dhana ya utawala bora wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu tano, sehemu ya kwanza inahusu masuala ya utangulizi kama vile jina la sheria inayopendekezwa, maelezo kuhusu nia ya mabadiliko na uwiano wa masharti ya vifungu vipya na masharti ya sheria zinazofanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Muswada, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Wilaya katika Fungu la 30, 56, 57 na 146, ili kuhuisha chaguzi za Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Vitongoji na Kanuni zitakazotungwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa na kuweka utaratibu mzuri wa uongozi katika Serikali za Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unapendekeza fungu jipya la 101(e) linalolenga kumpa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa uwezo wa kutengeneza Kanuni zitakazotoa taratibu mahsus za kutengeneza masuala mbalimbali yaliyomo katika sheria na hasa kanuni za kusimamia chaguzi za Serikali za Mitaa hasa Kijiji na Kitongoji.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada huu, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Miji katika fungu la 16,17, 18 na 19, kwa nia ya kuweka taratibu nzuri za chaguzi za Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji zitakazozingatia Kanuni zitakazotungwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Muswada huu pia unapendekeza fungu jipya la 87(e) linalolenga kumpa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa uwezo wa kutengeneza kanuni zitakazotoa taratibu za kutekeleza masuala mbalimbali yaliyomo katika sheria ikiwa ni pamoja na kusimamia chaguzi za Wenyeviti na Wajumbe wa Baraza la Vijiji, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Mitaa na Wenyeviti wa Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Muswada, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mipaka ya Bahari na eneo tengefu la biashara katika fungu la 3, 5,14 na 17 kwa nia ya kurekebisha utaratibu wa upimaji wa eneo la nchi lililo katika Bahari. Utaratibu unaopendekezwa una nia ya kuhuisha sheria zetu na sheria na taratibu za Kimataifa za upimaji wa mipaka ya nchi zinazopakana na Bahari ili kuondoa uwezekano wa migogoro inayoweza kujitokeza pale nchi inapodai haki katika eneo la Bahari au pale inapobainika kuwa kuna uhalifu katika eneo linalomilikiwa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya hifadhi ya Wanyamapori kwa kuongeza kipengele kipyka katika fungu la 23, kifungu cha 3 kwa nia ya kuongeza wigo wa aina ya madini ambayo yanaweza kutafutwa na kuchimbwa ndani ya hifadhi ya wanyamapori pale ambapo itadhihirika kuwa madini hayo ni mengi na yataongeza tija katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa kupitia kwako, naomba Waheshimiwa Wabunge wajadili Muswada huu na hatimaye upitishwe na kuwa sheria ambayo italeta marekebisho ya sheria zinazokusudiwa. Aidha, napenda kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii na kupitia kwako kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Nawashukuru sana na naomba kutoa hoja! (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. RAMADHANI A. MANENO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika, nami kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia salama hatimaye leo tumeweza kufika hapa na kuweza kufanikisha mambo mengi ya msingi tuliyokusudia na kuweza kuyapitisha hatimaye kupata baraka kama hayo ambayo yamepita muda si mrefu. Nikushukuru sana Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, nami pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Chalinze, kwa jinsi wanavyoniunga mkono, nami nawaahidi sitawaangusha siku hadi siku kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyoweza kunipa nguvu na maarifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86, kifungu kidogo cha Tano, toleo la mwaka 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria katika Sheria Mbalimbali (*The Written Laws Miscellaneous Amendment Bill, 2009*).

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati baada ya kukamilisha kazi ya kupitia na kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana katika Ofisi ya Bunge Dodoma tarehe 27 Julai, 2009 ili kupitia na kuchambua Muswada huu. Namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, kwa uwasilishaji mzuri na ufanuzi wa kina mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika katika Kikao cha Kamati, Mwanasheria Mkuu alieleza kuwa Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika sheria zifuatazo:-

- (i) Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Wilaya, Sura ya 287.
- (ii) Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Miji, Sura ya 288.
- (iii) Sheria ya Mipaka ya Bahari na Maeneo Tengefu kwa Biashara katika Bahari, Sura ya 238.
- (iv) Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapor, Sura ya 283.
- (v) Sheria ya Ushuru wa Barabara, Sura ya 220.

Mheshimiwa Spika kwa ujumla, marekebisho haya yanalenga kuwezesha utekelezaji mzuri wa sheria hizo na kuondoa upungufu ambao umedhahirika wakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia iliambiwa kuwa marekebisho hayo yatawezesha utekelezaji wa sheria hizo kuwa sambamba na sera ya sasa ya Serikali. Aidha,

marekebisheso yaliyopendekezo ya lileza kulenga kuweka masharti yatakayowezesha kukuza na kulinda dhana ya utawala bora wa sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kiliarifu Bunge lako kuwa kwa ujumla Kamati imeridhika na maudhui, madhumuni na sababu za Muswada huu kama ilivyoolezwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yoyote ya sheria au marekebisheso ya sheria yanayolenga kuimarisha, kukuza kuendeleza na kulinda dhana ya utawala bora wa sheria yanapaswa kuungwa mkono. Aidha, marekebisheso ya sheria yaliyokusudiwa kuboresha utekelezaji wa masharti yaliyowekwa na sheria, ni jambo la msingi katika utawala wa sheria. Kwa kuzingatia hayo, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kuhusu marekebisheso ya sheria kama ilivyoolezwa na mtoa hoja. Tunaipongeza Serikali kwa kuuleta Muswada huu ambao licha ya kuwa unajitosheleza, pia unazingatia mambo mengi muhimu katika utekelezaji bora wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na maoni kadhaa juu ya lugha na matumizi ya baadhi ya maneno katika Muswada huu. Mojawapo ya maneno ambayo Kamati ilikuwa na maoni tofauti na maneno yaliyotumika kwenye Muswada huu ni Ibara ya 7 ambayo inapendekeza marekebisheso ya kifungu cha 146 cha Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya (*The Local Government District Authority Act*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopitia mapendekezo ya kifungu cha 141(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa, ilizingatia pamoja na mambo mengine, umuhimu wa *misingi* ya sarufi katika tafsiri ya sheria na kushauri kwamba maneno “*all matter*” yasomeke “*all matters*” ili kuleta mantiki iliyokusudiwa. Aidha, katika kifungu cha 149(2) kinachosomeka “*any member or members or all members of the village council*”. Maneno “*or*” na “*all members*” yaondolewe.

Mheshimiwa Spika, mbali na maneno kuhusu matumizi ya lugha na sarufi, Kamati pia inashauri kuhusu mapendekezo ya kurekebisha kifungu cha 19 katika mapendekezo hayo ya aya ya 6. Inapendekeza kuhusu kuchaguliwa kwa Wajumbe wa Baraza la Vijiji kwa namna ambayo idadi ya wajumbe wanawake haitapungua robo ya idadi ya wajumbe wote. Kamati ilishauri kuwa idadi ya wajumbe wanawake itajwe kuwa haitapungua theluthi moja kwa kuondoa maneno “*not less than one quarter*” na kuweka maneno “*not less than one third*” kama ilivyo katika taratibu nyingine za Halmashauri. Hata hivyo, kwa kuzingatia hali halisi ya ushiriki wa akina mama kwenye Mabaraza ya Vijiji, Kamati inashauri kuwa uhamasishaji uendelee ili akina mama wajitokeze kwa wingi katika uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ilipokuwa ikichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisheso uliowasilishwa na mtoa hoja, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwasilisha jedwali la marekebisheso. Katika jedwali la Serikali, alitoa mapendekezo ya marekebisheso katika Sheria ya Ushuru wa Barabara kwa kufanya marekebisheso katika kifungu cha 4 kwa nia ya kuwezesha sehemu ya fedha zinazokusanya kupitia sheria hiyo kutumika pia

katika miradi ya umeme vijijini na miradi mingine ya maendeleo tofauti na sasa ambapo fedha hizo hutumika kwa ajili ya miradi ya barabara tu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, kwa kuzingatia kuwa suala hili lilihitaji uelewa wa kina kuhusu sekta husika, Kamati ilishauri kuwa mapendekezo haya ya Serikali yanayolenga marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Barabara yaendelee kufanyiwa kazi kabla ya kuirekebisha sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (*The Written Laws Miscellaneous Amendment Bill, 2009*). Aidha, naomba pia kumshukuru Mheshimiwa Celine Ompeshi Kombani, Mbunge – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge – Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mbunge – Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wasaidizi wake, kwa maelekezo ya kina yaliyoiezeshwa Kamati kufanya uchambuzi wa Muswada huu kwa umakini mkubwa. Kipekee, nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa umakini wao na michango na kuwezesha hoja hii kufikia hatua hii. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbiri, Mheshimiwa Yussuf R. Makamba, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma.

Mwisho kabisa, nawashukuru Katibu wa Bunge, Dr. Thomas D. Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Charles Mloka, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Athuman Hussein na Eliahika Mtui na watumishi wengine kwa kufanikisha shughuli za Kamati kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofit*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kutumia fursa hii, kushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa mwaka 2009 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6) Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, naomba moja kwa moja nianze kwa kuangalia Muswada huu ulio mbele yetu. Sehemu ya Pili ya Muswada, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Wilaya katika vifungu vya 30, 56, 57 na 146 na pia

kuwekwa kifungu kipy cha 201(a) kinachompa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, uwezo wa kutengeneza Kanuni kwa ajili ya taratibu za chaguzi za Serikali za Mitaa, Kijiji na Kitongoji na Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4 na cha 10 katika Muswada kinachosema kuhusu utaratibu wa kumchagua Mwenyekiti wa Kitongoji kuwa utafuta kanuni na taratibu zitakazowekwa na Mheshimiwa Waziri, Kambi ya Upinzani inaona kuwa ni muda mrefu tangu kuwepo na malalamiko na mapendekezo toka katika asasi, taasisi na vyombo mbali mbali kuwa uchaguzi wa viongozi wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa uwe kwenye mfumo ambaa unasimamizi na Tume ya Uchaguzi na kuondoka katika usimamizi na uangalizi wa Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Mheshimiwa Spika, Muswada huu kwa ujumla wake unadhalilisha malalamiko, ushauri na maoni ya taasisi husika ambazo lengo lake kuu ilikuwa ni kuondoa malalamiko ambayo yangethusiana na kutokutenda haki kwa washiriki kwenye mchakato mzima wa chaguzi hizo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 cha Muswada kinachofuta na kuweka kifungu kipy cha 146, kwanza Kambi ya Upinzani inasikitika kuwa kifungu kinachofutwa ni tofauti na kifungu kilichokusudiwa kufutwa na Serikali. Maneno yaliyoko katika kifungu cha 7 cha mabadiliko yako kwenye kifungu cha 141 na siyo kifungu cha 146. Kifungu cha 146 kinahusu Kijiji cha Ujamaa, kifungu cha 141 kinachofutwa kinasomeka ifuatavyo, naomba kunukuu:-

“A Village Assembly is the Supreme authority on all matters of general policy making in relation to the affair of the Village as such and shall be responsible for the election of the Village Council and the removal from the Council of any or all of the members of Council and for the performance of any other function conferred upon it by or under this Act or any written law”

Mheshimiwa Spika, kama wote tunavyoona Sheria ya mwaka 1982 ilikuwa ya kidemokrasia zaidi kuliko mapendekezo yanayoletwa na Wizara leo. Serikali kwa mapendekezo haya, inaondoa mamlaka kutoka kwa wananchi katika mukutano mkuu kuhusu viongozi wao pale wanapoona kuwa viongozi wao hawakutekeleza wajibu kwa mujibu wa sheria au wameharibu kabisa au wamehujumu fedha na rasilimali za wananchi na wananchi hao wamechukua hatua zote ikiwa ni pamoja na kulalamika kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya, Waziri mwenye dhamana na hakuna hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kama hatua ya mwisho wao wanachukua hatua ya kumuondo, mmoja au wote katika Serikali yao jambo ambalo siyo tu ni la kidemokrasia, lakini ni utekelezaji wa dhana nzima ya *D by D*. Kuondoa kifungu hiki na kurejesha mamlaka ya Waziri ambaye uzoefu umeonyesha hachukui hatua na wala hana uwezo wa kuchukua hatua kwa Vijiji vingi vyenye matatizo katika nchi hii, ni kwenda kinyume na hatua kubwa ya kidemokrasia tulioifikia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta marekebisho yanayoletwa na mabadiliko haya katika kifungu cha 7 kwa nia ya kulinda demokrasia kamili. Hata hivyo, ninakusudia kuleta jedwali la marekebisho ili lengo la demokrasia iliyokusudiwa tangu mwaka 1982 lisithirike na mabadiliko haya. Kifungu hiki kiliwekwa kama hatua ya mwisho pale jamii inapoona ngazi zote husika zimeshindwa kuchukua hatua na rasirimali zao zinaangamia. Kuondoa kifungu hiki ni kuondoa dhamira nzima ya Serikali kusimamia vema rasilimali za Taifa na pia itadhoofisha vita dhidi ya ujisadi na ubadhilifu wa mali za umma.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada huu inayopendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori kwa kuongezwa kifungu kidogo cha (d) katika kifungu cha 20(3) ili kupanua wigo wa aina ya madini ambazo zinaweza kutafutwa na kuchimbwa ndani ya maeneo tengefu ya wanyamapori. Naomba kunukuu kifungu hicho:-

“Any other strategic minerals which can be extracted in significant large quantities” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, suala hili lilishakataliwa katika Kamati ya Maliasili na Mazingira wakati wa kujadili Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaungana na mawazo na maoni ya wadau wote waliojadili sheria hiyo kupinga kifungu hiki ambacho kinataka kuingizwa katika sheria hiyo bila kuhusisha wadau na Kamati ya Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna madini mengi sana, tunayo migodi katika maeneo mbalimbali lakini kutokana na kukosa ujuzi wa kutosha na uelewa juu ya madini yetu, wanaonufaika na madini hayo ya Watanzania ni wawekezaji huku Watanzania tukiambulia mrahaba na kuachiwa mashimo tu. Leo, Serikali inakuja na pendekezo la sheria ya kufungua milango kwa madini ambayo yapo kwenye maeneo ya hifadhi yaanze kuchimbwa. Hili halikubaliki hata kidogo kwani pindi Bunge hili likishapitisha kifungu hiki cha sheria, ni dhahiri kila mtu atatumia mwanya huo kwani kauli ya *any other strategic minerals* ni kauli pana na mtu yejote anaweza kuitumia na kuhalalisha kuchimba madini kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani inaitaka Serikali, kwanza ijenge uwezo wa kutosha kwenye sekta hii na kuweka taratibu zenye tija zitakazowezesha Taifa kunufaika na madini ambayo tayari yamegundulika na yanaendelea kuchimbwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini kabla ya kukimbilia kutafiti madini yaliyoko ardhini kwenye hifadhi zetu. Kambi ya Upinzani inaona huko siyo tu kutaka kuharibu hadhi ya hifadhi zetu na vivutio vilivyopo, bali pia ni kuendelea kuwanufaisha wawekezaji huku Watanzania wakiendelea kubaki maskini. Tukumbuke rasilimali hii ya madini ni mali ambayo ikishachimbwa haijirudii (non-renewable resources) na wakati tunakazana kumaliza madini yote, tukumbuke pia wananchi wa Taifa hili hata wa vizazi vijavyo wana haki ya kunufaika na rasilimali zilizopo ndani ya nchi hii. Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nakusudia pia kuleta *amendment* kwa ajili ya sehemu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nawashukuru wote kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, nimepata wachangiaji sita, sikutarajia, lakini labda niwataje watatu tu kwanza, halafu hawa wengine tutajadiliana kwa karatasi maana tukienda hivi inakuwa shida tena. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mhehimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Kwa hiyo, ni wanne. Nilikuwa nadhani hawa wakiongea, itasaidia, lakini ngoja tuone hali inavyokwenda. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, wakati huo Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe. Mheshimiwa Magdalena, sijui uko tayari!

WABUNGE FULANI: Amechangia kwenye hotuba!

SPIKA: Kweli umechangia kwenye hotuba, basi tuokoe muda.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nilitaka tu nitoe taarifa kwamba ninaomba kuleta *amendment*, inatosha.

SPIKA: Sawa sawa! Sijui Mheshimiwa Dr. Mwakyembe uko tayari? Aah Mheshimiwa Dr. Mwita amerejea, kumbe alikuwa hapa karibu tu!

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Mheshimiwa Spika, nilikuwa msalani! (*Kicheko*)

SPIKA: Aaa, *astakafululah!* Bwana we! Haya endelea, Bwana, endelea! (*Kicheko*)

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mimi nina suala dogo tu katika hii *amendment*, tunapokuja ukurasa wa 32, kipengele cha 17(5) kinachosema:-

“the base-line from which the breath of the territorial sea of the United Republic is measured shall be low-water line or straight base-lines where there are-

- (a) bays or deltas; or
- (b) fringes of islands or reefs,

along the coast of of the United Republic including the coast of all islands, as marked on a large-scale chart or map officially recognized by the Government of United Republic”.

Mheshimiwa Spika, nataka ufanuzi tu kidogo kwa sababu inapozungumza hivi na tunapozingatia kwamba mipaka kati ya Zanzibar na Tanzania *Main Land* ambako ziko hizi *base*, je, tunaweza tukapa ufanuzi, inakuwa *measured* namna gani ili kuweza kupata ufanuzi wa kuweza kutizama, inaanzia wapi kwa mujibu wa sheria hii iliyokuja?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Baada ya hapo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nitangulie kwa kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuwasilisha Muswada huu. Mimi nitaongea kwa kifupi tu, nataka kuongelea hasa Sehemu ya Tano ya Muswada inayopendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori kwa kuongezewa aya moja ili kupanua wigo wa aina ya madini ambayo yanaweza zikachimbwa huko.

Mheshimiwa Spika, sheria hii ya Wanyamapori, ni mpya, tumeitunga juzi tu hapa, leo hii kabla hata mwaka haujapita, tunakuja na marekebisho. Marekebisho yenewe turuhusu wenzetu wanaojua fedha zaidi kutupita sisi, wachimbe Serengeti, waanze kufukua Mikumi, Ruaha na kwa jinsi tunavyojiachia Watanzania kesho tusishangae wakaumaliza hata Mlima Kilimanjaro. Mimi nashindwa kuelewa kama tuko *serious*, tumeshindwa kutawala madini ambayo yapo peupe sio kwenye hifadhi leo tunataka kuingia kwenye hifadhi. Leo hii tunalalamika wananchi wetu wanakufa kwa sumu inayotoka kwenye migodi. Kwa sababu wananchi wetu wana akili wanasesma leo utategemea kesho simba akalalamika, watakufa wanyama wetu kwa kiasi cha kutisha. Mimi ninaomba marekebisho kama haya yangekuja baada ya sisi kufanya marekebisho ambayo tumekuwa tunayadai muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na Kamati ya Bomani hapa, tumependekeza marekebisho *fundamental* kwa ajili ya madini na uhifadhi wa mazingira mpaka leo hatujaona Muswada hapa tunaletewa Muswada hapa kwenda kuchimba Serengeti, kwenda kuchimba Mikumi au Ruaha. Mimi nakataa moja kwa moja, naliomba Bunge hili likatae kabisa, Watanzania watatucheka na kutushangaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 1961, Baba wa Taifa, tunayemheshimu sana, Watanzania tunamuenzi, alitoa kauli ambayo inasomwa duniani kote inakaririwa kwenye Vyuo Vikuu, inaitwa “*The Arusha Manifesto*”. Baba wa Taifa alitamka hayo mwaka 1961. Sawa hayupo duniani lakini Watanzania wa ajabu sana hata kabla haijapita miongo ya kutosha, tumeanza kumsahau, tutakuwa Taifa gani sisi? Baba wa Taifa alisema hivi, namnukuu:-

“*The survive of our wildlife, is a matter of grave concern to all of us in Africa... In accepting the trustship of our wildlife, we solemnly declare that we will do everything in our powers to make sure that our children's, grandchildren, will be able to enjoy this rich and precious inhabitant*” (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakiri mbele yako kwamba siwezi kutafsiri sawa sawa maneno muhimu ya falsafa, mazito aliyyo yatoa Baba wa Taifa lakini kwa kifupi, Baba wa Taifa anasema:-

“Tumekabidhiwa dhamana kubwa ambayo tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha wajukuu wa watoto wetu nao wanakuja kuifaidi hii rasilimali kubwa na yenye thamani.”

Mheshimiwa Spika, kwa kupidisha Muswada huu, leo dhamira ya Mwalimu haitatimia kabisa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwa jinsi tunavyojifahamu sisi Watanzania, sijui tunaogopa kuongea Kingereza, hawa wawekezaji tunakuwa kama tunawaogopa. Mimi nimekwenda Geita, watu waliofika Geita miaka ya zamani, ukifika leo Geita, huwezi kuitambua. Milima haipo, watu wanabisha hii sio Geita kwa nini, kulikuwa na mlima pale umekwenda wapi? Wale watu wana mitambo ya ajabu, inakwangua ile milima utafikiri unakata mkate. Sitashangaa Kilimanjaro isionekane tena pale na wenzangu wa Pemba hapa mtakufa kwa kukosa maji ya kunywa, maji yote ya Pemba yanatoka Mlima Kilimanjaro. Ndio utaalamu unavyosema hivyo, usije ukaanza kulalamika maana tusije tukaingilia tena mjadala wa mafuta hapa. Maji yanayotoka Kilimanjaro ndio mkondo unaingia Pemba, Pemba wana maji safi, watakwangua hawa wenzetu wawekezaji hatutakuwa na tone la maji Pemba na sehemu zingine na tutaiacha nchi hii haina kitu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema maneno mawili tu kwamba madini chini ya ardhi haya ozi, hayazeeki, lakini wanyama wanazeeka, wanyama wanapotea na ni wajibu wetu kutunza kile kinachopotea. Madini unaweza kuyaacha hata miaka 100 au 200 au 300 ijayo watoto wetu, watoto wa wajukuu wa wajukuu watakuja kuchimba.

Mheshimiwa Spika, kama ni lazima tuchimbe basi Serikali ije na Muswada unaonyesha kwamba tofauti ya kuchimba nje ya hifadhi na ndani ya hifadhi, ukichimba ndani ya hifadhi asilimia 95 ya fedha zote zinazopatikana zinakuwa za Tanzania sio sisi tubakiziwe asilimia mbili, haiwezekani, kwa sababu unatuondolea rasilimali yetu ya kudumu. Leo hatuwezi kupidisha hii, mimi nitakataa katakata, nitawashangaa Wabunge watakaopitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, tumesaini mikataba mingi ya Kimataifa ya Kuhifadhi Wanyamapor, sijui tutaiambia nini dunia. Sio hivyo tu, Serengeti na Ngorongoro zipo pale kisheria, lakini hapa sioni marekebisho ya hizo sheria kuweza kuoana na sheria hii ya sasa ambayo tunataka kufanya marekebisho hapa.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu neno la mwisho dogo, naomba Serikali ya Awamu ya Nne ije kukumbukwa huko mbele kuwa Serikali iliyojenga Chuo Kikuu kikubwa kupita vyote Tanzania na Afrika Mashariki, ni sifa nzuri, iendelee ije kukumbukwa huko mbele ni Serikali iliyojenga shule nyingi sana za Sekondari katika

historia ya nchi yetu lakini isije ikakumbukwa kuwa Serikali iliyomsaliti Baba wa Taifa na kuua urithi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa namwita, kuna wale wengine ambao ilikuwa kama kumezea hivi lakini kumbe wana sababu za kuongea wengine wameleta *amendments*, kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Job Ndugai atafuatia Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitaongea kwa kifupi nitakavyoweza.

Kwanza niseme tu kwamba nimeleta *Schedule of Amendment* na nimeshagawa kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na kifungu hiki ambacho Mheshimiwa Mwakyembe amemaliza tu kukizungumzia, sikujua kama Mheshimiwa Mwakyembe naye kumbe alikiona. Nimefanya hivyo kwa kutumia Kanuni ya 86(9) ambayo inasema:-

“Mbunge ye yote wakati wa mjadala huo, anaweza kumshauri mto a hoja afanye mabadiliko katika Muswada, ama mabadiliko ya jumla au yale atakayoyataja Mbunge” na ndio nafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, tulipitisha Sheria mpya ya Wanyamapori tarehe 29 Januari, 2009 katika Bunge hili hili na katika mapendekezo ya Sheria ile mpya ya Wanyamapori ambayo *draft* yake ninayo hapa wakati imetu kama Muswada ilikuwa na kipengele hiki ambacho leo kinapendekezwa kipite kwamba katika utaratibu mzima wa kuchimba madini Sheria ya zamani ilikuwa inakataza kuchimba madini katika hifadhi, Sheria mpya ikaonekana kwamba kuweko utaratibu fulani wa kuruhusu. Wabunge katika Kamati yangu ya Maliasili na Mazingira, Wabunge katika semina tuliyofanya ukumbi wa Msekwa, walikubaliana na suala kama mafuta yapo sawa tuchimbe tukizingatia hifadhi ya mazingira, gesi na *uranium*. Kifungu hiki kilikuwepo cha “*Any other strategic minerals which can be extracted in significant large quantities*” kilikuwepo, Wabunge wakakitaa kabisa hiki kwamba ebu tusimame hapo.

Mheshimiwa Spika, kwanza Sheria mpya ya Madini ije kutokana na mapendekezo mbalimbali ambayo yameshakuja Bungeni, tuione ikoje na hapa kwenye hifadhi zetu tuwe na masharti magumu zaidi na tufaidike zaidi Watanzania. Kipengele kile kikaondolewa, tukaishauri Serikali ichape upya Muswada ule, Serikali ikachapa upya kipengele hiki hakikuwepo na mimi Mwenyekiti wa Kamati nashuhudia hayo.

Mheshimiwa Spika, Januari tarehe 29 leo miezi sita tu, tuna Kanuni humu zinasema angalau tuvumiliane mwaka, angalau tuvumiliane kidogo, tayari imeshakuja *amendment* ya jambo lile lile lakini kilichonisikitisha na kilichofanya nisimame, kwa kawaida siwezi mimi kuleta *amendment unless* ni jambo kama hili, wanajua Kamati yangu mimi na Wabunge walisema nini wakaweka kwenye *miscellaneous* wakapitisha kwa kaka yangu Mheshimiwa Lubeleje, wakarundika kitu kile kile na sentensi ile ile.

Mheshimiwa Spika, kilichonifanya nisimame sio kusema sana ni kusema tu wakati mwengine Bunge lako, jambo limekwama hapa badala ya kukaa tuzungumze linaendelea kupitishwa, siku ya mwisho leo wachache wanaanza kulitazama, wengi tumeona leo, tunasema aah, hii vipi? Kwa hiyo, nimesimama kumwomba Mheshimiwa

Mwanasheria Mkuu wa Serikali akubaliane nasi kwa jambo hili kuna haraka gani?
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nime-*move amendment* na kwa makofi haya nafikiri anaelewa kwamba nitakaposimama kwenye kifungu, nitaungwa mkono. Kwa hiyo, jambo hili alitoe, kama kuna mjadala tuje tufanye mbele kidogo hasa wakati wa mjadala wa Sheria ile ya Madini kwa ujumla na haya mambo ya hifadhi nayo tutayajadili wakati huo na wakati huo basi utapitisha mambo haya.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Ndugai kwa taarifa hiyo. Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka halafu mchangiaji wa mwisho Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu ulioko mbele yetu jioni ya leo wa Marekebisho Mbalimbali ya Sheria ambayo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wametangulia kuanza kujadili.

Mheshimiwa Spika, mimi kimsingi, ni vyema tu nibainishe wazi kwamba eneo nitakalolizungumza ni sehemu hiyo inayohusu sheria tulioipitisha juzi, Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, ninaungana na wenzangu kwa dhati kabisa kwamba katika Muswada wa Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, yako mambo ambayo wadau walikataa na Kamati ya Kudumu ilikataa na sisi Bunge hili tulikataa na mojawapo ni hili la kuchimba madini katika Hifadhi za Taifa. Sasa baada ya marekebisho yaliyofanyika katika Muswada ule Sheria ilipoletwa, taabu ninayoipata ni wasiwasi amba Mheshimiwa Ndugai ameueleza hapa baada ya kwamba tulikataa kipengele hiki kisiingie cha kuruhusu uchimbaji wa madini katika Hifadhi za Taifa ambapo *actually* watu walijaribu sana kuisukuma hili liwepo lakini tukaona kwamba haina mantiki, leo inaletwa katika marekebisho haya madogo ambayo yanaletwa hapa chini ya Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, swali ninalojuiliza ambalo sipati majibu ni nani hasa anayelisukuma jambo hili? Ni siri gani mliyonayo katika hifadhi zetu za Taifa juu ya aina fulani ya madini ambayo yapo na tayari mnaye mtu mgongoni ambaye mnataka kumpa eneo hilo? Tabu tulianayo leo katika nchi yetu ni kwamba tumegawa maeneo mengi kwa wawekezaji na hasa wawekezaji wa kigeni. Ukiangalia katika Wilaya ambazo zina madini kama dhahabu unakuta karibu eneo la Tarafa nzima, Tarafa mbili, Kata nzima inadaiwa kuwepo na *prospecting licence* ya Kampuni moja na unawezu ukakuta Kampuni hizo wala sio Kampuni za wazalendo ni Kampuni za wageni wenye mitaji mikubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kama tungekuwa tunatii na kuheshimu sana kauli za Baba wa Taifa na mimi kwa kweli ningependa tu ninukuu. Mwaka 1958, kabla ya uhuru, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema hivi, naomba kunukuu kwa ruhusa yako.

“Katika nchi kama yetu ambamo Waafrika ni maskini na wageni ni matajiri kuna uwezekano mkubwa kwamba Mwaafrika akiruhusiwa kuuza ardhi katika miaka 80 au miaka michache ijayo ardhi yote ya Tanganyika itamiliwi na matajiri wageni na wenyeji watakuwa watwana. Lakini hata kama wageni wasinge kuwa matajiri litaibuka tabaka la Watanganyika matajiri na wajanja na tukiruhusu ardhi iuzwe kama kanzu katika muda mchache kutakuwepo na kundi dogo la Waafrika wakiwa na ardhi na walio wengi watakuwa watwana katika nchi yao”

Mheshimiwa Spika, mwaka 1958, Baba wa Taifa aliyasema haya, sasa leo kana kwamba hatuoni kabisa kwamba ardhi ya Tanzania inaishia kwenye mikono ya wageni, tunaona kabisa kwamba ardhi ambayo haikuhifadhiwa inaisha, lakini tunataka kujenga hoja ya kuhalalisha hata ardhi iliyohifadhiwa katika Hifadhi za Taifa nayo tutoe kwa wawekezaji ambao kimsingi ni wageni. Sasa hapo ndipo unapojuiliza, juzi tulipitisha Sheria ya Wanyamapori leo sheria iliyopo pamoja na ukame tulionao mifugo, ng'ombe hawaruhusiwi kuingia katika Hifadhi za Taifa, leo tunapozungumza juzi watu wa Longido watatu wamehukumiwa kwa kuingiza mifugo yao Ngorongoro na wako jela sasa, wamehukumiwa kwa kuingiza ng'ombe katika hifadhi kwa ajili ya malisho tu, kwamba huyu ni ng'ombe anahitaji majani kama pofu, kama nyati ili ale majani aondoke zake, Sheria ya Uhifadhi hairuhusu. Lakini kwa kuwa kuna wakubwa wanataka kuwekeza katika Hifadhi za Taifa katika kuchimba madini yaliyoko mle ndani, haya magreda na mitambo ya kwenda kuchimba kwenye hifadhi, hayaharibu uhifadhi ila ng'ombe anayefanana na pofu anaharibu? Unajiuliza, hivi watu wanaoleta marekebisho haya, watu wanaolishupalia hili, kuna jambo ambalo linawasukuma na nadhani *pressure* sio ya kawaida, sasa ni ipi sijui. Ila mimi ninachotaka kusema, Bunge hili lilitokana na Watanzania, lisikubali kabisa, Muswada huu tuukatae, tuweke rekodi kama kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika jambo ambalo sitakusahau maisha yangu yote na sitalisahau Bunge hili ni juu ya umadhubuti wa Bunge hili kutimiza wajibu wake wa msingi wa kuishauri na kuisimamia Serikali bila ya kutazama sura ya nani anayekosolewa katika mambo ya msingi kwa maslahi ya Taifa. Nikiacha mambo haya yaende kienyeji, kienyeji, hadhi (*integrity*) ya Bunge hili na Serikali hii itatiliwa mashaka na mimi kama sehemu ya Bunge hili, nisingependa tufike mahali tukatiliwa mashaka.

Mheshimiwa Spika, umeliongoza Bunge hili kwa viwango na kwa kasi inayostahili. Hata leo ukipigwa madongo na vigazeti maalum viliivoandaliwa kwa nia ya kuwabeba mafisadi na kupotosha ukweli, sisi Wabunge wa Bunge lako tutasimama kidete kukuunga mkono wewe na Watanzania wanajua hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anayetetea maslahi ya nchi, kamwe hawezi kukataliwa na Watanzania wanyonge watamuunga mkono mpaka mwisho. Walatini wanasema: “Sauti

ya Watu, sauti ya Mungu” na Bibilia inasema: “kitakachofunguliwa duniani na mbinguni imefunguliwa, kitakachofungwa duniani, kitafungwa na mbinguni”. Tuwe na msimamo kwenye mambo ya msingi. Tutawaudhi wachache lakini Watanzania na historia itaandika kwamba tumefanya mambo mema. Ni jambo la kushangaza kwamba hii ni nchi ya pekee ambapo watu wanaokwenda kinyume na mambo ya msingi wanawenza kupewa nafasi ya kutamba na kuharibu majina ya watu ambao ni waadilifu na wachapakazi kama Samwel Sitta.

Mheshimiwa Spika, kuna wengine leo ungewashusha Kariakoo, njoo baada ya robo saa, utakuta hawana hata nguo moja kutohana na rekodi yao ambavyo sio safi. Sasa Bunge hili na Serikali yetu lazima iendelee kujenga uhalali kwa Watanzania, tukipita kwa wananchi, tufungue vioo, tushangiliwe, tusifike mahali pa kuingia kwenye magari *tinted* kwa kuhofia kwamba misimamo yetu katika uso wa wapiga kura wa Tanzania ni mzigoo.

Mheshimiwa Spika, juzi niliona gazeti moja katika miiongoni mwa magazeti yanayokutukanatukana Mheshimiwa Spika na mimi nikafanya tathmini, likasema mimi na mwenzangu Felix Mrema tunapumulia mashine, sababu anaungwa na Wamasai wazee wa mila lakini ana tatizo moja amejiharibia katika msimamo kwenye masuala ya Kitaifa. Suala gani la Kitaifa kupiga vita ufisadi ndio unajiharibia au unajijengea? Sasa nikasema pengine ningependa kumwalika Mhariri wa gazeti hilo na mmiliki wa gazeti hilo pale Simanjiro ili washuhudie jinsi wananchi wa Simanjiro wasivyoupenda ufisadi na ambavyo hawawezi kamwe kunikataa kwa sababu ya kuwa na msimamo kwenye mambo ya msingi. Bunge hili liwe na msimamo kwenye mambo ya msingi, tukatae yale ambayo hayana tija kwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, siungi mkono hoja mpaka marekebisho haya yafanyike ya kuondoa kifungu hiki. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, mwongozo!

SPIKA: Mmh, Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo wako, suala ambalo linajadiliwa hivi sasa na kuleta mjadala mkali sana halikupita kwenye Kamati ya Kisekta na ndio sababu tunaona mjadala huu kama lingepita kwenye Kamati ya Kisekta kwa vyovyyote vile lingepata ushauri wa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa hili sasa kwamba lirudi kwenye Kamati ya Kisekta, lakini na kwa hapo baadaye, *Miscellaneous Amendment* inapoletwa na inapokuwa ina masuala ya Kisekta isipelekwe kwenye Kamati ya ujumla kwa sababu ndio inapelekea baadhi ya maamuzi kufanyika bila Kamati za Kisekta kuweza kuyazingatia. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako katika suala hili. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninachotakiwa kutoa mwongozo hapa ni kuhusu utaratibu wa mchakato wa kuitisha Miswada hii ya Sheria Mbalimbali. Hadi sasa hatujabadili utaratibu, utaratibu uliopo ni huu huu tunaofuata kwamba Kamati ya

Katiba, Sheria na Utawala, ndiyo inazingatia Miswada hii, sasa hatuwezi kubadili ghafla hivi sasa. Ningeshauri pendekazo hili zuri lisisimamishe Muswada huu badala yake tumalize hatua hii, lakini kwa kuwa ni Bunge ambalo linakwenda na kupata uzoefu totalitazama hilo ili tuweze kubadilisha na siku za usoni iweze kukaa vizuri zaidi. Lakini kwa sasa napenda tuendelee tu na mimi nadhani, sijui, hivi kweli suala hili Serikali italifikisha mpaka tupige kura kweli? Loh, nitashangaa sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):
Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ufanuzi kidogo kuhusu suala la *Village Assembly* au Mkutano Mkuu wa Kijiji pamoja na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kama utakumbuka katika Bunge lako Tukufu lililopita, ulinitaka nitoe ufanuzi wa mabadiliko ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Nilitoa *briefing* kuhusu mambo mbalimbali na mabadiliko mbalimbali ambayo yalifikiwa na wadau mbalimbali ikiwa pamoja na Vyama vya Siasa uliofanyika kule Morogoro. Kwa hiyo, mambo yaliyokubalika, nililieleza Bunge lako kwa Wabunge wote kwenye kikao cha *briefing* kule ukumbi wa Pius Msekwa na mabadiliko haya nafikiri kila Mbunge ameyahamtu ndiyo chimbuko la kuleta Mabadiliko ya Sheria hii kutokana na mabadiliko tuliyofanya katika sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, mimi nilitegemea kwamba baada ya ule Mkutano wa Morogoro, Vyama vya Siasa vyote 17 vilisaini yale makubaliano, makubaliano hayo ni pamoja na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa, vingetoa elimu hiyo kwa wengine. Hili likubalika na vyama vyote vya siasa.

La pili, tulikubaliana kabisa kimsingi kwamba kuanzia sasa, uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kuchagua Mwenyekiti wa Kijiji utafanyika katika Kitongoji na si katika Kijiji. Kwa hiyo, Mkutano wa Kijiji pale (*Village Assembly*) ile bado ni *supreme*, bado kazi zake ziko pale pale isipokuwa kwa ajili ya uchaguzi tu, kwa sababu ule uchaguzi tumeupeleka kwenye Kitongoji na huu uchaguzi ni wa msingi, tumeupeleka kwenye Kitongoji kwa madhumuni ya kupata wapiga kura wengi zaidi. Sasa siku ya uchaguzi, uchaguzi wote utafanyika katika ngazi ya Kitongoji.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Kitongoji, naomba nitoe ufanuzi kwamba siku ya uchaguzi kutakuwa na maboksi matatu. Moja kwa ajili ya Mwenyekiti wa Kitongoji, la pili kwa ajili ya Mwenyekiti wa Kijiji na boksi la tatu ni kwa ajili ya wale Wajumbe wa Serikali ya Kijiji, wale Wajumbe 25. Matokeo ya Mwenyekiti wa Kitongoji yatatorewa pale pale kwenye Kitongoji. Mwenyekiti wa Kijiji kura zake zitahesabiwa zitapelekwa kwenye Makao Makuu ya Kijiji pale. Pale wata-combain na matokeo ya Vitongoji vingine, kwa hiyo, matokeo yatangazwa katika ngazi ya Kijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hiyo *amendment* ambayo imeletwa na dada yangu Mheshimiwa Sakaya ya kusema kwamba labda tumenyang'anya madaraka ya Mkutano Mkuu wa Kijiji, hapana hatujayatoa ni kwamba kazi zote zitakuwa pale pale isipokuwa

kwa huo uchaguzi kwa madhumuni ya kwamba uchaguzi utafanyika katika Kitongoji. Kwa hiyo, hilo tu naomba niliweke wazi kwamba hatujanyang'anya hayo madaraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waziri mwenye dhamana wa Serikali za Mitaa kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa, bado liko pale, tulikubaliana kabisa kimsingi kwamba liendelee mpaka hapo sheria zitakapobadilishwa, Sheria ya Uchaguzi pamoja na Sheria za Serikali za Mitaa ambazo zinamtambua Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kusimamia uchaguzi. Mpaka sasa hivi ziko pale pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliona tu nitoe ufanuzi kwa madhumuni ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri imesaidia sana sana.

Serjent at arms, sijui leo taa zikiwa hivi sasa tunaendeshaje shughuli hizi. *Engineering*, nadhani kuna tatizo huko bado zile *main lights* hazijawaka, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wako gizani tu. Ebu shughulikieni hilo, tunavumilia tu sasa.

Sasa namwita mtoa hoja. Mheshimiwa Mwansheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa mchango wao walioutoa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue kwa kuwataja Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Celina Kombani.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nifafanue na kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Hoja iliyotolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti, aliyewasilisha hoja hii na mambo yote aliyoyazungumzia, tumeyazingatia na kuyaleta kwenye marekebisho ambayo nadhani Waheshimiwa Wabunge wanayo.

Mheshimiwa Spika, kwenye mchango wa Mheshimiwa Sakaya, aliyoyazungumza, ni kama yale ambayo amezungumza Mheshimiwa Celina Kombani, juu ya kifungu kile cha 146. Kwenye mchango wake alisema tulikosea kuweka kifungu kile katika haya marekebisho tunayoyaleta mbele ya Waheshimiwa Wabunge. Fungu aliloweka yeye ni fungu 141, fungu linalofanyiwa marekebisho ni 146 na si 141. Kwenye Sheria ambayo tuliitaja pale ambayo ilijadiliwa mwaka 2002, ataona kwamba fungu lile lililoelezwa pale ndilo ambalo linahusika katika eneo lile ambalo tumelisema kwenye marekebisho yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Village Assembly* kuhusika kwenye uchaguzi, Mheshimiwa Kombani ameshalielezea, kwa hiyo, siwezi kulirudia tena.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuongeza madini ambayo yanaweza kuchimbwa kwenye Mbuga za Wanyama, Serikali yetu ni sikivu, imesikia hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Hivyo, napenda kukujulisha kwamba Serikali imeondoa lile fungu ambalo lilikuwa linapendekezwa lifanyiwe marekebisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja aliyoitoa Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, naomba nimrejeshe kwenye Katiba ya Nchi. Katika Katiba ya nchi, iko wazi kabisa. Kwenye Ibara ya Kwanza inasema:-

“*Tanzania ni nchi moja ni Jamhuri ya Muungano*”.

Ibara ya pili inasema:-

“*Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar, na ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo.*”

Mheshimiwa Spika, kama ni kupima eneo la ukanda ule wa biashara basi inaanzia kwenye mahali bahari inapogota ambapo kwa Tanzania ni Tanzania Bara na hiyo ya Visiwani. Nadhani Katiba ya Nchi inajieleza vizuri tu. Kwa hiyo, namwondo hofu kwamba hakuna lolote baya ambalo lilitendeka katika mapendekezo ya marekebisho tulioleta mbele yako.

SPIKA: Samahani, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 28(8), inaniruhusu kwamba ikisalia dakika kumi kabla ya saa mbili kasarobo, Bunge au Kamati ya Bunge Zima ama Kamati ya Matumizi bado haijamaliza shughuli zake, Spika, anaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kulihoji Bunge. Kwa hiyo sasa, nafanya hivyo ili tumalize Muswada huu, endelea.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kutoa hoja. (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana mtoa hoja kwa maelezo mafupi, clear na zaidi yanayozingatia hisia za Waheshimiwa Wabunge, Katibu! (*Makofi*)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009
[*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill 2009*]

MWENYEKITI: Katibu, tuitishe kwenye vifungu.

Sehemu ya 1

Ibara ya 1
Ibara ya 2

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Sehemu ya 2

Ibara ya 3
Ibara ya 4

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 5

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 6

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 7

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 8

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Sehemu ya 3

Ibara ya 9
Ibara ya 10

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 4

Ibara ya 15

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18

Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 5

(Sehemu ya Tano yote ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, taarifa!

MWANASHERIA MKUU: Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge Zima, imeupitia Muswada wa Sheria, Ibara kwa Ibara na imekubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Marekebisho katika Sheria Mbalimbali wa mwaka 2009 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill 2009*], kama ulivyorekebishwa, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa*
Mara ya Tatu na Kupitishwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, baada ya hatua hiyo, sasa Muswada umekamilika na kama kawaida utapelekwa katika hatua zinazofuata. Nawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya, uchangiaji ulikuwa makini. Sasa nitoe matangazo.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Tafrija, anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo saa mbili usiku, kutakuwa na tafrija ya kujipongeza kwa kukaribia kumaliza, kwa sababu tunamaliza kesho maana msijekufiria tunamaliza leo halafu mtu ukaendelea, kesho ukaamka hovyo hovyo. Bado kesho kuna kazi ya kumalizia Mkutano wa 16 wa Bunge na tafrija hii itafanyika katika viwanja sijui vipi, nikuruhusu utoe ufanuzi kidogo.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, kwa heshima ya Bunge lako na kwa heshima ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa heshima ya Waheshimiwa Wabunge wote, naomba kutoa taarifa kwamba, shughuli hiyo imepangwa ili Waheshimiwa Wabunge baada ya kumaliza kazi nzito kabisa ya takribani miezi miwili, waweze kupata nafasi ya kushauriana na kutafakari yaliyojiri. Shughuli hii itafanyika mara baada ya kuahirisha shughuli hizi za Bunge leo jioni hii katika viwanja vya Bunge, vile viwanja vyetu vya kawaida vya shughuli za sherehe za Bunge si viwanja vipyta, ni viwanja vile ambavyo tumekuwa tukivitumia siku za nyuma na hasa shughuli iliyofanyika mara ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kukushukuru wewe na Ofisi yako, kwa kuamua kugharamia shughuli hii ya leo. Lakini tuwashukuru wenzetu wa *TBL* kwa kushirikiana na Ofisi yako katika kugharamia shughuli hii. Naomba kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote tuweze tutafakari yale yaliyojiri katika miezi hii miwili kabla hatujaenda kuwatumikia tena na kufanya kazi zetu za kiuwakilishi katika Majimbo yetu. Mambo yote yameandaliwa na nadhani kutakuwa na usiku mwingine mzuri wa kuhitimisha shughuli hizi za Bunge kabla hazijaahirishwa rasmi siku ya kesho.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana, nashukuru kwa hilo. Mwaliko huo mmekwishausikia, kwa hiyo, ni vizuri tukahudhuria.

Sasa nitamwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Masuala ya Muungano ama Mwanasheria Mkuu, atoe hoja ya kuahirisha Bunge ili tuweze kusikia *motion* ya Mheshimiwa Mbunge mwenzetu.

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO:
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe mpaka kesho saa tatu asubuhi.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimepokea hoja ya *adjournment* na nitamwomba sasa mwenzetu aweze kuiwasilisha, Mheshimiwa Dr. Mzindakaya!

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kukushukuru wewe mwenyewe, kwa kunipa nafasi hii ili nitumie kifungu cha Kanuni za Bunge, namba 50 (1) na (2). Napenda kutoa maelezo binafsi kuhusu ufanuzi wa mchango wangu na namna ulivyonukuliwa vibaya na vyombo vyatuhari pale nilipotoa mchango wangu wakati wa Bajeti ya kujadili Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Sina haja ya kukisoma kifungu hicho kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wameshakuwa wazoefu, Kanuni hiyo inaeleweka.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, nilitoa hoja zangu ambazo kwa bahati mbaya zilinukuliwa vibaya na baadhi ya magazeti. Magazeti hayo ni:-

- Gazeti la Nipashe la Tarehe 23 Julai, 2009 ;
- Gazeti la Tanzania Daima la Tarehe 23 Julai, 2009 ;
- Gazeti la Mwananchi la Tarehe 23 Julai, 2009 ;
- Gazeti la Habari Leo la Tarehe 23 Julai, 2009 ; na
- The Guardian la Tarehe 23 Julai, 2009

Mheshimiwa Spika, gazeti la Nipashe, katika ukurasa wake wa tatu, lina kichwa cha Habari kinachosomeka kama ifuatavyo:-

“Dk. Mzindakaya: Nilihalalisha Magendo Kigoma.”

Aidha katika aya ya kwanza, Mwandishi wa gazeti hilo, Bw. John Ngunge, anasema:-

“Mbunge wa Jimbo la Kwela (CCM), Dkt. Chrisant Mzindakaya, amesema akiwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma miaka 23 iliyopita, alihalalisha biashara ya magendo”.

Katika aya ya nne, anaendelea kusema nanukuu:-

“(Kwa maana ya mimi Mzindakaya) Desemba 1986, alipoteuliwa na Rais Ali Hassan Mwinyi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, aliagizwa pamoja na mambo mengine kudhibiti biashara ya magendo Mkoani humo”.

Aya ya tano, inasomeka hivi kwa kuendeleza aya ya nne:-

“Baada ya kufika Kigoma, nilimwambia Rais, magendo Mkoani hapa yana umri mkubwa kuliko mimi, siwezi, nikahalalisha”.

Hivyo mtu akiisoma habari hii, anaridhika moja kwa moja kuwa Mheshimiwa Mbunge alihalalisha biashara ya magendo ambayo si halali.

Mheshimiwa Spika, ukilinganisha maelezo ya Gazeti la Nipashe na *Hansard* ya tarehe 22/7/2009 ambayo inakumbukumbu ya mchango wangu inasema hivi:-

“...Mimi nilipokwenda Kigoma, Wabunge wa Kigoma ni mashahidi. Rais alinituma, akasema kaondoe magendo, nikakaa miezi mitatu nikarudi; nikasema Rais, magendo ya Kigoma yana umri mkubwa kuliko mimi, nipe muda. Nikahalalisha biashara, eeh! Nikahalalisha na tulifanya biashara kubwa kweli...”

Mheshimiwa Spika, neno nilihalalisha magendo halipo katika *Hansard*, kwa hiyo, mwandishi aliweka maneno yake.

Mheshimiwa Spika, Gazeti la Tanzania Daima, ukiachilia mbali kichwa cha habari cha gazeti hili, ukurasa wa pili kinachosema, “*Mzindakaya alipua Mawaziri, Makatibu Wakuu Bungeni*”, lipo jambo ambalo ni tofauti na lilivyo katika *Hansard* na linahusu hoja yangu binafsi.

Katika aya ya tano, gazeti hili linasema hivi:-

“Mzindakaya aliliambia Bunge kuwa, anakusudia kuwasilisha hoja binafsi katika Bunge lijalo kuhusu wenye viwanda wanaosindika mafuta kutoingia mkataba na makampuni ya mafuta ya kula bali Mikoa inayozalisha mafuta hayo”.

Pia mwandishi wa makala kuhusu jambo hili, ameninukuu katika aya ya saba kama ifuatavyo:-

“Bunge lijalo nitaleta hoja kuhusu suala la mafuta, hoja hiyo inahusu watu wenye viwanda wanaosindika waisiingie mkataba na makampuni yanayoleta mafuta, nitakuja na takwimu zinazoonyesha fedha ngapi Serikali ilizowasamehe wauza mafuta zingewenza kuwasaidia watu wengine.”

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *Hansard*, hakuna kifungu cha maneno kama kilivyo hapo juu kwani mwandishi kaonesha kama ni nukuu ingawa yapo baadhi ya maneno niliyotamka.

Mheshimiwa Spika, *Hansard* katika aya ya tatu, inasema hivi:-

“...mimi nakusudia Bunge lijalo kuleta hoja kuhusu suala la mafuta, kwa sababu hata kule Wizara ya Fedha...Pili, hoja yangu itahusu kusema ni kwa nini wenyewe viwanda wanaosindika mafuta, wasiingie mikataba na Mikoa ya kulima mbegu za mafuta?”

Mheshimiwa Spika, neno kuhusu kuleta hoja yangu, linajitokeza tena katika *Hansard*, aya ya mwisho, inasema:-

“Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya maelezo haya, naomba niseme tena kwamba nitajiandaa ili Bunge lijalo nilete hoja ya namna ya kujitegemea...”

Hivyo utagundua kuwa maneno yaliyoko kwenye nukuu ya Mwandishi yasemayo “waisiingie mkataba na makampuni yanayoleta mafuta” hayapo katika *Hansard* bali ni nyongeza tu ya Mwandishi ambayo inaweza kuniletea mtafaruku na jamii.

Mheshimiwa Spika, gazeti la Mwananchi chini ya kichwa cha habari “*Mzee wa mabomu aibuka tena*”, Mwandishi wa makala hayo, ndugu Kizito Noya, katika aya ya kwanza, anasema hivi, nanukuu:-

“Mbunge wa Kwela, Chrisant Mzindakaya, amewashutumu Makatibu Wakuu wa Wizara kuwa ndio wanaoifanya nchi iendelee kuwa maskini na tegemezi kutokana na kutowapa ushauri mzuri Mawaziri. Atishia kupeleka hoja binafsi Bungeni kuitaka Serikali ionyeshe mipango ya nchi kujikwamua na umasikini. Alisema Makatibu Wakuu wa Wizara wanachangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa umasikini nchini kutokana na kushindwa kuwashauri Mawaziri mambo ya maendeleo.”

Mheshimiwa Spika, maneno yaliyoko katika aya hii hayaendani na niliyotamka katika *Hansard*. Sikusema Makatibu Wakuu ndiyo wanaoifanya nchi iendelee kuwa masikini na tegemezi bali nilichokisema ni kuwa Makatibu Wakuu watembelee Mikoa ili kufahamu vizuri nchi kijiografia ili wawze kutoa ushauri ipasavyo kwa Mawaziri na wala sikuwashambulia Mawaziri kwa lolote isipokuwa nilitambua juhudhi wanayofanya ya kutembelea Mikoa.

Aidha kuhusu hoja yangu binafsi haihusu Serikali kuonyesha mipango ya nchi kujikwamua na umasikini bali kama inavyosomeka katika *Hansard*, hoja inahusu suala la mafuta ya kula na mikataba baina ya wenyewe viwanda vya mafuta ya kula na Mikoa inayozalisha mbegu za mafuta. Wote tunafahamu kuwa Mipango ya Serikali katika kujikwamua na umasikini imejikita katika MKUKUTA, MKURABITA na kadhalika ikiambatana na mifuko kama TASAF na mingineyo. Hivyo basi, katika hali hiyo, Mwandishi ameipotosha jamii kwa kuandika mambo ambayo sikuyasema.

Mheshimiwa Spika, Gazeti la Habari Leo, gazeti hili pia limegusia hoja binafsi niliyosema kuwa nakusudia kuleta kwa kueleza kuwa:-

“Mbunge wa Kwela Dk. Chrisant Mzindakaya (CCM) ameibuka na kuahidi kupeleka Bungeni hoja binafsi kuhusu kujitegemea, akijikita kuhusu kuondolewa kwa ushuru wa mafuta ghafi na mawese nchini na kuzagaa kwa juisi za rangi zenye kemikali”.

Mheshimiwa Spika, hapa Mwandishi anazungumzia hoja ya kujitegemea lakini haoneshi wazi kujitegemea katika maeneo gani. Bahati mbaya, amechanganya na mambo mengine kama inavyojonesha hapo juu, akijikita kuhusu kuondolewa kwa ushuru wa mafuta ghafi, hali hii inaweza kumchanganya msomaji katika kuelewa hoja ya kujitegemea inahusu nini hasa; ushuru wa mafuta ghafi, mawese au juisi za rangi zenye kemikali?

Mheshimiwa Spika, haya yote yanaonyesha upungufu na uwezo mdogo wa Mwandishi wa gazeti hilo katika kuandika na kufafanua maeleo yatolewayo na Waheshimiwa Wabunge Bungeni kwa faida ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Gazeti la *The Guardian*, lenyewe kuhusu hoja yangu binafsi linasema:-

“Mheshimiwa anakusudia kuleta katika Bunge lijalo hoja kuhusu kujitegemea kwa chakula (Mzindakaya said, he would table a private motion in the next Bunge session to ask the government to reintroduce self-reliance in food production).”

Mheshimiwa Spika, hapa panaweza kujitokeza tofauti ya kiuelewa kwani *Hansard* inazungumzia hoja kuhusu kujitegemea kwenye mafuta ya kula, hapa Mwandishi, Ndugu Patrick Kisembo, anazungumzia kuwa hoja itahusu kujitegemea kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, mafuta ni sehemu ya chakula na kwa maana hiyo chakula ni dhana pana (*Broad term*). Ukitazama katika *Hansard*, hoja itazungumzia mafuta ya kula na namna tunavyoweza kujitegemea katika hilo na si kuendelea kuagiza toka nje. Hapa pia Mwandishi hakuwa makini katika uandishi wake.

Mheshimiwa Spika, jana Bunge lako Tukufu lilikamilisha kupitisha hotuba za Wizara zote. Wabunge wote tuliwapongeza Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalam wao, kwa kazi nzuri wanayofanya. Makatibu Wakuu na Serikali yetu ya Awamu ya Nne, wanafanya kazi vizuri na kwa uzalendo mkubwa sana kwa nchi yao. Kutokana na juhudzi zao na utaalam wao ndio wamesaidia sisi kufikia mafanikio tunayoyana.

Mheshimiwa Spika, nchi zilizoendelea mfano Uingereza, Waandishi wanaoandika majadiliano Bungeni, ni wale wenye utaalam mahususi juu ya kazi hiyo na waliochunguzwa na kuhakikiwa kwa umakini (*vetted*) katika utaalam huo.

Mheshimiwa Spika, najua kuwa, magazeti kama moja ya vyombo vya habari, yanafanya kazi nzuri ya kuelimisha umma ikiwa ni pamoja na kuwapa haki ya kupata habari hususani zihusozo Bunge kwa ujumla wake. Pia natambua vyombo hivi vina

mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi kisiasa, kiuchumi na kijamii lakini vyombo hivi, visipotumika vyema kwa maana ya kufuata misingi yake ikiwa ni pamoja na kusimamia haki na ukweli katika kazi zao, basi huenda vikaharibu haiba ya Mbunge au Bunge kwa ujumla wake kwa Jamii. Hivyo, ni vema Wahariri wakaleta Waandishi wenye ujuzi na masuala ya Kibunge ili kuzuia upotoshaji kama huu na kujenga maelewano mazuri baina ya wananchi na Bunge lao.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kwa uchambuzi huo wa magazeti niliyoyataja hapo juu ambayo hayakunitendea haki hata kidogo na kutokana na upotoshaji wa maelezo yangu katika magazeti hayo, nimeona ni vema kuleta maelezo haya binafsi kwa lengo la kuwaelimisha ndugu zetu Waandishi wa Habari kuwa si vema kupotosha maelezo yatolewayo na Mbunge ye yote ndani ya Bunge wakati wa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge ni chombo kinachoheshimika katika jamii kwa kutetea maslahi ya wananchi na ili kunitendea haki, naomba Wahariri Wakuu wa Magazeti yaliyopotosha maelezo yangu, watoe katika magazeti yao, kurasa za kwanza (*front page*), maelezo haya niliyotoa Bungeni na hivyo kuufanya umma upate uelewa sahihi wa yale niliyozungumza tarehe 22 Julai, 2009 na hii itasaidia kuimarisha mahusiano mazuri kati yetu na wao pamoja na wananchi wote kwa ujumla waliosoma habari hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Nashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mzindakaya, ametumia nafasi yake katika Kanuni kuweza kutoa hayo maelezo binafsi na sasa tumefikia mwisho wa shughuli zilizopangwa leo. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi hapo kesho.

(*Saa 01.55 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumamosi
Tarehe 1 Agosti, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)